**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**KIKAO CHA SITA – TAREHE 6 FEBRUARI, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE DR. LUCAS J. SIYAME):**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini kwa mwaka 2005

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka 2005 (*The Annual Report and Accounts of the Parastatal Pensions Fund for the Year 2005)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania Kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2006 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Communications Regulatory Authority for the Year ended 30$^{th}$ June, 2006).*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijafanya hiyo shughuli uliyoniitia hapa, naomba kutumia nafasi hii kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba nimetii amri ya Mheshimiwa Spika ya kumwomba radhi Mheshimiwa Shibuda. Lakini kutii kwangu hakuondoi ukweli kwamba kama bilioni 90 wakulima walizokatwa zingejenga shule tusingekuwa na haja ya kuweza kuwachangisha wananchi wakati………

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo naomba unisikilize. Maagizo ya Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni kuomba radhi na sio kuendeleza mjadala tena. Ninaomba

uishie katika maagizo ya Mheshimiwa Spika, hayo mengine kama unataka kuyaendeleza utayaleta kwa utaratibu unaotakiwa.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Wananchi wameshanisikia. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kwa ruhusa yako kuwasilisha kwenye meza yako Tukufu. Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2006.

**MWENYEKITI:** Tunashukuru Mheshimiwa John Cheyo, lakini mtu mzima huwa ana utaratibu wake wa kuomba radhi. Nafikiri hiyo ndiyo ilikuwa ni utaratibu wako. Mheshimiwa Shibuda amesikia. Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee na Taarifa za Kamati. Naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU - MAKAMU MWENYEKITI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:-**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2006.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na agenda inayofuata kwa heshima na taadhima naomba nitambue leo uwepo wa Mheshimiwa Samwel Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki, akiwemo ndani ya ukumbi wa Bunge katika kiti chake cha Ubunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu ni mara chache sana Mheshimiwa Spika huwa tunakuwa naye akiwa amekalia kiti chake cha Ubunge. Kwa hiyo, huenda leo ana agenda maalum kwa niaba ya wapiga kura wake. *(MakofiKicheko)*

Mheshimiwa Spika, tunakukaribisha sana ili uweze kuwawakilisha wapiga kura wako namna ya mkao wa Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 69

### Masoko ya Mitaji na Hisa

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Masoko ya Mitaji (*Capital Markets*) na Masoko ya Hisa (*Stock Exchange)* ni sehemu muhimu sana katika sekta ya fedha ya nchi yoyote; na kwa kuwa, masoko hayo huwezesha kampuni zinazomilikiwa na watu wengi (*Public Companies*) kupata mitaji mikubwa kwa masharti nafuu zaidi kuliko mikopo ya benki:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani masoko hayo yanatumiwa na Kampuni za hapa Tanzania katika kupata na kukuza mitaji yao?

(b) Je, ni Kampuni ngapi zinazochimba Madini hapa nchini zimesajiliwa na kupata sehemu ya mitaji yao katika masoko ya mitaji na hisa hapa nchini Tanzania?

(c) Je, Masoko ya Mitaji na Hisa hapa nchini yanakabiliwa na matatizo gani katika kukuza matumizi ya masoko hayo na Serikali inachukua hatua zipi ili kukabiliana na matatizo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Masoko ya Mitaji na Hisa, yametumiwa na Kampuni za Tanzania kupata na kukuza mitaji kama ifuatavyo:-

| KAMPUNI | THAMANI WAKATI WA KUJIANDIKISHA (SHS. BILIONI) | THAMANI TAREHE 5/2/2007 (SHS. BILIONI) |
|---|---|---|
| 1. TOL | 3.20 | 10.56 |
| 2. TBL | 130.00 | 465.99 |
| 3. TATEPA | 3.50 | 6.72 |
| 4. TCC | 41.00 | 148.00 |
| 5. SIMBA CEMENT | 19.10 | 62.40 |
| 6. DAHACO (SWISSPORT) | 8.10 | 24.48 |
| 7. TWIGA CEMENT | 78.30 | 125.95 |
| **JUMLA** | **283.00** | **844.10** |

Aidha, Kampuni kutoka nje ya nchi zilizojiorodhesha *(listing)* katika Soko la Mitaji na Hisa kama ifuatavyo:-

- *Kenya Airways Corporation* ina mtaji wa shs. 738.6 bilioni;

- *Jubilee Holdings* (*Jubilee Insurance*) shs. 211 bilioni; na

- *East African Breweries Ltd.* (Kenya) shs.3,112.0 bilioni.

Makampuni hayo matatu ya Kenya yana jumla shs. 2,267.6 bilioni.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi, hakuna Kampuni ya Madini iliyosajiliwa au kupata sehemu ya mitaji hapa nchini kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam. Kampuni nyingi za kigeni zimeorodheshwa katika masoko ya mitaji ya nchi zinakotoka na kupata mitaji huko huko. Jukumu letu kama Serikali ni kuwashawishi waone faida ya kujiorodhesha hapa nchini. Mara nyingi kama hawahitaji mtaji hawashawishiki kwenda kwenye Soko la Mitaji.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya matatizo yanayoyakabili Masoko ya Mitaji na Hisa hapa nchini ni haya yafuatayo:-

- Kampuni nyingi za Tanzania ni ndogo ndogo za kifamilia na zinashindwa kukidhi masharti ya kujiorodhesha katika Masoko. Masharti hayo ni pamoja na kuwa na *track record* nzuri ya faida isiyopungua kwa miaka mitatu mfululizo, uwazi wa kutunza hesabu *(disclosure*) na kadhalika. Serikali kwa kushirikiana na *CMSA* ziko kwenye harakati ya kuelimisha Makampuni ya Umma na ya watu binafsi namna ya kukidhi masharti ya soko la hisa na unafuu wa kupata mitaji ikilinganishwa na vyombo vingine vya fedha. Aidha, matokeo ya uuzaji wa hisa za *DAHACO, TPCC* na *Tanga Cement Company Ltd.,* umedhihirisha kuwepo kwa fedha nyingi katika mzunguko ambazo ziko tayari kwa wawekezaji kwa njia hii. Ukiwaelimisha tuna hakika wanaweza kuingia kwenye soko.

- Watanzania wengi bado wanahitaji elimu kuhusu Masoko ya Mitaji ili kuwawezesha kushiriki. Wizara ya Fedha ikishirikiana na Mamlaka ya Dhamana na Masoko ya Mitaji, tunazo programu mbalimbali za kuwaelimisha na kuwahamasisha Watanzania kushiriki katika Masoko ya Mitaji. Juhudi hizi bado zinaendelea.

- Kwa kuwa *DSE* iko Dar es Salaam, huduma za masoko ya mitaji zimekuwa mbali na washiriki wengi. Mamlaka inawahimiza madalali kuwa na wakala sehemu mbalimbali za nchi yetu ili kusambaza huduma hii. Kwa kukamilika kwa mfumo wa teknolojia ya habari *"Automated Trading System (ATS),* itawezesha kusogeza huduma hizi karibu na wananchi mikoani.

- Makampuni mengi na hasa binafsi yanaogopa kuweka taarifa zao hadharani kwa kudhani kuwa kutumia masoko ya mitaji kutaifanya Serikali ijue wanachokifanya na hivyo kuwatoza kodi kubwa.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Naibu Waziri wa Fedha kwa majibu mazuri nina maswali mawili ya nyongeza.

Katika majibu yake ilijitokeza wazi kwamba tatizo la hapa nchini si uwezo wa wananchi kuwekeza katika hisa isipokuwa ni upungufu wa hisa za Makampuni yaliyopo sokoni kwa maana ya *Stock Exchange.*

Swali, kuna baadhi ya Makampuni mazuri ambayo yana *track record* nzuri yanatunza vitabu vizuri na ni *Public Company* tayari sio *Private* nayo ni pamoja na Mabenki mathalani *Barclays Bank. Barclays Bank* ipo Kenya na ipo sokoni kwa nini sio

Tanzania? *CRDB* ni Benki inayofanya vizuri na ina wana hisa tayari lakini haiko sokoni kwa nini?

La pili, Mwenyekiti ni kuhusiana na Makampuni ya Madini. Tuna matatizo na Makampuni ya Madini kwa sababu hatujui utaratibu wao wa kutunza vitabu vyao vya fedha na kadhalika. Sasa hivi Makampuni hayo yameorodheshwa kwenye *Stock Exchange* ya nje ya Tanzania yako Johannesburg, London na Canada kwa nini sio Dar es Salaam mahali ambapo ndipo wanapochimba mali yetu kutoka chini. Sisi wananchi tunataka tuwe na hisa kutoka kwenye Makampuni hayo? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Makampuni mengi makubwa nayo yangeweza kujiorodhesha kwenye Soko la Mitaji hapa Tanzania hususan Mabenki. *Barclays Bank* kwa mfano inashiriki kwenye soko la hisa imewekeza hatifungani ya shilingi bilioni 30. Kwa sasa hivi wangekuwa wamewekeza hata kwenye hisa lakini kumetokea mabadiliko kidogo kwenye Benki ya *NBC.* Kama mnafahamu *NBC, ABSA* wana asilimia 70 ya hisa. Asilimia 70 hizo *ABSA* yenyewe Afrika ya Kusini imenunuliwa na *Barclays Bank.*

Kwa hivyo *NBC* na *Barclays Bank* sasa hivi wako katika majadiliano ya kuona jinsi gani wanaweza wakashirikiana katika shughuli zao kabla *Barclays Bank* haijawekeza katika hisa. Lakini sasa hivi wanazo hatifungani. *NBC* yenyewe ilikuwa na nia ya kutaka kuwekeza kwenye mtaji lakini *NBC* kwa sasa hivi sio *Public Company* kwa maana ya *definition* ya kisheria *Public Company*. Halafu Serikali bado tuna hisa asilimia 30.

*CRDB* wana nia sana kutaka kuwekeza kwenye soko la hisa. Lakini *CRDB* kwa sasa hivi tuna mkataba na Serikali inaendeshwa kwa ubia na Denmark. Kwa hiyo, mpaka wabia hawa watakapouza *share* zao ndiyo *CRDB* inaweza kuwa na mikono huru ya kuweza kujiunga katika soko.

Makampuni ya Madini nadhani ni suala ambalo hata Waziri Mkuu analifahamu. Serikali inalishughulikia suala hili kwa aina ya pekee. Kwa hivyo kwa kweli nisingetaka nijibu suala dogo kwa kuwekeza hisa wakati Serikali inashughulikia suala zima kubwa la Makampuni haya yashiriki vipi katika uchumi wa nchi yetu. Nadhani nimetosheleza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nitaruhusu swali moja la nyongeza. Majibu yamekuwa marefu sana kwa hiyo labda nimpe nafasi Mheshimiwa Hamad Rashid aulize swali moja la nyongeza halafu tuendelee na maswali mengine.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali moja la nyongeza. Kwa kuwa rasilimali za Tanzania Watanzania wengi wangetegemea kuzipata kupitia soko hili la mtaji. Na kwa kuwa rasilimali kubwa za madini haiwafaidii Watanzania. Je, Waziri atakubaliana nami kwamba wakati umefika kuleta sheria tuiangalie kama ina kasoro ili tuwabane hao wanaowekeza Tanzania wasiweze kuchukua rasilimali zetu bila ya kuwaridhisha Watanzania?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme kwamba suala la Makampuni ya Madini Serikali ilishaelekeza kwamba linaangaliwa katika suala zima uwekezaji na suala zima la sheria. Vikao vimefanyika kupitia Kamati ambayo iliyoteuliwa pamoja na kuwashirikisha wenye Makampuni. Lakini kama alivyoeleza vizuri Naibu Waziri ni kwamba kuingia katika soko la hisa ama katika hatifungani kunategemea faida ambayo yule mwekezaji anaona kwamba anapata.

Kwa upande wa Makampuni ya Madini kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Makampuni ya Madini mtaji wao mkubwa unatoka kwenye nchi zao. Kwa upande wa Tanzania itabidi kwa kweli tuendeleza kukuza uchumi wetu. Kwa sababu fedha ambazo zilizokuwepo katika hisa ni kama milioni 200 na kitu. Na fedha ambazo Makampuni mengi ya Madini ambayo nahitaji katika kuwekeza ni fedha nyingi sana.

Kwa hivyo kitu ambacho tunachoweza kufanya ni kuwashawishi kama tulivyosema suala zima la kuleta sheria hapa tutalitafakari kwa sababu katika nchi mbalimbali sheria kama hizi kwa kweli hazipo. Tumeangalia katika nchi mbalimbali ambazo zinawekeza lakini hakuna sheria kama hii ya kulazimisha watu waweze kujiunga katika soko la hisa. Suala kubwa nafikiri ni kukuza uchumi wetu ili ionekane kwamba wale ambao wanawekeza wanaweza kupata mitaji kutoka hapa hapa nchini.

Na. 70

**Utekelezaji wa Ahadi ya Kutoa Dawa Katika Zahanati - Kondoa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Bajeti ya Mwaka 2006/2007 Waziri wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii aliahidi kuwa, Serikali itatoa dawa kwa ajili ya Zahanati mpya za Jogolo, Mwailisabe pamoja na Kituo cha Afya Makorongo Wilayani Kondoa:-

Je, ahadi hiyo ya Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zahanati mpya za Jogolo na Mwailisabe pamoja na Kituo cha Afya Makorongo vimo katika orodha ya vituo ambavyo vinastahili kupatiwa dawa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Hata hivyo taarifa tulizo nazo mpaka sasa ni kwamba Zahanati za Jogolo na Mwailisabe bado hazijaanza kutoa huduma kwa sababu ya ukosefu wa watumishi na vitendea kazi. Aidha, kituo cha Afya cha Makorongo bado hakijakamilika. Kutokana na sababu hizo Wizara yangu imeshindwa kupeleka dawa katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu itakuwa tayari kupeleka dawa katika Zahanati za Jogolo na Mwailisabe

iwapo zitakuwa na watumishi na vitendea kazi. Kadhalika, Kituo cha Afya cha Makorongo kitakapokamilika kwa majengo, watumishi na vitendea kazi nacho kitapatiwa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya Mheshimiwa Mbunge napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imewapangia kazi Maafisa Tabibu saba (7) na Wauguzi 14 kwenda kufanya kazi katika Wilaya ya Kondoa. Napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuwasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ili kuona uwezekano wa kuwapanga watumishi hao katika zahanati za Jogolo na Mwailisabe ili kuanza kutoa huduma badala ya kuwaweka tu wale watumishi na kuwarundika katika sehemu moja.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Aidha, napenda nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na tunashukuru Wizara kwa kutuongezea watumishi. Hata hivyo naomba niulize masuala mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la ufunguzi wa zahanati mpya linakwaza na upungufu wa watumishi. Je, Serikali ama Wizara ina mpango gani wa kutatua tatizo la upungufu wa watumishi wa afya nchini?

Swali la pili, kwa kuwa katika majibu yake alisema kwamba Kituo cha Afya Makorongo bado majengo yake hayajakamilika. Na kwa kuwa mimi mwenyewe nilikagua majengo hayo wiki iliyopita na hivi sasa jengo la mwisho la wodi ya wanaume ndiyo linakamilishwa. Je, Naibu Waziri atakuwa tayari kwa sababu Makorongo sio mbali sana aende akakague na kujihakikishia mwenyewe kuwa majengo yamekamilika ili aweze kutoa dawa kwa ajili ya kufungua kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna upungufu wa wafanyakazi. Kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba wafanyakazi huwa wanapelekwa katika Halmashauri halafu wenyewe Halmashauri zile Kurugenzi ndizo ambazo zinaamua kupeleka wafanyakazi kule.

Lakini si hivyo tu ni kwamba sasa hivi Wizara ya Afya, Halmashauri ya Kondoa imepangiwa nafasi 31 za watumishi wa kada mbalimbali ambao wanatakiwa tuwapeleke kule Kondoa. Sasa hivi Wizara yangu inaanza kuchambua kuona ni wataalamu kiasi gani ambao tunaweza kuwapeleka katika Halmashauri ya Kondoa. Naendelea kusisitiza kwamba watakapokuwa tumewatumia hao wafanyakazi basi ni vizuri Halmashauri ziangalie na ziipe kipaumbele zile sehemu ambazo zina upungufu mkubwa wa wafanyakazi badala ya wengi kuwakuta wamerundikwa katika Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la pili ni kwa sababu Mbunge ananiambia kwamba wiki hii tu amekwenda kukagua na kuona yanaisha na kwamba wodi itakuwa iko tayari. Mimi napenda kusema nitakwenda kuiangalia katika muda muafaka. Siahidi kwamba nikitoka hapa kwa sababu nina majukumu mengine.

Lakini nitakwenda kuiona. Vile vile ninaendelea kusisitiza kwamba sio lazima mimi nikakague, inapoonekana kwamba ipo tayari wataalamu kule Wilayani wapo,

Mganga Mkuu yuko pale, Mganga wa Mkoa wa hapa Dodoma anaweza akaenda akakagua kwa niaba yetu na kama iko tayari hakuna sababu ya kuizuia isianze kazi.

**WAZIRI WA WAFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Naibu Waziri wangu kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Mheshimiwa Degera amezungumzia kuhusu uhaba wa Wafanyakazi katika vituo vyetu kwa nchi nzima na nakubaliana naye idadi ya wafanyakazi tulionao wataalam ni asilimia 40 tu, ya wale tunaowahitaji. Kwa hiyo, tuna upungufu mkubwa kila mahali na mipango tunayoifanya ni kwamba sasa hivi tumeshapitia vituo vyetu vya kufundishia hawa wataalam kwa nia ya kuboresha vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuongeza idadi na huu utakuwa ni mradi ambao tunautizama katika miaka miwili mitatu ijayo.

Lakini vilevile utaratibu huu wa kuwatuma wafanyakazi moja kwa moja kwenye Halmashauri unasaidia kwa sababu hapo zamani ilibidi waombe kazi katika Halmashauri na vilevile kwa kushirikiana na *Global Fund* tumepewa pesa za kuajiri wafanyakazi wa dharura na hili zoezi linaendelea mategemeo yetu ni kwamba tutapata wafanyakazi wengi ambao tutaweza kuwapeleka katika Halmashauri moja kwa moja.

Na. 71

**Matibabu ya Ugonjwa wa Saratani**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ugonjwa wa saratani umekuwa tishio sana, hasa saratani ya matiti na kizazi kwa akina mama; na kwa akuwa, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* ndiyo pekee inayotoa matibabu ya ugonjwa huo Nchini; na kwa kuwa, Taasisi hiyo imeanza kuelemewa sana kutokana na wingi wa wagonjwa wa saratani:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, umefika wakati muafaka kuanzisha Kitengo cha Taba ya Saratani katika hospitali zote za rufaa nchini; na kwa kuwa, kwa kufanya hivyo kutapunguza msongamano wa wagonjwa *Ocean Road* pamoja na kupunguza gharama kubwa wanazopata wagonjwa na ndugu zao kwa usafiri na malazi wanapokwenda kutibiwa Dar es Salaam?

(b) Pamoja na kutambua juhudi kubwa zinazochukuliwa na Madaktari Wanawake Tanzania kupitia Chama chao cha *MEWATA* katika kukabiliana na saratani ya matiti kwa akina mama. Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura katika kukabiliana na ugonjwa huo kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa ugonjwa wa Saratani ni tishio kubwa kwa jamii, pia ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa pamoja Saratani ya matiti na kizazi kwa akina mama pia saratani ya nundu dume (*Prostate)* kwa wanaume imekuwa ikiongezeka kwa kasi siku hadi siku. Taasisi ya Saratani ya *Ocean*

*Road* inahudumia asilimia kumi (10%) tu ya wagonjwa wote wa saratani hapa nchini. Hivyo ni dhahiri kuwa Taasisi hiyo haitoshelezi.

Hata hivyo Serikali ina mipango ya kuanzisha huduma hii katika hospitali zote za rufaa hapa nchini. Tayari makubaliano yamekwishafanyika kati ya Serikali na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*International Atomic Energy Agency*) ili kuanzisha Kitengo cha matibabu ya magonjwa ya Saratani katika Hospitali ya Bungando mkaoni Mwanza.

(b) Serikali inatambua na kuzipongeza juhudi kubwa zinazochukuliwa na Madaktari Wanawake wa Tanzania kupitia Chama chao cha MEWATA katika kukabiliana na Saratani ya matiti kwa akina mama.

Pamoja na mchango huo wa MEWATA Serikali imeandaa mipango na hatua za kudumu za kukabiliana na ugonjwa huu. Serikali kwa kuitumia Taasisi kyake ya Saratasi ya *Ocean Road* imeweka mikakati ya kufundisha wataalam katika Wilaya zote namna ya kugundua dalili za magonjwa ya Saratani mapema na pia mambo ya kufanya baada ya ugunduzi huo. Tayari mafunzo hayo yamekwishafanyika katika Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga. Aidha, mipango inafanywa ili kwenda kuendesha mafunzo hayo katika Wilaya ya Musoma mkaoani Mara.

Ushahidi wa kitaalam unaonyesha kuwa njia bora na ya kudumu katika kukabiliana na magonjwa ni kuwapo elimu husika kwa watendaji katika sehemu zao. Ni matumaini yetu kuwa kwa kutoa mafunzo hayo katika Wilaya zote tutafanikiwa kupunguza tatizo la Saratani nchini.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kupata nafasi hii niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Aidha nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa dhati sana Wanawake Madaktari hawa wa Tanzania ambao wameguswa na uzalendo na kuamua kuchangisha pesa na kutumia muda wao mwingi kwa ajili ya kushughulika na saratani ya matiti kwa wanawake. Napenda tuwapongeze sana (*Makofi*)

Serikali inawaunga mkono namna gani MEWATA katika kuendele na jitihada za kuokoa maisha ya wanawake wa Tanzania hasa kutoka na ugonjwa huu wa saratani ya matiti pamoja na saratani za namna nyingine?

Swali la pili, kwa kuwa tunaambiwa matibabu ya saratani ni bure, lakini ukienda Muhimbili hasa kwenye vipimo gharama zake ni kubwa kiasi cha kwamba Watanzania wa kawaida hawawezi kumudu gharama za vipimo pale Muhimbili. Aidha Watanzania matibabu yenyewe pale *Ocean Road* ambapo pia tunaambiwa ni bure. Mara nyingi ukienda na kwa sababu na mimi nimeuguza wagonjwa wengi mara nyingi unambia hakuna dawa ukanunue kwenye maduka na pia ni gharama sana. Kwanini Serikali isihakikishe kwamba gahrama za vipimo zinakuwa bure lakini pia na dawa zenyewe zinakuwepo pale *Ocean Road* ili wagonjwa waweze kutibiwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali inapongeza sana juhudi za Madaktari Wanawake katika harakati za kuwasaidi akina mama wenye matatizo ya saratani za matiti. Serikali inawaunga mkono, kwa sababu kunapokuwa na fedha Serikali huwasaidia MEWATA. Lakini lazima tufahamu kwamba wakati wanapokuwa wanafanya hizi shughuli zao, majengo wanayotumia wanatumia hospitali za Serikali na vifaa wanavyotumia ni vifaa vya Serikali na watumishi wanaokwenda kule ambao ni Madaktari wale pia ni watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili tulielewe kwamba si lazima tulipeleke fedha lakini tunaweza tukawa tunasaidia kama Serikali katika njia moja au nyingine ili kuweza kufanikisha hii kazi ambao wenzetu Madaktari wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la vipimo na matibabu napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba, ugonjwa wa salatani kawaida mgonjwa anatibiwa bure anapokuwa amelazwa pale Hospitali pale *Ocean Road* akiwa tayari amegundulika kwamba yeye ana ugonjwa wa saratani. Atapewa dawa na vipimo vingine bure atakapokuwa anaendelewa kutibiwa pale ndani ya Hospitali ya *Ocean Road*. Hatuwezi tukasema tuwalipie wote ambao wanakwenda Muhimbili au *KCMC* au Bugando wakati wakiwa katika *process* ya *diagnosis*. Kwa sababu kuwalipia na kufanya bure inawezekana mtu anahisi kwamba ana-cancer lakini kipindi kile bado hayahadhirika. Sasa tutakapokuwa tunawalipia watu wote na bahati mbaya mwisho ikaonekana kwamba si cancer mimi nafikiri tutakuwa tunafanya ndivyo sivyo. Kwa hiyo naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba wagonjwa wanapokuwa tayari wameshagundulika ndiyo sisi pale tunaanza kuwatibu na tunatoa dawa bure na ninawahakikishia pale *Ocean Road* zipo nyingi na inapotokea kwamba dawa sasa inakosekana kwa bahati mbaya ndiyo hapo Wizara tunafanya utaratibu mwingine kwamba Wizara tuweze kununua.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wagonjwa wanaokwenda *Ocean Road* na hasa akina mama wenye matatizo ya saratani ya matiti wanakwenda kule na kupata dawa ya *radiation* au tiba ya mionzi na wana matumaini ya kwamba wakifanyiwa matibabu watapona. Lakini ushahidi wa mazingira ni kwamba takribani wengi kama asilimia 70 au 80 sina hakika. Lakini niseme wengi wao waliofanyiwa tiba hii wamefariki muda mfupi baada ya kufanyiwa matibabu hayo. Hivi Serikali inalijua hili na inatoa kauli gani na kuwaondoa hofu akina mama ambao wanadhani kwamba radiation ni tiba ya ugonjwa wa saratani.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** : Mheshimiwa Mwenyekiti, saratani inavyojitokeza mara nyingi ukiacha saratani ya damu ambayo inaenea kila mahali nyingi inakuwa kinundu mahali fulani sasa matibabu yake inaweza ikawa ama upasuaji ukiweza kukitoa kile unaweza ukamfanya mtu apone au ukampa dawa au ukampa hiyo mionzi. Sasa hawa wanaopewa mionzi kwa kawaida wako katika hatua ya mbali kabisa, ni watu ambao wamekuwa na ugonjwa kwa muda mrefu na hatuna njia ya kumfanyia upasuaji na hiyo ndiyo njia peke yake iliyopo. Sasa Mheshimiwa Mbunge amesema anaushahidi wa kimazingira lakini nadhani ushahidi wa kisayansi ingekuwa utafute watu wenye ugonywa ambao umeenea kiasi hicho hicho mmoja umpe mionzi,

mmoja usimpe mionzi halafu ndiyo unaweza ukasema hawa nimewapa mionzi ndiyo huwa wanakufa.

Lakini huwa tunatoa kwa sababu hatuna njia nyingine na inapotokea kwamba wanafariki basi inakuwa ni bahati mbaya na hatudhamirii kufanya hivyo.

Na. 72

**Miswada Kuandikwa Kwa Lugha ya Kiswahili**

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, tangu Hayati Mwalimu J. K. Nyerere atangaze kuwa, Kiswahili ni lugha rasmi ya Taifa na pia lugha rasmi ya kuendesha mijadala yote Bungeni; na kwa kuwa, Miswada huletwa kwa lugha ya Kiingereza:-

(a) Je, kwa nini hadi leo Miswada huandikwa kwa lugha ya Kiingereza na kufanyiwa majumuisho kwa lugha ya Kiswahili, Serikali haioni kuwa, haiwatendei haki wananchi ambao wengi wao hawaelewi Kiingereza?

(b) Je, kwa kipindi chote hicho cha amiaka 43 (1963 – 2006) Serikali imeshindwa kupata wataalam wa kutafsiri Miswada hiyo ili kuondoa utata unaotokana na matumizi ya lugha ya Kiingereza?

(c) Je, Serikali haioni kuwa, huu ni muda muafaka kwa Miswada yote inayoletwa Bungeni iwe inaandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa manufaa na ufahamu wa wananchi wote?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kanal Farah Mbunge wa Rahaleo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Miswada yote inayoletwa mbele ya Bunge hili kwa madhumuni ya kujadiliwa na kupitishwa huandikwa kwa lugha ya Kiingereza kwa sababu ya Mfumo wa Sheria ambao nchi yetu umeurithi kutoka Mfumo wa Kiingereza. Mfumo huo wa Sheria na utaratibu wa kurithi Sheria kama ilivyofanya Tanzania pia unafuatwa na nchi nyingi ambazo zamani zilikuwa chini ya utawala wa kikoloni wa Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti mijadala yote kuhusu miswada inayoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu huendeshwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo inaeleweka kwa Watanzania walio wengi sanjari na hilo miswada hiyo huambatana na tafsiri ya lugha ya Kiswahili kuhusu madhumuni na sababu ya miswada yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu wa Bunge kujadili miswada ya sheria kwa lugha ya Kiswahili na kuwepo kwa tafsiri ya Kiswahili ya madhumuni na sababu za miswada yenyewe wananchi wanapata fursa kubwa kupitia kwa wawakilishi wao na vyombo vya habari Bungeni kuelewa kile kilichomo katika Muswada.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao wataalam wa kutafsiri miswaada ya Sheria kutoka katika Lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili ingawa wataalam hawa ni wachache na hawakidhi mahitaji yaliyopo. Hata hivyo Wizara yangu inaendelea na mikakati ya kuimarisha kitengo cha tafsiri kilichopo kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inaona upo umuhimu mkubwa wa kutafsiri na kuchapisha Sheria zote kwenye lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya wananchi wote na kukipa Kiswahili hadhi yake. Hadi sasa sheria kadhaa zimeshatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ikiwemo Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura ya 144, Sheria ya Ndoa Sura ya 29, Sheria ya Mabaraza ya Kata Sura ya 206, Sheria ya Filamu na Michezo ya Jukwaani Sura ya 230. Sheria kadhaa zipo katika hatua za mwisho za kutafsiriwa ikiwemo Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mnweyekiti, mojawapo ya mipango ya muda mrefu ya Wizara yangu ni kuhakikisha kuwa Sheria zinazotungwa na Bunge zinakuwa katika lugha zote mbili kwa wakati mmoja yaani zitungwe kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo kumekuwa na vikwazo mbalimbali katika kufikia malengo haya kwa mfano. Bado maelekezo yanayoletwa kwa ajili ya kutunga Sheria hizo yanakuwa ni ya Kiingereza na yanaletwa katika kipindi kifupi tu kabla ya Mkutano wa Bunge kujadili muswada unaohusika.

Hivyo azma ya kuwa na muswada ambao unakuwa uko katika lugha zote mbili inashingwa kufikiwa. Sababu nyingine inayosababisha miswada mingi kuendelea kuandikwa kwa Kiingereza ni asili ya muswada wenyewe. Matharani iwapo muswada unaandikwa kwa ajili ya kutekeleza maagizo yanayotokana na Maazimio ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Africa au Jumuiya nyingine za Kimataifa kama *SADC*, *EAC* nakadhalika mara nyingi miswada hiyo inakuwa imeandaliwa kwa kiingereza na hivyo huchukuliwa na nchi Tanzania ikiwa mojawapo kwa lugha iliyokuwa imeandaliwa kwanza na kisha baadaye kutafsiriwa Kiswahili. Hivyo mara baada ya Kitengo cha kutafsiri Sheria kitakapokuwa kimeimarishwa na *Legislative Programme* kutolewa mapema na Serikali uwezekano wa kuwa na Miswada katika lugha zote mbili upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo lugha inayotumika kuandika Sheria huwa sio lugha nyepesi ni lugha ya kitaalam hivyo hata Sheria zikiandikwa kwa Kiswahili bado maudhui yake yanaweza kutoeleweka kwa wananchi iwapo hakutakuwa na juhudi za ziada za kutengeneza vijarida ay vipeperushi kufafanua maudhui ya Sheria iliyotungwa kwa lugha nyepesi.

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH**: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina swali moja dogo la nyongeza. Kama majibu ya Mheshimiwa yalikuwa marefu kiasi hicho kufahamisha uzito na heshima ya Kiswahili inavyotakiwa kuwa kwanini hakufanyiki juhudi za makusudi kuzikutanisha taasisi na mamlaka ili tuweze kumaliza kazi hii kwa haraka na Bunge kupata heshima yake ya kuzungumza Kiswahili moja kwa moja yaani *total hundred percent.* Haionekani ya kwamba tatizo hili pia lina viza mashule yetu kuingia katika kufundisha Kiswahili?

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Saleh Ali Farrah, Mbunge wa Rahaleo kwa kuongeza na kuonyesha kama

Serikali inavyoamini kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha yetu na ndiyo lugha inayoeleweka na Watanzania walio wengi au wote.

Kwa hivyo ni makusudi mazima ya Serikali kwamba itajitahidi kuona kwamba kila linalowezekana linafanyika kusudi miswada iwe kwenye Serikali. Lakini lazima tukubali kwamba itategemea uwezo wetu. Lakini naahidi Bunge lako Tukufu kwamba Wizara ya Sheria na Katiba na Serikali kwa ujumla itajitahidi kukuza Kiswahili ikiwa ni pamoja na kuandika Sheria zetu kwa Kiswahili.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watanzania wengi wanazungumza Kiswahili; na kwa kuwa tunao vijana wengi waliomaliza masomo yao hawana kazi ambao wangeweza kufundisha Kiswahili; na kwa kuwa sasa kuna kasi kubwa na msukumo wa nchi za Afrika kukifanya Kiswahili kiwe ni lugha ya Afrika; na kwa kuwa lugha hii imeanza kutumika katika Vikao vya Wakuu wa Nchi za Afrika; na kwa kuwa Bunge la Afrika linatumia lugha hii.

Je, haitakuwa jambo la kushangaza Tanzania ambayo ndiyo kitovu cha lugha hii tutoe visingizio vya kutokuwa na watu wenye kuweza kumudu kutafsiri lugha hii na kuitumia lugha hii kwa ufasaha na kwa hiyo kuwakatisha tamaa nchi nyingine za Afrika? (*Makofi*)

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongela, Mbunge wa Ukerewe na Rais wa Bunge la Afrika; na vilevile nampongeza sana kwa jitihada zake kama Rais wa Bunge la Afrika kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya Afrika na sisi tunalingojea hilo kwa hamu na Bunge la Afrika lenyewe kutumia Kiswahili kama lugha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu langu la msingi lilionyesha kwamba Serikali ina azma ya kukikuza Kiswahili na kwa hivyo mojawapo ya kufanya hivyo ni kujaribu kutunga Sheria zetu kwa lugha za Kiswahili na nikatoa mifano ya Sheria ambazo tayari zimeshaandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Na ninatambua kwamba kuna vijana wetu walio wengi ambao wako tayari kuweza kufundisha Kiswahili na kutafsiri Sheria hizi katika lugha ya Kiswahili, lakini tatizo ni uwezo wa Bajeti ya Serikali kwa sababu hao vijana watakapokuwa wanafanya hiyo kazi inabidi tuwape hata fedha za kujikimu.

Napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kama ilivyo azma ya Bunge la Afrika ni vilevile azma ya Bunge la Tanzania kama linavyofanya sasa hivi kutumia Kiswahili kama lugha yake ya mawasiliano. Ni azma ya Serikali vile vile kukuza na kukipa hadhi Kiswahili kama lugha yetu ya taifa. Na mimi naahidi kwamba Wizara ya Sheria na Katiba nayo itaimarisha kitengo chake kutafsiri Sheria zetu ili basi azma ya Wabunge na Watanzania ifikiwe.

Na. 73

**Fidia kwa Wananchi Wanaoshambuliwa na Wanyama Katika Maeneo Karibu na Hifadhi.**

**MHE. MARIAM KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya wananchi katika Wilaya ya Nanyumbu na Masasi wanaoishi mpakani mwa hifadhi ya Msanjesi hupata tatizo la kushambuliwa kwa mazao yao na wengine kuuawa na wanyama wakali kama simba.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kiwango cha fidia ya shilingi 50,000/- kwa Ndugu waliofiwa ni kidogo na kimepitwa na wakati hivyo kiangaliwe upya na kuongezwa?

(b) Kwa kuwa wananchi wanapowaua wanyama huchukuliwa hatua. Je, ni fidia gani inayotolewa kwa wananchi mashamba yao yanaposhambuliwa na wanyama?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haina utaratibu wa kutoa fidia kwa wananchi wanaoathirika kutokana na wanyamapori waharibifu. Matukio mengi ya uharibifu wa mali na maisha ya wananchi, yanatokana na wananchi kuvamia maeneo ya wanyamapori kwa ajili ya kilimo, ufugaji na kuweka makazi hali inayosababisha na kuzidisha migongano kati ya wanyamapori na binadamu. Maisha ya mtu aliyeuawa na wanyamapori hayawezi kulinganishwa na thamani ya fedha au vitu.

Hata hivyo, kutokana na majonzi ya wananchi kufiwa na ndugu zao Serikali inatoa kifuta machozi cha shilingi 50,000 kwa kila familia ya marehemu iliyoathirika baada ya kupata taarifa sahihi kutoka kwenye Wilaya husika. Suala la kuangalia upya kiwango cha kifuta machozi ni la msingi ambalo litashughulikiwa kiutawala kutegemea uwezo wa Serikali kifedha. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kutumia askari wanyamapori huua mnyama mkali au mharibifu pale inapobidi kufanya hivyo. Hii hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori (Sura 283 iliyorekebishwa mwaka 2002 Kifungu cha 53). Kifungu hicho pia kinaruhusu mtu kuua mnyama mkali au mharibifu pindi anapotishia au kusababisha uharibifu wa maisha au mali ya mtu.

Aidha, Wizara yangu itaendelea kuwalinda wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuendesha doria za msako wa wanyamapori wakali na waharibifu, kununua risasi za kutosha na kutoa mafunzo kwa askari wa vijiji, viongozi na wananchi kwa ujumla. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu itaendelea kushirikiana na wadau pamoja na vyombo vingine vya dola katika kutekeleza jukumu hili.

**MHE. MARIAM KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kurekebisha mipaka iliyopo katika eneo la Hifadhi ya Msenjesi na Mpombe ambayo ipo karibu kabisa na makazi ya wananchi ili kuweza kuwapa uhamisho wanyama hawa wanaowazuru wananchi kusogea mbele na kuwaachia nafasi wananchi hawa?

La pili je, kiwango hiki cha kifuta machozi cha shilingi 50,000 mpaka hivi sasa kwa kweli haoni kwamba hatutendi haki na upo uwezekano kabisa wa Serikali angalau kuongeza na ikiwezekana pesa kupelekwa katika Halmashauri zetu za Wilaya ili linapotokea tatizo familia ziweze kupewa mara moja na kusadia angalau hata katika shughuli za mazishi kwa wanaopata tatizo hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusogeza mipaka ya hifadhi. Ameomba tusogeze ili wananchi waweze kupata nafasi ya kuishi. Mipaka hii imewekwa kwa utaratibu maalum kisheria, kwa hivyo kusema kusogezwa kwa mipaka ya Hifadhi kwa kweli itakuwa ni ngumu.

Na kuhusu kuongeza kiasi cha kifuta machozi, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi nimesema, Serikali imeona kwamba kiwango cha shilingi 50,000 kutoa kwa mtu aliyeuawa na mnyamapori tunakubali ni kidogo na tutakiangalia kutegema uwezo wa kifedha wa Serikali.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa naibu Waziri amesema tatizo la msingi ni wananchi kuvamia maeneo ya wanyama na kwa kuwa tatizo liliko Masasi liko pia Wilaya ya Karatu hususan vijiji vya Shaham, Apakitete na Chemchem ambapo wananchi huvamiwa katika maeneo yao na wanyama bila wao kuingia katika maeneo ya wanyama.

Je, Serikali iko tayari sasa kutenga fedha maalum kutoka kwenye fedha zanazopatikana kutokana na rasilimali ya maliasili ili ziweze kutumika kwa ajili ya fidia kwa watu wanaovamiwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika jibu langu la msingi nimesema kwamba mara nyingi utakuta wananchi wanavamiwa na wanyamapori kwa kuwa wanaingi katika maeneo ya wanyamapori.

Lakini pia inawezekana kabisa wanyamapori kuingia katika eneo la wananchi na kufanya uharibifu. Hivyo basi nimejibu kwamba wananchi ambao wanapata madhara kutoka kwa wanyamapori wanalipwa fidia. Fedha imetengwa na tutawalipa wote ambao wamepata madhara na kuuawa na wanyamapori. Vilevile nimesema kwamba kile kiwango cha shilingi 50,000 cha kifuta machozi kinaangaliwa upya. Tunaangalia uwezekano wa kukiongeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza niendelee na hatua moja kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, kuendelea na swali linalofuata. Kanuni Namba 54, kipengele cha kwanza, kinampa mamlaka Spika kulihutubia Bunge wakati wowote na anaweza kumkatisha Mbunge yeyote kuzungumza akitaka kufanya hivyo. Lakini, mnaweza kusema wewe siyo Spika, Mheshimiwa Mhagama ni Mwenyekiti. Lakini, naomba niwasomee Kanuni hiyo ikiambatana na Tafsiri ya Maana ya Spika. Maana ya Spika ni kwamba ni Spika wa Bunge, ama Naibu Spika, au Mwenyekiti wa Bunge ama Mbunge yeyote aliyekalia Kiti cha Spika wakati shughuli za Bunge zinaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa, nimeletewa matangazo mawili ya dharura. La kwanza, linatuomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa kadri tunavyojua taratibu zetu, *Pigeon Holes* zetu ndiyo huwa zinatumika kutupa taarifa mbali mbali, kwa hiyo zimejaa kutokana na shughuli nyingi za Bunge. Kwa hiyo, tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuondoe zile taarifa tulizowekewa mle kusudi tuwekewa taarifa nyingine muhimu ambayzo zinatakiwa zitufikie leo hii. Na kwa wale ambao wamepoteza funguo zao, tunawaomba sana wawasiliane na Utawala ili utaratibu wa kuwapa funguo zingine ufanyike na shughuli za kutuhudumia ziendelee.

Taarifa ya pili, ni kwamba iko Miswada miwili itaanza kugawiwa hapa ndani. Lakini Ofisi ya Katibu wa Bunge imenipa taarifa isemayo kwamba Muswada wa *The Supplementary Appropriate for Financial Year 2003/20004* na *Optometry Bill* ya Mwaka 2007: Miswada hii bado haijaweza kukidhi matakwa ya Kikanuni. Lakini Waheshimiwa Wabunge watagawiwa hivi punde, ili mpate nafasi ya kuisoma tayari kwa kuichangia katika Mkutano wa Bunge ujao. Aidha, Vikao vya Kamati vinavyohusiana na Miswada hiyo navyo vijiandae kwa ajili ya kuipitia. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea baada ya kufuata utaratibu wa Kanuni hiyo Na. 4(i).

Mheshimiwa Mariam Mfaki, swali linaloelekezwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nikukumbushe kwamba kuna swali linalotangulia la kwangu, halijaulizwa.

**MWENYEKITI:** Oh! Samahani! Tunaanza na Balozi Abdi H. Mshangama.

Na. 74

**Kuanzishwa Mradi Maalum wa Hifadhi ya Misitu – Lushoto**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:- Kwa kuwa vyanzo vingi vya maji na mito Wilayani Lushoto vinakauka na vilele vya milima vinageuka kuwa jangwa kutokana na kilimo kisichozingatia hifadhi ya mazingira.

Je, Serikali itakuwa tayari kuendeleza au kuanzisha mradi maalum wa Hifadhi ya Misitu na vilele vya vilima Wilayani Lushoto, ambao utajumuisha kuwapatia wananchi miche ya mbegu za miti bila malipo ili kuhamasisha upandaji wa miti kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:- Mheshimiwa Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Mshangama, naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Wizara ya Maliasili na Utalii inalo jukumu la kusimamia maendeleo ya misitu nchini, ikiwa ni pamoja na kuhifadhi misitu na upandaji wa miti. Kwa sasa Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 inahimiza Usimamizi Shirikishi wa Misitu ambapo inawataka wananchi wahamasike kupanda miti na kuhifadhi misitu wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Lushoto. Lushoto ni Wilaya mojawapo kati ya Wilaya ambazo zimepewa kipaumbele kuendelezwa katika masuala ya kuhifadhi mazingira na kupanda miti ambapo pia misitu ya hifadhi na mashamba ya Taifa ya Shume na Maghamba yapo katika Wilayani hiyo.

Wilaya hiyo ilifanikiwa kupatiwa mradi wa kupanda miti wa *Soil Erosion Control and Agro-forestry Project* ambao ulitekelezwa kwa takriban miaka 20 kuanzia mwaka 1981 hadi mwaka 2000 ulipomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza malengo ya mradi huo, wananchi walipata mafunzo yanayohusiana na masuala ya kuhifadhi mazingira kwa nia ya kupunguza umaskini hususan katika vijiji vya Longoi, Shume na Gogolo katika kuhifadhi ardhi kwa kutumia matuta (makingamaji), kupanda miti inayokua haraka, kurutubisha ardhi na ya malisho ambapo pia wananchi walifanikiwa kuhifadhi na kuendeleza Misitu ya Asili katika maeneo yao pamoja na kufuga ng'ombe wa kisasa, hasa wale wa maziwa. Pia wananchi walijifunza kuhusu kilimo cha kuchanganya miti na mazao yaani kilimo mseto. Baada ya mradi huo kumalizika shughuli zake zilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Kwa sasa Serikali haina mpango wa kuanzisha mradi mpya wa kufadhili upandaji miti Wilayani Lushoto. Mpango uliopo ni kusimamia na kuendeleza mikakati iliyopo ya kuhifadhi na kupanda miti kwa kuwahimiza wananchi kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto katika jitihada za kuendelea kukuza miche katika bustani zao ndogo katika ngazi ya familia na vijiji, hatimaye waipande kwa manufaa yao.

Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu inaendelea kutoa elimu kuhusu uhifadhi wa Misitu na upandaji miti kwa kuwatumia wataalam wa masuala ya misitu wa kituo cha Misitu Uenezi Kanda ya Kaskazini kwa njia ya ugani, kuonyesha video za mafunzo pamoja na kipindi cha *Radio* cha Misitu ni Uhai kinachorushwa na *Radio Tanzania Dar es Salaam* kila siku ya Jumatatu saa 11.30 jioni. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Sera ya Misitu ya mwaka 1998, Wizara itashirikiana na Mhesihmiwa Mbunge kuwahamasisha wananchi wa Lushoto kuendeleza juhudi katika kuhifadhi misitu na kupanda miti.

Na. 75

**Mikopo Iliyotolewa na Serikali kwa Wananchi**

**MHE. MARIAM S. MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitoa shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa kwa ajili ya kuwakopesha wananchi wakiwemo akina mama na vijana kwa lengo la kuanzisha, kuendeleza na kuongeza mitaji katika miradi yao ili kuondokana na umaskini; na kwa kuwa kutokana na Serikali kupunguza riba ya mikopo hiyo walipaji watakuwa wengi.

(a) Je, fedha hizo zimepelekwa katika Benki zipi na kuna nakala zozote za mgao huo wa fedha zilizotolewa kwa Wabunge ili wawahamasishe wananchi kuhusu kukopa?

(b) Je, Serikali iko tayari kuyahimiza mabenki kutoa masharti ya mikopo hiyo hadi vijijini ili wananchi wayasome, kuelewa na hatimaye wakope?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imekwishatoa jumla ya shilingi bilioni 10.5 katika Benki za *CRDB* na *NMB* kwenye Mikoa yote ya Tanzania Bara. Fedha hizo zinakopeshwa katika Mfumo wa Dhamana ya Mikopo na wananchi wanaombwa waendelee kujitokeza katika maeneo yao ili waweze kuzikopa fedha hizo.

Mwongozo wa taratibu za kukopa umeishatolewa na Serikali na kusambazwa katika Mikoa yote nchini. Aidha kwa kutambua mchango wa Waheshimiwa Wabunge katika kuwaelimisha wananchi na kuwa hamasisha wananchi kukopa chini ya mfumo huu, nao pia wamekwishagawiwa mwongozo huu.

(b) Serikali iko tayari kuyahizimi mabenki kuandaa na kutoa mashari ya benki hizo mpaka vijijini ili wananchi waweze kusoma na kuyaelewa. Aidha Serikali imeandaa na itasambaza nchini kote vipeperushi ambavyo vinaelezea taratibu zote zinazotakiwa kuwawezesha wananchi kupata mikopo hiyo. Hata hivyo jambo la msingi, ni kuhakikisha wananchi wengi ambao wapo vijiji wanaelimishwa juu ya utaratibu mzima wa kupata mikopo kutoka mfuko huu. Watendaji katika Halmashauri zetu, madiwani na Waheshimiwa Wabunge wana nafasi kubwa ya kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi juu ya masharti na taratibu za kuwawezesha kupata mikopo hii.

Serikali imekwishatoa mafunzo kwa Maafisa watatu ambao ni Afisa Ushirika, Afisa Maendeleo ya Jamii ya Afisa Mipango kutoka kila Halmashauri ya Wilaya au Manispaa ya Jiji, juu ya mpango huu lengo likiwa nao waupeleke kwa wananchi. Hivi sasa wataalam wa sekretarieti ya mipango huu wamepita mikoa yote kutathimini zoezi hili na kutoa mafunzo kwa viongozi wengine wa ngazi za Mkoa, Wilaya na Halmashauri. Natoa wito katika Bunge lako Tukufu kuwa Maafisa na Viongozi waliopata mafunzo hata waendelee kuyatoa kwa wengine ili dhana nzima ieleweke. Pia Halmashauri ziwezeshe Maafisa waliopatiwa mafunzo kufika vijijini kutoa elimu ya mikopo hii.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina swali dogo la nyongeza:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeisha kiri kwamba inaendelea kutoa mafunzo kwa viongozi ambao wataendelea na wenyewe kutoa mafunzo mpaka huko vijijini kwa wananchi ambao ndio walengwa; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Halmashauri zitaendelea kutoa mafunzo. Sasa kutokana na Halmashauri kutokuwa na fedha za kutosha. Je, Serikali kuu iko tayari kuziwezesha Halmashauri ili ziweze kuendelea kutoa mafunzo kwa wananchi wote na hatimaye wananchi wote kuelewa na kuweza kukopa kama nilivyouliza katika swali langu la mwanzo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba mpango huu unafanikiwa. Mpaka sasa hakuna Halmashauri yoyote

ambayo imetoa taarifa Serikalini kwamba inashindwa kuratibu na kusimamia na kuwezesha Mfuko huu. Hivyo, Serikali ikipokea malalamiko kutoka Halmashauri yoyote, itachukua hatua haraka inavyowezekana. *(Makofi)*

Na. 76

**Elimu Kuhusu *SACCOS* na Ujasiriamali**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi hawajaelimishwa kuhusu umuhimu wa kujiunga na Vyama vya Akiba na Mikopo *SACCOS* pia wengi wao hawana elimu ya ujasiriamali na kwa kuwa zoezi la uelimishaji linakwenda sambamba na kuwatumia watalaam wa Ushirika, ujasiriamali na maafisa wa Maendeleo ya Jamii:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa bila bila kuwaelimisha wananchi kuhusu *SACCOS* na ujasiriamali zoezi zima la kuondoa umaskini halitafikia malengo yanayotarajiwa na Serikali ya Awamu ya Nne?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuelimisha jamii kwa njia ya kampeni kuhusu suala hilo kama ilivyo kwa kampeni nyingine kama Nyota ya Kijani kwa kutumia vyombo vya habari na vijarida mpaka vijijini?

(c) Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kuwapatia watalaam hao magari angalau gari moja kila jimbo ili iwe rahisi kuwafikia walengwa kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ili kufikia malengo yanayotarajiwa katika zoezi zima la kuondoa umaskini, upo umuhimu wa kutoa elimu juu ya umuhimu wa wananchi kujiunga katika vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)* kwa njia mbalimbali. Kwa kutambua umuhimu wa elimu ya ushirika na ujasiriamali Serikali kwa kupitia programu mbalimbali za *PADEP, TASAF, DADPS, ASDP, AMSDP* imehakikisha kuwa suala la kujengea uwezo taasisi za wananchi ikiwemo *SACCOS* linazingatiwa.

Aidha, kwa kupitia mpango kabambe wa Modenaizesheni ya Ushirika nchini, unaosimamiwa na Wizara yangu wadau mbalimbali wameshirikishwa katika utoaji wa elimu ya Ushirika na ujasiriamali kwa wananchi wa vyama vya ushirika na wananchi. Wadau hao ni pamoja na Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SCCULT)*, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi, Mpango wa Huduma na Ushauri wa Fedha Vijijini *(RFSP)*, Shirikisho la Vyama vya Ushirika Nchini *(TFC), SIDO, CRDB*, Benki Kuu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Benki Kuu, imekwishachukua hatua za awali za kutoa elimu ya ushirika, kuendesha semina ya elimu ya ujasiriamali kwa Maafisa Ushirika, Maafisa Mipango na Maendeleo ya Jamii ili nao waweze kuwafikishia wananchi elimu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuendesha kampeni kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kujiunga na *SACCOS* na hata vyama vya ushirika vya aina nyingine. Mheshimiwa Mbunge, natambua kauli mbiu za mwenge ya mwaka uliopita 2006 ilibeba ujumbe ufuatao: "Vyama bora vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)* vitaimarisha mitaji na kukuza ajira wote kwa pamoja tujenge uchumi". Hii ilikuwa ni moja ya kampeni iliyofanyika nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati uliopo mbele yetu sasa ni kutumia viongozi wa Serikali, Wabunge na kwa kushirikiana na wadau wengine wakiongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2005, kenye mikutano yote majimboni na sehemu nyingine watumie fursa hiyo kuwahamasisha wananchi kuanzisha na kujiunga kwa wingi kwenye vyama vya ushirika wa akiba na mikopo. Serikali itaendelea kutangaza manufaa ya *SACCOS* kwa njia ya redio, televisheni, mabango na vipeperushi ambavyo vitasambazwa hadi maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirikisho la vyama vya ushirika nchini *TFC* pamoja na Chama Kikuu cha Ushirika wa akiba na Mikopo *(SCCULT)* wanaendelea kuhamasisha wananchi juu ya uundaji na uendelezaji wa Ushirika wa *SACCOS* na aina nyingine za vyama kwa njia ya vipindi vya redio na televisheni. Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia watalaam usafiri ili kuwafikia walengwa huko vijijini. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali imeweza kutoa jumla ya pikipiki 75 kati ya mwaka 2001 – 2006 kwa baadhi ya Halmashauri na Miji ili kuwafikia wananchi wengi zaidi hususan vijijini.

Katika bajeti ya 2006/2007 Wizara yangu pia imetenga kiasi shilingi milioni 35 kwa ajili ya kuongeza pikipiki. Serikali itaangalia uwezekano wa kuwa na gari kila Wilaya ili maofisa waweze kutimiza majukumu ya kuanzisha, kufufua na kuimarisha vyama vya ushirika. Halmashauri ya Jiji/Miji/Wilaya hazina budi kushirikiana na Serikali Kuu katika kutumia vizuri nyenzo chache za usafiri kwenye maeneo yao. Serikali itaendelea kuwaandaa maafisa ushirika wawe waadifu, watalaamu na wenye uzalendo kama tunavyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi ya 2005.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa wajasiriamali wengi wamekuwa wakifanya vizuri sana katika usindikaji wa bidhaa zitokanazo na maziwa na matunda, lakini wamekuwa wakikosa soko la nje kutokana na tatizo la vifaa vya kupakia *(Packaging)*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mafunzo maalum ya kitalaam ya kutengeneza vifungashio hivyo ili kuwezesha soko la nje kwa wajasiriamali wetu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, wana *SIDO*. *SIDO* inatoa mafunzo ya wajasiriamali katika masuala ya ku-*pack* na ubora wa vyakula. Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* pia linatoa mafunzo hayo. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge aweze kuwasiliana pamoja na Wizara hiyo ya Viwanda,

Biashara na Masoko kusudi wananchi wake hao ambao amewatambua kupata mafunzo kutoka katika Taasisi hizo.

Na. 77

**Kilimo cha Majembe ya Kukokotwa na Wanyama**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya (2005 – 2010) inahimiza kilimo cha kisasa cha kutumia majembe ya kukokotwa na wanyama, mbolea, mbegu bora na kilimo cha umwagiliaji ili kuondokana na jembe la mkono; na kwa kuwa Serikali iliyopo madarakani ni ya CCM;

Je, Serikali imejiandaa vipi katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi hasa kwa wakulima wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu kwa makini sana swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunaelewa kwamba kilimo ndio msingi wa uchumi wetu katika modenaizesheni ya uchumi wa Tanzania. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 inaeleza wazi kuwa kilimo cha kisasa ni sharti muhimu katika kujenga uchumi wa kisasa. Kwa hiyo, kuwajengea uwezo wakulima na hasa wale wadogo ambao ndio wengi ni jambo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa wakulima wengi wana vishamba vidogo, mavuno yao pia ni kidogo na kilimo chao hakina tija. Kwa kutambua haya Wizara yangu inaendelea kubuni mikakati mbali mbali inayolenga kumwondolea mkulima vikwazo katika kuendeleza kilimo. Baadhi tu ya mikakati hiyo ni kama ifuatayo:-

Mkakati wa kuendeleza zana bora kwa kutumia wanyamakazi: Wizara yangu inaendelea kufanya ukarabati wa vituo vya Maksai na kuvipatia zana timilifu ili kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani na wakulima. Kufikia Oktoba 2006, vituo 55 vya wanyamakazi vilikwishakarabatiwa na kupewa plau, ripa, kaltiveta na rija za mikokoteni.

Aidha, ili kumwezesha mkulima kupata zana za kukokotwa na wanyamakazi kwa bei nafuu katika mwaka wa 2006/2007, utaratibu wa mikopo chini ya Mfuko wa Pembejeo umeanzishwa ambapo mikopo ya kununua zana za kukokotwa na wanyamakazi itatolewa kwa riba ya asilimia nane (8%) na kurejeshwa katika kipindi cha miaka mitatu. Wakulima wanashauriwa kuanzisha vyama vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* ili waweze kupata mikopo hiyo. Unafuu uliopo ni kwamba *SACCOS* zinaweza kuwadhamini wakulima kupata mikopo hata kama hawana dhamana ya mali isiyohamishika.

Mkakati mwingine ni Kuongeza upatikanaji na matumizi ya mbolea: Katika mwaka 2006/2007, Serikali imeongeza Bajeti kwa ajili ya ruzuku ya mbolea kutoka shilingi bilioni 7.486 kufikia shilingi bilioni 21.906. Aidha, Makampuni 11 yameishaingia mkataba na Serikali kwa ajili ya kusambaza mbolea yenye ruzuku ili kurahisisha upatikanaji wa mbolea na kwa muda muafaka. Serikali inaendelea kuboresha utaratibu huu wa mbolea ya ruzuku kila mwaka.

Mkakati mwingine ni Matumizi ya Mbegu bora: Makampuni 18 yamesajiliwa kwa ajili ya kuzalisha mbegu hapa nchini na tayari yamezalisha tani 4,616.5 mwaka 2005/2006. Lengo ni kuhamasisha uzalishaji uongezeke kufikia tani 20,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati mwingine unaoendelea ni wa Kilimo cha umwagiliaji: Kufikia mwaka 2005/2006, eneo linalomwagiliwa lilifikia hekta 264,388. Serikali inaendelea kuongeza eneo linalomwagiliwa na kuongeza tija ya uzalishaji katika skimu zilizokwishaendelezwa kufikia angalau hekta milioni moja. Mikakati inayotumika ni kukarabati skimu za umwagiliaji zilizochakaa na kujenga mabwawa na malambo ya kuhifadhi maji. Aidha, wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi wanahamasishwa kufungua mashamba makubwa ya mazao ya chakula na ya biashara yatakayotoa ajira kwa wananchi. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Namshukuru na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake aliyotoa. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, katika maelezo yote hayo aliyoeleza mikakati aliyonayo, hajaeleza hii mikakati ni ya muda gani, yaani itachukua kipindi cha muda gani kama ilivyo mikakati ya Elimu, tunajua kabisa kwamba Elimu ilianza 2002, ikaisha 2006. Je, Mkakati huu alioueleza na mwingine ambao hakueleza utaanza lini na utachukua muda gani ili kukamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika sehemu ya pili ya kuongeza mahitaji ya matumizi ya mbolea, amesema Serikali imetoa shilingi bilioni 7.4 kwa mwaka huu wa fedha.

Lakini, katika Mkoa wa Tabora na wa Ruvuma, mbolea haikuwafikia wananchi wale ambao walikuwa wamelengwa kupewa ruzuku, badala yake mbolea ile aina ya *NPK* ikapelekwa kwa makampuni ya kununua Tumbaku. Je, ipo fidia ya kuwalipa wakulima waliokosa hii mbolea au atawaambiaje wakulima wa Mkoa wa Tabora na wa Ruvuma ili wakae na matumaini kwamba mbolea ya ruzuku na wao wataipata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri! Naona Mheshimiwa Selelii anagusa na Jimbo la Mwenyekiti hapa Mezani!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, kwanza kabisa kuna mkakati mkubwa ambao tumeueleza mara nyingi sana. Hii ni mikakati midogo midogo tu ambayo iko ndani ya mkakati mkubwa wa kuendeleza sekta ya kilimo *(Agricultural Sector Development Programme)*. Na tumekwisha eleza kwamba mkakati huu ni wa miaka 7 ambao umeanza mwaka huu na utakamilika 2014 - baada ya miaka 7. Kwa hiyo *time frame* ipo kabisa ya mikakati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya mkakati mkubwa, laima kuwe na mikakati midogo midogo. Kwa hiyo, mikakati hii yote kwa kifupi tu ni kwamba *time frame* ni ya kutekeleza mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo wa miaka 7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea, kwanza naomba nimsahihishe kwamba sikusema mwaka huu tumetoa bilioni 7, nimesema tumeongeza kutoka bilioni 7.4 kwenda mpaka bilioni 20.906. Lakini pamoja na masahihisho hayo, mimi ningependa kusema kwamba katika utekelezaji wa suala zima la kupeleka mbolea ya ruzuku, yako matatizo ambayo yamejitokeza na hasa unapofikia katika ngazi ya Mkoa kwenda Wilayani na kwenda Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tumesimamia kabisa kuhakikisha kwamba makampuni yale ambayo tumeyapa mikataba yanapeleka mbolea mpaka kwenye vituo vikuu vya Mikoa. Sasa Kamati zile za Mikoa na Wilaya ambazo na Mheshimiwa Mbunge anatoka huko, anazijua na nadhani na yeye ni mmoja wapo, zinasimamia usambazaji wa mbolea kutoka ngazi ile ya Mkoa kwenda Wilayani na kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika jambo lolote kuna matatizo yanajitokeza na inawezekana katika hili, kuna matatizo yametokea katika usambazaji wa mbolea. Kilichobaki tu sasa ni kuangalia nini kimejitokeza katika Wilaya ya Nzega na kwa nini mbolea haikuwafikia baadhi ya wakulima ili turekebishe katika msimu unaokuja utaratibu huu mbolea iweze kuwafikia. *(Makofi)*

Na. 78

**Madai ya Wakulima wa Pamba Songwe**

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE (K.n.y. MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA)** aliliza:-

Kwa kuwa tarehe 14/08/2006 Waziri wakati akijibu Swali Namba 620, aliwathibitishia wakulima wa Pamba wa Jimbo la Songwe kwamba mara uhakiki wa madai yao ukishakamilika, mwezi Novemba 2006 malipo yataanza kutolewa; na kwa kuwa tangu uhakiki huo ukamilike, wakulima hao hawajaanza kulipwa fedha zao ambazo wamekuwa wakidai mwaka 1995 bila mafanikio;

Je, ni lini wakulima hao watalipwa fedha zao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, napenda kufanya masahihisho kidogo kwenye maelezo aliyotoa kama ifuatavyo:- Swali lililojibiwa tarehe 14/08/2006 ni Swali Na. 622 na siyo 620 kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu nililolitoa tarehe 14/08/2006 sikutamka kuwa ifikapo mwezi Novemba wakulima wa Songwe watalipwa madai yao ya fedha za Pamba. Nilichosema ni kuwa kazi ya uhakiki imekamilika katika ngazi ya Mkoa isipokuwa kazi ya uhakiki katika ngazi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kuwa si muda mrefu itakamilika na suala hilo litafikia tamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa kazi hiyo sasa imekamilika na Serikali imeanza kuchukua hatua katika kutimiza ahadi yake. Kwa kuanzia, Serikali ilileta hapa Bungeni katika Mkutano wa Nne wa Kikao cha Arobaini na Nne cha tarehe 16 Agosti, 2006. Kwa mujibu wa Azimio la Bunge Na. 4 la mwaka 2006, Bunge liliridhia madeni kadhaa ya Serikali yafutwe na mojawapo ya madeni hayo ni yale ya Vyama vya Ushirika ya kiasi cha shilingi 15 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matumizi ya Serikali yanafuata mwongozo wa Bajeti inayopitishwa na Bunge hili, Serikali itaendelea kushughulikia madeni ambayo yanahitaji kutoa malipo yakiwemo madeni ya wakulima yaliyohakikiwa. Tunamwomba Mbunge awe na subira kwa kuwa Serikali itatekeleza ahadi yake.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na masahihisho ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wakulima wa Wilaya ya Chunya mpaka sasa hawajaruhusiwa kulima zao la pamba kutokana na utafiti wa muda mrefu sana wa mdudu ajulikanaye kama *Red Ball*, Je, Serikali haioni kwamba kucheleweshwa malipo ya wakulima hawa kwa muda mrefu sana kuna wazidishia sana wananchi hawa umaskini wao walionao na hivyo kushindwa kabisa kutimiza malengo yao ya maendeleo na mahitaji ya kila siku? Maendeleo ninayoyazungumzia ni pamoja na ujenzi wa shule za Sekondari ambao hivi sasa unakwenda kwa kasi lakini uchangiaji umekuwa duni sana kwa sababu wananchi hawa hawana fedha. Sasa baada ya muda si mrefu kama Mheshimiwa Naibu Waziri anavyosema, ni lini basi wananchi hao watalipwa ili twende tukawaeleze na wapate matumaini kwamba wataenda kulipwa?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la madai ya wakulima, haliko katika Wilaya ya Chunya peke yake, ni tatizo ambalo linakabiliwa katika maeneo mengi ambako wakulima walikopwa mazao yao na hatimaye vyama vikashindwa kuwalipa. Ndiyo maana uhakiki wa madeni ya vyama vya ushirika kwa nchi nzima unatakiwa uigharimu Serikali shilingi 11 bilioni. Kwa hiyo, siyo tatizo dogo kwamba linaweza likashughulikiwa mara moja. Kwa hiyo, nilitaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili linashughulikiwa na hatua zitachukuliwa kulingana na uwezo wa fedha na Bunge hili litahusishwa kwa sababu ni suala la fedha za Serikali kwenda kuwalipa wale wanaodai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wakulima wa Chunya kuzuiwa kulima Pamba, hili ni suala la utafiti ambalo kwa kawaidxa utafiti unachukua muda mrefu. Haiwezekani ukawazuia halafu ukatafiti wiki moja ukapata jibu. Kwa hiyo, nadhani kwa sababu suala hili ni la kisayansi, lazima lipewe nafasi ili wakati uamuzi utakapofanyika

tuwe tumejiridhisha kwamba hatua yoyote itakayochukuliwa haitakuwa na madhara kwa kilimo cha zao la pamba na kwa uchumi wa nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Martha Mlata ili aendelee na swali linalofuata kadri ya kanuni yetu ya Bunge, saa 4.30 muda wa Maswali unakwisha. Lakini, ninaomba niwatangazie kwamba, tutaongeza muda wa ziada kwa kuwa tumetumia muda mwingine katika kuwasilisha Hati Mezani na leo tumekuwa na hati nyingi sana. Lakini vile vile majibu ya swali la kwanza yalikuwa ni marefu mno. Kwa hiyo, tutatumia muda wa nyongeza kidogo ili tuweze kuendelea na maswali ambayo yako kwenye Meza yetu kwa siku hii ya leo.

Na.79

**Udhibiti wa Mipaka Kuzuia Ujambazi**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la ujambazi hapa nchini limekuwa ni tatizo sugu, na kwa kuwa wimbi la ujambazi linatoka nje ya nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti mipaka ya nchi jirani ambako inaelekea wahalifu hutoka?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi sita baada ya Serikali ya Awamu ya Nne kuingia madarakani, ujambazi nchini ulikithiri baada ya majambazi wanaotuhumiwa kutoka nje ya nchi kushiriki katika vitendo vya uhalifu kwa kushirikiana na baadhi ya wananchi. Aidha, wahamiaji haramu wanaoingia Mikoa ya mipakani na baadhi ya wakimbizi waliopo kwenye Makambi yetu hapa nchini hususan Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa na Tabora walishiriki katika uhalifu huo. Uhalifu wa makosa hayo ni kama vile mauaji, unyang'anyi wa kutumia silaha, unyang'anyi wa kutumia nguvu, uvunjaji wa nyumba na kuiba, kupatikana na silaha na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua za kutokomeza ujambazi huu kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Hatua hizo ni pamoja na:-

Moja, kuanzisha operesheni maalum chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Jeshi la Polisi kushirikiana na vyombo vingine vya dola, kama vile mamlaka ya mapato, Idara ya Uhamiaji, Usalama wa Taifa na JWTZ, katika kudhibiti hali ya uhalifu na uingiaji haramu katika Mikoa ya Mipakani.

Pili, kufanya operesheni maalum katika misitu inayozunguka maeneo ya Mikoa husika kwa lengo la kuwasaka wahalifu wanaofanya vitendo vya ujambazi pamoja na kuwakamata wahalifu wanaoingiza na kumiliki silaha kinyume cha sheria.

Tatu, Jeshi la Polisi lina Askari Polisi katika Makambi ya Wikimbizi. Moja ya kazi zake Askari Polisi hao ni kuchunguza nyendo za Wakimbizi, ikiwa ni pamoja na kuwafanyia upekuzi wale wanaotiliwa mashaka kumiliki silaha na hata kushirikiana na wahalifu.

Nne, kuimarisha ushirikiano na nchi jirani katika kusaka majambazi yanayofanya uhalifu nchi hadi nchi kwa kutumia utaratibu wa mikutano ya ujirani mwema na kitengo cha *Interpol*.

Tano, kuanzisha Polisi Jamii kwa kushirikisha wananchi kuanzia kwenye Kata zao kwa kushirikiana na Polisi Kata.

Sita, kuanzisha mfuko maalum wa kuwazawadia wananchi watakaotoa taarifa zitakazofanikisha kukamatwa kwa silaha haramu.

Saba, kuimarisha doria na misako ya mara kwa mara mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani maalum kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jitihada zake za kuimarisha ulinzi na usalama nchini hasa katika Mikoa ya mipakani. Aidha, ninawashukuru Askari Polisi na vyombo vyote vya dola, pamoja na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, ninaomba niulize maswali mawili. Kwanza, kabisa namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba baadhi ya wahalifu hutumia njia zijulikanazo kama njia za panya na hatimaye kuwaacha maaskari ambao wanakuwa wakilinda milango mikuu ya kuingilia nchini?

(b) Kwa kuwa ujambazi umekuwa ukihusishwa sana mara kwa mara na wakimbizi ambao humiliki silaha kinyume cha sheria; Je, Serikali imepata mafanikio gani katika kusajili pamoja na matatizo yake kusajili silaha hizi na je, zoezi hili litakuwa ni endelevu au ni la muda mfupi tu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka nimhakikishie kwamba Serikali inatambua kwamba zipo njia za panya huko mipakani zinazotumiwa kwa vitendo mbalimbali vya uhalifu pamoja na kupitisha magendo ya bidhaa mbalimbali nchini. Hata hivyo Jeshi la Polisi, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola inafanya kila jitahada kuhakikisha kwamba tunawachukulia hatua wahalifu wa aina hii na kujipanga vizuri ili kuziba mianya yote ambayo inasababisha kuingiza vitendo vya uhalifu nchini mwetu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote naomba tuendelee kushirikiana ili kutupa taarifa hasa pale mnapoona kuna mahali ambapo watu wanatumia njia hizi za panya ili tuondoshe kabisa tatizo hili la njia za panya.

Kwa upande wa swali la pili la usajili wa silaha, Serikali katika mwaka huu iliweza kuzihakiki silaha 50,393 na kati ya hizo silaha 567 ziligundulika ziko kinyume cha sheria. Hivi sasa katika mchakato huo hata hivi karibuni Mkoa wa Kigoma tumeweza kuteketeza silaha haramu 2771 katika jitihada hizo za kuzuia udhibiti wa kutokuingia silaha haramu. Katika kipindi cha miezi mitatu katika Mikoa ya mipakani ningependa kutoa takwimu zifuatazo:- Kwa Mkoa wa Mara, jumla ya bunduki zilizokamatwa zilikuwa sita katika miezi ya Oktoba, Novemba na Desemba. Matukio ya ujambazi yaliyotokea yalikuwa sita na kesi zilizoko Mahakamani zilikuwa nne na kesi zilizo chini ya upelelezi ziko mbili. Kwa Mkoa wa Kagera kati ya miezi mitatu matukio ya ujambazi yalikuwa 34, majambazi yaliyokamatwa 134, silaha zilizokamatwa ni *SMG* saba, gobole 13, *Hand grenade* tatu na risasi 49.

Kwa upande wa Mkoa wa Rukwa matukio ya ujambazi yalikuwa 25, idadi ya majambazi ilikuwa 30, kesi ambazo ziko Mahakamani 15, kesi ambazo ziko chini ya upelelezi 10, silaha zilizokamatwa 19. *(Makofi)*

Kwa upande wa Mkoa wa Kigoma, katika miezi mitatu, matukio ya ujambazi yalikuwa 20, silaha zilizokamatwa *SMG nne*, bastola moja, gobole 17, mabomu mawili na risasi aina ya *SMG* na *SAR* 41 na *G3* 425. Matukio yaliyotokea ni 25 na kesi zilizoko Mahakamani ni nane. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 80

***The Great North Road***

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Waziri wa Miundombinu alipokuwa akitoa bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007 alisema pamoja na mambo mengine kuwa *The Great North Road* inapita Iringa – Dodoma – Babati kwenda Arusha; na kwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo aliombwa mara mbili bila mafanikio ya kutoa ufafanuzi wa tamshi hilo:-

Je, *The Great North Road* inayotoka *Capetown* kwenda Cairo inapita njia gani nchini Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *The Great North Road* inayotoka *Capetown* - Afrika Kusini kwenda Cairo - Misri inaingia Tanzania kwa kupitia mji mdogo wa Tunduma na hasa Miji ya Mbeya, Iringa, Dodoma, Babati, Arusha na hatimaye Namanga inayotoka kuelekea nchi jirani ya Kenya.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa ipo *school of thought* nyingine ambayo inasema barabara hii ya *Great North Road* inapita Tunduma, Mbeya, Chunya, Itigi, Babati, Arusha na Namanga: Je, Mheshimiwa Waziri ana- *reconcile* vipi hizi *school of thought* mbili ambazo hata mashuleni tulifundishwa?

(b) Ukifungua tovuti ya *The Great North Road* unakuta ramani ipo kwa nchi za Kusini mwa Tanzania, Zambia wanaonyesha ramani, Zimbabwe, *South Africa* na Kaskazini mwa Tanzania, Kenya, Sudan kuelekea Misri wanaonyesha ramani kwenye tovuti hiyo: Je, watalaam wa Tanzania wanashindwaje kuwasiliana na watengeneza tovuti hawa ili waweke kumbukumbu za Tanzania kwenye tovuti hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui Mheshimiwa Mwambalaswa alisoma miaka gani! Lakini nimweleze kabisa kwamba ni kweli kabisa kwamba barabara hiyo anayosema ya kupita Rungwe, Itigi ilikuwa inatumika kwa wale ambao tulikuwepo zamani na mabasi ya *railway*. Lakini sio kweli kwamba ndiyo ilikuwa *Great North Road.* Pamoja na matumizi hayo ilikuwa ni barabara muhimu, lakini ukweli ni kwamba *Great North Road* ni hiyo niliyoitaja na hii ni kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba, kwa mujibu wa *GN* Namba 471 ya mwaka 1962 sasa wakati huo sijui amemaliza kusoma sheria ya *Highway Act,* inaeleza wazi kwamba *Great North Road* na nitaisoma hapa, *Great North Road* inatokea Kenya kwenda Arusha, Dodoma mpaka Mbeya, Zambia ni maili 804 inatoka Namanga inaingia Oldonyosambu, inakwenda kwenye kona ya Dodoma pale Arusha, inaingia Arusha inakwenda Makuyuni inaingia Babati, Gendi, Bereko, inaingia Kolo, inaingia njia panda ya pale Kondoa pale Bicha kuingia pale Kondoa, inafika Mayamaya ambayo hapa imeandikwa 'Meiyameiya'; baada ya pale inaingia Dodoma, Fufu, *Ruaha River*, pale mpakani mwa Iringa, inaingia Izazi, Iringa, Ihemi hapa imeandikwa Iheme, Hulete, Sao, Makambako, Iyai hapa imeandikwa Iyari lakini ndiyo hiyo Iyai inaingia Igawa, Chimala, Igurusi njia panda pale Mbeya, Mbalizi, Mlowo, Vwawa na Tunduma na inaingiza Zambia ni kwa mujibu wa Sheria ya *Highway Act* na ninayo hapa. *(Makofi)*

Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kuhusu kuweka kwenye tovuti katika sheria mpya ya *highway* ambayo tunaitengeneza ya barabara ambayo tutakuja hapa Bungeni, suala la kuweka tovuti hizi njia kuu tutalizingatia. Nashukuru kwa mawazo yako. *(Makofi)*

Na. 81

**Reli ya Tabora – Mpanda**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, reli ya Tabora – Mpanda ndiyo njia pekee ya usafiri wa uhakika kwa maendeleo ya Mpanda na Mkoa wa Rukwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu na mfupi wa kuiboresha reli hii kwa kumwaga na kushindilia kokoto kwa kutumia mashine *(Trade Tamping Machine)* ili iwe imara zaidi, itakayowezesha treni ziongeze kasi na kupungua kwa ajali za mara kwa mara?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha reli ya sasa ambayo ni ndogo ya uzito wa ratili 45 na kuweka angalau ya ratili 75 na injini yenye uwezo mkubwa zaidi ili kuwezesha ongezeko la kasi ya mwendo na maendeleo kwa ujumla?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza idadi ya mabehewa ya abiria ya Daraja la I, II na III ili kupunguza msongamano uliopo sasa kutokana na kuwa na idadi ndogo ya mabehewa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ili kuweza kushindilia kokoto kwa kutumia mashine *(Tamping machine)* kwa ajili ya kuboresha reli hii iwe imara, inabidi ziwepo kokoto zisizopungua kina cha milimita 150 sawa na inchi sita. Awali tuta la reli ya Mpanda lilikuwa la udongo, Halmashauri ya Mpanda ilitoa kokoto mita za ujazo 75,000 zitumike katika kuimarisha reli hii.

Aidha, Shirika la Reli lilikuwa linachukua kokoto kutoka mgodi wake wa Tura na kuzipeleka reli ya Mpanda; kokoto hizo zimetumika kuimarisha sehemu korofi zinazotitia wakati wa mvua. Zoezi la kuweka kokoto katika njia linaendelea kufanyika kwa kutumia injini na mabehewa machache yaliyopo kwa kushindilia kwa njia ya kawaida hadi hapo itakapofika kina cha ujazo wa milimita 150 ambacho kinastahili kutumia mashine. Athari za kutumia mashine bila kufikia kina hicho ni udongo kuchanganyika na kokoto na kufanya njia kutokuwa imara.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa muda mfupi na mrefu wa kuboresha njia zote za Shirika la Reli Tanzania, hususan kwa kuongeza uzito wa reli.

Kwenye mkataba kati ya Serikali na mkodishwaji, Serikali ina mpango wa muda mrefu wa kutandika reli za uzito wa paundi 80 kwa yadi kutoka Kaliua hadi Mpanda (Km 210) na kwamba reli hizo zitang'olewa kutoka reli ya kati ambapo tumepanga reli ya kati kuweka paundi 120 kwa yadi.

Pamoja na kuzitumia reli hizo, madaraja hayo yataimarishwa pia ili kuruhusu utumiaji wa injini na mabehewa ya *axle load* ya tani 20 hatua itakayowezesha treni kubeba mzigo mkubwa na kuongeza kasi ya mwendo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Shirika la Reli Tanzania liko kwenye hatua za mwisho za kukodishwa, Kampuni itakayokodisha ndiyo itakayohusika na suala la kuongeza idadi ya mabehewa ya abiria ya Daraja I, II, na III kulingana na mwenendo wa biashara utakavyokuwa.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ambayo sina matumaini makubwa sana kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, pengine inaweza kuchukua muda mrefu hayo anayoyazungumza yakawa yametekelezeka. Lakini napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba; Kwa kutumia karakana ya Tabora, Morogoro na Dar es Salaam na mafundi tulionao na kama karakana hizo hizo zikiwezeshwa;

(a) Je, haiwezekana tukapa mabehewa angalau moja kila mwezi kutoka katika kila karakana ili kupunguza tatizo la mabehewa katika njia ya reli? *(Makofi)*

(b) Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba mapato yatokanayo na reli ya Mpanda pia yanachangiwa na barabara ya kutoka Sumbawanga kuja Mpanda? Mheshimiwa Waziri atashauriana na Waziri mwenzake anayeshughulikia masuala ya barabara kuhakikisha barabara hii inapitika ili kuweza kuleta ufanisi kwa reli ya Mpanda?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Arfi kwamba tukitumia karakana ambazo amezitaja tunaweza kutengeneza mabehewa tukapata ya kutosha. Tatizo tulilonalo ni uhaba wa fedha. Fedha ikipatikana,ninamhakikishia Mheshimiwa Arfi kwamba mabehewa haya kidogo tuliyonayo yanaweza kutengenezeka na tutaingiza katika reli. Lakini hivi sasa hela hatuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakubaliana na Mheshimiwa Arfi kwamba mapato yanayotokana na barabara hiyo ambayo amezungumza Mheshimiwa Mbunge yanachangia pia katika masuala ya uchumi wa nchi yetu na masuala mengine ya uchukuzi.

Napenda nimhakikishie kwamba barabara hii iko katika mpango wa matengenezo na kwa sababu Waziri anayehusika ni Waziri huyo huyo wa Miundombinu, tutampelekea ipasavyo suala hili na mwenzangu ambaye anasimamia masuala ya barabara nadhani amelisikia, litashughulikiwa.

Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba reli ya Mpanda itaboresha. Mimi mwenyewe nimeshaitembelea ninaijua hali yake na kufika pale ilipo ni kwamba kila leo tunahakikisha inakuwa *maintained* iweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba uchumi wa Mpanda unakua na tunategemea tukibadilisha hizo paundi za reli tulizosema tutaweza kubeba mzigo mzito na tutaweza kuboresha masuala ya uchukuzi na usafiri katika reli hii.

Na. 82

**Ukuaji wa Lugha ya Kiswahili**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Kwa kuwa, matumizi ya lugha ya Kiswahili yameongezeka kwa kiwango kikubwa duniani na kwa kuwa Tanzania ndiyo chimbuko la lugha hiyo:-

(a) Je, ni watalaamu wangapi wa Kiswahili wamesoma na kupeleka kuifundisha lugha hiyo nje ya nchi?

(b) Je, nchi hizo ni zipi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Tanzania ndiyo chimbuko la lugha ya Kiswahili na kwamba Kiswahili kimekua na kupanuka kwa kiwango kikubwa duniani. Kulingana na takwimu za *UNESCO*, Kiswahili kinazungumzwa na watu zaidi ya 180,000,000 duniani kote.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge, hivi karibuni mmeshuhudia kutambuliwa kwa Kiswahili kuwa lugha mojawapo rasmi katika vikao vya Umoja wa Afrika na Bunge la Afrika. Sio hayo tu, bali mtakumbuka kwamba mwaka 1986 *UNESCO* ilipitisha Azimio la kukubali Kiswahili kitumike kwenye vikao vyake vyote.

Pamoja na maazimio hayo, Kiswahili kimekuwa kikifundishwa na kutangazwa katika Vyuo na Idhaa mbalimbali za nje duniani. Nachukua nafasi hii kuwapongeza wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kukuza, kueneza na kuwezesha Kiswahili kutumika sehemu mbalimbali nje ya mipaka yetu na ughaibuni.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni vigumu kupata takwimu za watalaamu waliosoma Kiswahili na kupelekwa kufundisha Kiswahili nchi za nje kutokana na kutokuwepo utaratibu wa kuratibu shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara yangu inashirikiana na Wizara nyingine hususan Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi na sasa tunaandaa utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watalaamu wa kufundisha Kiswahili kwa wageni na pia masharti ya kiutumishi yatakayowalinda wanapokwenda kufundisha huko pindi wakihitajika. Ingawa wapo watalaamu wengi kutoka Tanzania wanaofundisha Kiswahili nchi za nje, wengi wao wapo huko kwa mikataba binafsi.

(b) Kama nilivyoeleza hapo awali, wataalam na watumiaji wa Kiswahili wameenea katika Vyuo vinavyofundisha Kiswahili na idhaa zinazotangaza kwa Kiswahili karibu duniani kote.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ziko nchi nyingi ambazo zinatoa watalaam wa Kiswahili zaidi ya Tanzania: Je, Wizara ina mpango/mkakati gani wa kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata nafasi zaidi kwenda kufundisha Kiswahili nchi za nje?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Kiswahili kinazungumzwa takribani duniani kote. Imekuwa ni vigumu sisi Wizarani pale na Serikali kwa ujumla kuratibu ni wa akina nani na wangapi wanakwenda nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tumeanza mkakati Wizarani pale kwa kushirikiana na taasisi zote zinazoendeleza Kiswahili kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na wengine ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata hizi fursa kila zinapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo ni kwamba huku nyuma ilikuwa ni vigumu sana kuweza ku- *track* kujua hawa watu wako wapi na wanafanya nini katika shughuli hizo. Kama nilivyosema mikataba mingi sana ya wanaofundisha Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani wameingia hivyo kwa mikataba binafsi.

Na. 83

**Kujenga Kituo cha Riadha Mkoa Manyara**

**MHE. MARTHA JACHI UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Mara, hasa Wilaya za Mbulu na Hanang, zinajulikana ndani na nje ya nchi kwa kutoa wanariadha bora nchini:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kujenga Kituo cha Riadha katika Mkoa huo ili kukuza vipaji vya vijana na kuboresha michezo nchini?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Umbulla kuwa upo umuhimu wa kujenga Kituo cha Riadha Mkoani Manyara, kwa sababu ni maarufu kwa mchezo huo. Mkoa wa Manyara ni chimbuko la wanariadha mashuhuri hapa nchini kama vile John Stephen, Gidamis Shahanga, Alfredo Shahanga, Marehemu John Bura, Agatius Masong, Thomas Robert, Francis Nahali na Marehemu Simon Robert. Hata hivyo, kwa sasa Serikali inashindwa kujenga Kituo cha Riadhaa Mkoani humo, kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge, kutokana na ufinyu wa bajeti. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, ninapenda wananchi waelewe kuwa ingawa Manyara ni Mkoa maarufu sana kwa mchezo wa riadhaa, vile vile iko Mikoa mingine ambayo imeonyesha juhudi kubwa ya kukuza mchezo huo ambao umeliletea Taifa letu sifa kubwa katika mashindano ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuwahamasisha Watanzania wote wenye uwezo wa kushiriki kuchangia ujenzi wa vituo vya michezo mbalimbali hapa nchini, ikiwemo riadhaa na michezo mingine katika Mikoa yote nchini.

Kwa hivi sasa, vituo ambavyo vipo na vinajiendesha vyenyewe kwa watu binafsi viko Dodoma, Arusha, Dar es Salaam, Mbulu, Hanang na Babati.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanariadha wachache wa Tanzania walioshinda katika michezo ya Tanzania, walioshinda katika michezo ya dunia kama alivyoainisha Mheshimiwa Naibu Waziri, wameweza kufanya hivyo kwa bahati na kwa jitihada zao wenyewe na sio kwa kujengewa uwezo kama wanavyojengewa wanariadha wengine huko Duniani: Je, Serikali haioni kwamba vijana wetu watakapojengewa uwezo kwa viwango vya kiulimwengu *(athretic global standards)* wanaweza wakashinda kwa wingi katika michezo ya dunia na kuiletea nchi yetu sifa kubwa kimichezo ya riadha? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli alichosema ni kwamba wanariadha maarufu wengi ni vipaji vyao wenyewe lakini vinaendelezwa na vyama husika. Nataka nimhakikishie kwamba sasa hivi tumejipanga vizuri, vyama vyote vya michezo kikiwemo Chama cha Riadha Tanzania tuna mkakati na *program* nzuri tu ya kuendeleza vijana hawa kwa utaratibu wa kuwapatia mafunzo.

Sasa hivi vikundi vyote vya riadha katika Mikoa yote tuna utaratibu kwanza kuwatambua katika kila Mkoa kwa vipaji vyao na umri wao na mbio wanazokimbia na kupatiwa mafunzo ya uhakika. Tunao utaratibu huo ambao tumeuandaa wa kuwapeleka vijana hawa nchi mbalimbali, tuna *group* ambalo tayari tumeshalipeleka *South Africa* na wengine wamekwenda nchi mbalimbali kwa makundi yao ili kupata mafunzo wafikie *standard* ya juu zaidi ya kimataifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali lililobakia, naomba tukubali kwamba tulipange katika utaratibu wa siku zitakazofuata ili dakika tano hizi zilizobakia kabla ya saa tano tutoe matangazo na hatimaye tuendelee na *order paper* ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea taarifa maalum kabisa kutoka kwa Katibu wa *Amani Forum.*

Waheshimiwa Wabunge, Bunge letu limeweza kupata heshima nyingine kubwa sana ndani ya nchi yetu, lakini pia katika nchi za Maziwa Makuu. Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni amechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa *Amani Forum* na ni Makamu Mwenyekiti wa *Regional* kama mnavyofahamu ziko nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, *DRC*, Zambia, Malawi hizo ndio zinazounganisha *regional* yetu *ya Amani Forum*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni amechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa *Regional* kwenye *Amani Forum*. Mheshimiwa Dr. Chegeni tunakupongeza, tunaomba utukumbuke Watanzania katika huo ufalme wako mpya ulioupata. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa leo tarehe 6 Februari, 2007 kutakuwa na kikao cha Kamati kuanzia saa tano asubuhi hii, Chumba Namba 231, ghorofa ya pili jengo la Utawala. Mheshimiwa Omar Kwaangw' - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, naye ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo tarehe 6 Februari, 2007 kuanzia saa 5.00 asubuhi hii, Ukumbi wa kukutana ni 231 ghorofa ya pili, katika jengo la Utawala.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira na Mwenyekiti wa Bunge, pia naye ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kwamba leo tarehe 6 Februari, 2007, wao kikao chao kitakuwa saa 7.00 mchana, kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika Ukumbi Namba 228 ghorofa ya nne jengo la Utawala. Mheshimiwa Job Ndugai anaomba sana Wajumbe wahudhurie bila kukosa.

Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba leo tarehe 6 mwezi wa pili, 2007 kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika Ukumbi Na. 133 ghorofa ya kwanza kuanzia saa 7 mchana. Mheshimiwa Haroub Maoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anawaomba Wajumbe wote wahudhurie bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo hapa matangazo ya wageni wetu walioshirikiana nasi katika kikao cha leo toka asubuhi. Kwanza naomba niwatambulishe wageni wetu kutoka kikundi cha akina mama cha *Chinangali West* cha Mjini Dodoma ambacho kinajishughulisha na biashara ndogo ndogo za uzalishaji mali. Jumla yao wako 40 na wao kwa ridhaa yao wamekuja kujifunza shughuli za Bunge zinavyoendeshwa.

Naomba hao akina mama wote kwa ujumla wao wasimame waweze kutambuliwa na Waheshimiwa Wabunge na tunashukuru sana kwa kuamua kuja kutembelea na kuona shughuli zetu. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Tunawashukuru, tunawakaribisha, tunaomba mhamasishe na vikundi vingine, nao wachukue uamuzi kama mliouchukua nyinyi. Tunawashukuru sana.

Nimeombwa na Mheshimiwa Suzan Lyimo niwatangazie Wajumbe wa Kamati Ndogo ya *TWPG* ya kuzindua *Strategic Plan* wakutane saa 7.00 ama mara baada ya

kusitisha shughuli za Bunge wote wafike katika Ofisi ya *TWPG* kwenye jengo la Utawala.

Nimeombwa na Mheshimiwa Raynald Mrope, nimwombe Mbunge yeyote ambaye amekosea na akachukua simu ya Mheshimiwa Mrope badala ya simu yake wakati tunapita kwenye lango Kuu kwenye masuala ya usalama kabla hatujaingia ndani ya Bunge. Kwa hiyo, Mheshimiwa Raynald Mrope anaomba sana simu hiyo irudishwe kwake ama utawala ili utaratibu wa kubadilishana simu hizo uweze kukamilika na Raynald Mrope aendelee kuwasiliana na wapiga kura wake kule Jimboni. *(Makofi)*

Nimeombwa na Mheshimiwa Haroub Masoud kwamba Mbunge wa Kwahani niwatambulishe wageni wake maalum ambaye ni Mheshimiwa Hassan Shaban - Mwenyekiti wa CCM (Wilaya) ya Kati. Nafikiri yupo hapa, ningeomba asimame kama yupo. *(Makofi)*

Masoud Said kutoka Koani, Alfa Said, Sabri Abdallah, Salum Nassor na Flaji Haroub. Flaji Haroub yeye ni mtoto wake Mheshimiwa Haroub Masoud na pia Ali Mwilu. Tunawakaribisha sana na mtoto wetu Flaji Haroub tunakushukuru kwa kuja kuona shughuli za baba hapa katika Ukumbi wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hafidhi Ali, Mbunge wa Dimani Zanzibar, ameomba niwatambulishe wageni wake kutoka Jimbo la Dimani Zanzibar. Wageni hao ni ndugu Ali Makame, Katibu Mwenezi wa Tawi la Dimani, Shamani Mrefu, Mjumbe wa Umoja wa Vijana; Ogori - Mjumbe wa Halmashauri ya Tawi; Othmani - Msimamizi wa Kampeni wa Jimbo hilo la Dimani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, ameniomba niwatambulishe wageni wake wafuatao:-

Kwanza, ameniomba kwa heshima na taadhima nimtambulishe mume wake mpenzi Seif Abdallah, yuko hapa leo. Naomba asimame. Halafu ameniomba pia nimtambulishe wapiga kura aliofuatana nao; nao ni mama Rweyongeza na wenzake. Naomba nao wasimame kwa pamoja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Ngasongwa, Waziri wa Mipango na Uwezeshaji, oh samahani! Samahani Alhaj, Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Ngasongwa, ameomba niwatangazie uwepo wa wageni wake. Wa kwanza ni Maina Juma Mrisho, maarufu kwa jina la Mkurugenzi, anatoka Malinyi, Mji Mdogo wa Makao Makuu wa Jimbo lake la Ulanga. Naomba naye huyo Mkurugenzi naye tumfahamu. *(Makofi)*

Halafu vile vile anasema, pia huyo ni mpiga debe wake mkubwa sana toka mwaka 1995 yuko naye tu na wako sambamba hawajaachana.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo ambayo nimeyapata kwenye Meza ya Spika na sasa tutaendelea na ajenda inayofuata.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Kanuni ya 55(3), wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu akijibu swali langu la nyongeza Namba 80 amesema sijui Mheshimiwa Mbunge alisoma wapi! Naomba afute usemi huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge ameomba Mwongozo wa Spika akitumia Kanuni ya 55 ambayo inatufanya Wabunge tunapozungumza ndani ya Ukumbi wa Bunge tusitoe maneno ambayo aidha, yanaweza kuudhi. Ningeomba Mheshimiwa Naibu Waziri aombe radhi na kutoa maelezo tu labda alilitamka hilo kwa maana ipi. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri ufanye hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yangu na *Hansard* itathibitisha, sikusema alisoma wapi. Nilisema, sijui Mheshimiwa Mbunge alisoma lini kwa sababu kwa mujibu wa Sheria niliyokuwa nayo ya mwaka 62 barabara ile tayari inapita katika mkondo niliouelezea. Sasa kama yeye alisoma kabla ya mwaka 62 basi inawezekana ndiyo maana anafikiria hivyo. Lakini kuanzia mwaka 62 na sheria inasema kwamba barabara hiyo inapitia Iringa – Dodoma na ndiyo maana nikasema sijui alisoma lini kwa maana ya mwaka. Lakini kama hakunielewa naomba radhi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru. Nafikiri ni uungwana tunapokuwa hapa Bungeni, unaweza ukasema neno ambalo linaweza likamkwaza mwingine. Tunakushukuru kwa hilo na Mheshimiwa Mwambalaswa nafikiri amelipokea.

Waheshimiwa Wajumbe, leo tutakuwa na kazi ya Hoja za Kamati. Kabla sijawaita watoa hoja za Kamati, ninawaomba niwasomee kifungu cha Kanuni Na. 43(5) kinachoambatana na kifungu (c) cha Kanuni hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa na utaratibu wa kupokea hoja za Mawaziri. Lakini Kanuni Na. 43 inazungumzia kuhusu uwasilishaji wa hoja za Kamati. Namba 43 inasema, isipokuwa kama Kanuni hizi zimeagiza vinginevyo, hakuna mjadala wowote utakaoendeshwa Bungeni ila tu kuhusu shughuli iliyoingizwa katika Kitabu cha Shughuli za Bunge na kuwekwa katika Orodha ya Shughuli kama ilivyofanyika leo.

Lakini vile vile Kanuni Na. 5 ya Kanuni hiyo inatuambia endapo hoja haikupelekwa kwenye Kamati na imewekwa kwenye orodha ya shughuli, au kama ilipelekwa kwenye Kamati na Kamati hiyo imemaliza kuishughulikia na imewekwa kwenye orodha ya shughuli, hoja itawasilishwa na kuamuliwa na Bunge kwa kufuata masharti yafuatayo:-

Sasa sharti litakalotuhusu ni lile linaloelezwa katika kifungu kidogo cha (c). Kamati zetu zimepitia hoja hizo zitakazowasilishwa na Wenyeviti na zitajadiliwa hapa ndani ya Bunge na kupitishwa. Kwa hiyo, ninaomba tuendelee sasa na utaratibu wetu na ninaomba nimwite mtoa hoja - Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama ili aanze kutoa hoja yake.

## HOJA ZA KAMATI

## TAARIFA YA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA

**PAMOJA NA MAPENDEKEZO NA MAONI YALIYO KATIKA TAARIFA HIYO**

**MHE. WILLIAM J. KUSILA – MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2006.

Kabla ya kufanya hivyo, kwa niaba ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa salam za rambirambi kwako wewe binafsi, kwa Bunge lako Tukufu, kwa wananchi wa Jimbo la Tunduru na kwa Taifa kwa ujumla, kwa kumpoteza Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amin.

Aidha, naungana na Watanzania wengine kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(11) ya Kanuni zetu za Bunge, Toleo la 2004, ninayo heshima kubwa kuwasilisha taarifa ya Kamati kwa mwaka 2006 mbele ya Bunge lako Tukufu. Kamati hii ina Wabunge 16 wafuatao:-

Mimi mwenyewe William J. Kusila, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Kapten George H. Mkuchika - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz , Mheshimiwa Kanali Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya na Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda. *(Makofi)*

Katika kipindi hiki, Kamati imekuwa ikiratibiwa na Makatibu wawili ambao ni Ndugu Elisa D. Mbise na Ndugu Athuman Hussein.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama yameainishwa katika Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizofanywa na Kamati kwa mwaka 2006, Kamati yangu ilitekeleza majukumu yake kama yalivyoanishwa kwenye Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004, kama ilivyofafanuliwa katika taarifa ambayo Waheshimiwa Wabunge wote mmeshagawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyojitokeza, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilibaini kuwa uundwaji wa Wizara mpya ya Usalama wa Raia umesaidia sana katika kudhibiti wimbi la ujambazi nchini. Vile vile, mabadiliko makubwa ya uongozi ndani ya Jeshi la Polisi yameleta mafanikio makubwa katika kupambana na uhalifu hasa wimbi la ujambazi. Kwa vipindi tofauti, Kamati imekuwa ikipokea Taarifa ya Ulinzi na

Usalama kutoka Wizara ya Usalama wa Raia ambazo zimekuwa zikionyesha mikakati mbalimbali iliyoandaliwa ili kupambana na uhalifu nchini.

Kamati ilibaini kuwa hatua alizochukua Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla katika kuhakikisha Usalama wa Raia na wakazi wengine nchini pamoja na mali zao, zimekuwa na mafanikio makubwa sana kijamii, kisiasa na hata kiuchumi. Kutokana na mafanikio hayo, wakati wa taarifa zake kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara zilizo chini ya Kamati hii, Wajumbe walimpongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kwa kufanikiwa kudhibiti wimbi la ujambazi nchini ambalo lilikuwa tishio la amani katika kipindi cha mwisho wa mwaka 2005 na mwanzoni mwa mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo kadhaa ambayo yanaendelea kuwa kero kubwa katika sekta ya Ulinzi na Usalama likiwemo tatizo la msongamano wa Wafungwa Magerezani. Kamati ilibaini kuwa miongoni mwa mambo yanayochangia msongamano mkubwa Magerezani ni pamoja na haya yafuatayo:-

- Masharti magumu ya dhamana;
- Sheria ya Kiwango cha Chini cha Adhabu;
- Sheria ya Makosa ya Kujamiiana;
- Ukosefu wa magari ya kuwapeleka watuhumiwa Mahakamani;
- Kutokupatikana kwa nakala za hukumu kwa wakati; na
- Kutokuwepo muda maalum wa kukamilisha upelelezi na Kutokutana kwa Kamati za kusukuma kesi *(Case Flow Management Committees)* katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipotembelea baadhi ya Kambi za Wakimbizi katika Mikoa ya Kigoma na Kagera, ilibaini ukubwa wa athari zinazotokana na kuwepo kwa Wakimbizi nchini. Katika maeneo hayo, kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira na mbaya zaidi ni uhalifu unaofanywa na baadhi ya wakimbizi kwa kutumia silaha. Kwa sababu hiyo, kazi kubwa ya viongozi wa Serikali katika maeneo hayo imekuwa ni kupambana na uhalifu unaosababishwa na Wakimbizi pamoja na Wahamiaji haramu badala ya kuhusika na kusimamia mambo ya maendeleo katika maeneo yao. Kamati ya Ulinzi na Usalama inaipongeza Serikali kwa msukumo mkubwa inaoendesha hivi sasa wa kuhakikisha kuwa wakimbizi wote wanarejea katika nchi zao na hatua ilizochukua hivi sasa kuyafunga baadhi ya makambi ya wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawapongeza sana Maafisa na Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda mipaka ya nchi yetu. Katika mwaka 2006, Kamati iliona jinsi Askari wanavyoshirikiana na wananchi kuhakikisha kwamba wananchi wanafanya shughuli zao za kujiletea maendeleo bila hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati ilibaini kazi nzuri iliyofanywa na *JKT* katika miradi yake licha ya kuwa na mitaji midogo sana.

Aidha, Kamati ilishuhudia juhudi za Kiwanda cha kutengeneza nguo cha *CAMISUMA* kinachomilikiwa kwa ubia baina ya *SUMA JKT* na *CAMI Textile Tanzania Ltd.*

Vile vile, Kamati iliona kazi inayofanywa na Kampuni ya Dawa za Binadamu ambayo ina dhima yenye kikomo, yaani *limited liability.* Kampuni hiyo inaitwa *TANZASINO* na inaendeshwa kwa ushirikiano baina ya *SUMA JKT* na Serikali ya China. Moja ya bidhaa zinazozalishwa na *TANZASINO* ni *Paracetamol* ziitwazo "*Tanzadol"* ambazo zina ubora wa Kimataifa. Kamati iliarifiwa kuwa *TANZASINO* imewahi kupata tuzo ya ubora wa bidhaa huko *New York.* Huo ni ushahidi kuwa *TANZASINO,* kampuni ambayo inamilikiwa na *SUMA JKT* kwa asilimia 55 inafanya vizuri licha ya kuwa na mtaji mdogo.

Pamoja na mafanikio hayo ya *TANZASINO*, Kamati iliarifiwa kuwa mchakato wa kupata leseni kwa ajili ya kutengeza bidhaa mpya ni mrefu kiasi cha kuifanya *TANZASINO* kutokuweza kutengeneza na kuingiza kwenye soko la bidhaa zake mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kufufua upya *JKT* kwa kuanza kuchukua vijana wanaojitolea umeonesha mafanikio makubwa sana. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kambi ya *JKT* Bulombora iliyoko Mkoani Kigoma na kuona jinsi vijana wanavyofanya kazi za uzalishaji mali pamoja na utunzaji wa mazingira. Aidha, Kamati ilishuhudia hali ya ukakamavu, nidhamu pamoja na usafi vitu ambavyo ni muhimu kwa vijana ambao ndiyo kielelezo cha uhai wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati yangu ilipofanya ziara Kisiwani Pemba, ilibaini kukosekana kwa Kituo cha Uhamiaji katika Bandari ya Pemba. Hata hivyo, Kamati ilipata maelezo ambayo yalionyesha kuwa uingiaji na utokaji wa wageni katika Kisiwa hicho umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Kwa melezo haya, kuendelea kutokuwepo kwa kituo cha Uhamiaji katika Bandari ya Pemba, ni hatari kwa usalama wa nchi yetu. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kurekebisha dosari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipofanya ziara Tanzania Visiwani iliridhika na kiwango cha juu cha ushirikiano miongoni mwa vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vile vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati inawapongeza sana viongozi wa vyombo hivyo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano huo mzuri na inashauri uendelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushirikiano wa Kamati, kuhusu suala la Wakimbizi, Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa katika nchi wanazotoka kwa sasa kuna amani, Serikali ihakikishe kwamba Wakimbizi wote wanarudi kwao haraka iwezekanavyo. Aidha, Kamati inashauri kuwa, Kambi zote za wakimbizi ambazo hazihudumiwi na Mashirika ya Kimataifa zifungwe na tungependa kuipongeza Serikali kwa hatua ambazo imeanza kuzichuikua za kufunga baadhi ya makambi hayo ya wakimbizi. *(Makofi)*

Sambamba na zoezi hilo, Serikali izungumze na Mashirika ya Kimataifa yanayohudumia wakimbizi pamoja na Serikali za nchi wanazotoka wakimbizi ili waangalie uwezekano wa kujenga kambi za wakimbizi ndani ya nchi wanazotoka wakati

taratibu nyingine za kuwatafutia makazi ya kudumu ndani ya nchi zao zinafanywa. *(Makofi)*

Kuhusu wahamiaji haramu, Serikali iendelee na operesheni ya kuwaondoa nchini kwa nguvu na operesheni hiyo iwe ya kudumu. *(Makofi)*

Vile vile, ili kupambana na tatizo la uhamiaji haramu unaoambatana na uhalifu, Kamati ilishauri kuwa wananchi wapewe Elimu ya Uraia ili waweze kutoa taarifa kwa vyombo husika pale wanapoona watu kama hao katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kubaini kutokuwepo kwa Sheria ya Zimamoto, inashauri kuwa Serikali iandae Muswada wa Sheria ya Zimamoto haraka ili Bunge liujadili na hatimaye kuupitisha ili Zimamoto iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Sambamba na hilo, muundo na utumishi wa Zimamoto uwekwe bayana ili kudhihirisha taratibu na vigezo katika kumwendeleza mtumishi anayehusika na Zimamoto na uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na kwamba hali ya Mipaka yetu ni shwari Kamati inashauri kwamba Serikali ihakikishe barabara za Mikoa ya mipakani zinapitika wakati wote wa mwaka ili pamoja na mambo mengine, kurahisisha shughuli za ulinzi pamoja na shughuli za biashara kati ya nchi yetu na majirani wanaotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha shughuli za ulinzi mipakani, Kamati inashauri kwamba Mikoa yote hasa ya mipakani kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi Tanzania wafanye jitihada ya kuanzisha na kuimarisha mafunzo ya mgambo na ili kutekeleza hilo, Sekretarieti za Mikoa inayohusika zihakikishe kwamba zinatenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya kuendesha shughuli za mgambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mambo yaliyoleta katika nchi hii ni Jeshi la kujenga Taifa, ni maoni ya Kamati kwamba kwa hivi sasa Taifa linahitaji sana *JKT* ili kuimarisha mshikamano na uzalendo miongoni mwa Watanzania, kitu ambacho ndicho tumekuwa tukijivunia kwa miaka mingi. Kamati inashauri kwamba Serikali irudishe mafunzo ya *JKT* kwa vijana wote waliomaliza Kidato cha Sita pamoja na wale waliohitimu Vyuo mbalimbali kama ilivyokuwa awali. *(Makofi)*

Kwa kuanzia, Kamati inashauri kwamba utaratibu huu uanze kwa kuwachukua vijana wote waliohitimu Chuo Kikuu. Kwa kuwa Sheria ya Vijana kujiunga na *JKT* kwa lazima, yaani *Compulsory National Service Training* bado ipo, Serikali ianze utekelezaji wake katika mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Sambamba na ushauri huu ni maoni ya Kamati hii kuwa Jeshi la Kujenga Taifa lipanuliwe kwa lengo la Kambi kila Wilaya ili kutoa mafunzo ya ufundi na ulinzi kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira kwa vijana limepewa uzito mkubwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Ni maoni ya Kamati kwamba kama *JKT* ikiimarishwa ipasavyo, vijana wengi watapata ajira kwa kuajiriwa au kujiajiri wenyewe baada ya kumaliza mafunzo ya *JKT*.

Kamati inashauri kwamba Serikali iangalie uwezekano kwa siku zijazo kupeleka fedha za mikopo kwa vijana kupitia *JKT* kama ilivyo kwa fedha zinazopelekwa Mikoani ili wale wanaohitimu mafunzo na stadi mbalimbali za kazi wapewe mikopo ya vifaa pamoja na mitaji ya kuanzisha shughuli za kiuchumi. Utaratibu huu utakuwa na matokeo makubwa zaidi kwa kuwa watakaokopeshwa watakuwa na ujuzi wa kuzalisha mali na hivyo kuweza kurejesha mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo umuhimu wa kuangalia kwa karibu zaidi Vituo vya Polisi vilivyo mipakani kwa maana ya kuweka Askari Polisi wa kutosha pamoja na vifaa vya kufanyia kazi. Katika Wilaya ya Tarime kwa mfano, wakati nchi jirani imeweka Askari Polisi mia mbili katika vituo vyao vya mpakani, vituo vyetu vina Askari wanane tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tarime ni moja ya Wilaya zenye matukio mengi ya uhalifu hapa nchini kwetu na kiwango kikubwa cha mauaji ya watu yanayotokana na mapigano ya kikabila. Kamati inashauri kwamba idadi ya askari katika Wilaya hiyo pamoja na vifaa vya kutendea kazi hasa magari, iongezwe.

Aidha, Wilaya nyingine zilizopo mipakani zipatiwe Ofisi zenye hadhi pamoja na usafiri angalau kwa kuanzia na pikipiki. Vile vile Kamati inashauri kwamba kwa madhumuni ya kutatua makazi ya Askari wote katika Jeshi la Polisi, Magereza na Jeshi la Wananchi wa Tanzania uwepo mpango wa kujenga maghorofa awamu kwa awamu ndani ya makambi hayo katika Mikoa yote nchini ili kutatua tatizo kubwa la makazi ya Askari katika majeshi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza hatua ya Mheshimiwa Rais kuteua Majaji kwa lengo la kuimarisha Mahakama. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, juhudi za kuajiri Mahakimu wa kutosha ziendelezwe ili kuondoa tatizo la kuchelewa kwa kesi ambalo linasababisha msongamano wa mahabusu na wafungwa Magerezani. Aidha, masharti ya dhamana yaangaliwe upya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba Kamati za kusukuma kesi zinafanya kazi katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira katika vyombo vya Ulinzi na Usalama ni maoni ya Kamati kuwa iwapo vijana wanaopitia mafunzo ya *JKT* wataendelea kupewa nafasi zaidi, ulinzi na kujituma katika masuala yanayohusu Usalama wa Raia na mali zao vitaboreka na amani itaendelea kustawi nchini. Aidha, pale inapowezekana vyombo vyote vya ulinzi viwe na utaratibu wa kutembelea Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu ili kuwahamasisha wasomi wengi kujiunga navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa hali ya mipaka yote ni shwari, Kamati inashauri kuwa kipindi hiki ni kipindi kizuri kwa vyombo vya Ulinzi na usalama kuendelea kujiimarisha. Vile vile Kamati inashauri kuwa Sera ya usalama iwaunganishe wadau wote wa ulinzi na usalama katika utekelezaji wa masuala ya kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha, Kamati yangu inawashukuru sana Waheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya - Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu - Waziri wa Usalama wa Raia na Mheshimiwa Joseph Mungai - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano mzuri sana ambao waliupatia Kamati yetu na ambao ulikuwa wa kiwango cha juu sana.

Naomba pia kuwashukuru Mheshimiwa Omari Yussuf Mzee - Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed na Mheshimiwa Laurence K. Masha - Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wote Kamati ilipowahitaji. Shukrani maalum ni kwa Watendaji wa Wizara zilizo chini ya Kamati hii pamoja na vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kutekeleza ipasavyo majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kukushukuru wewe binafsi kwa uteuzi wako. Namalizia kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika, kwa uteuzi wake alioufanya kwa Waheshimiwa Wabunge ambao aliwateua kuwa Wajumbe wa Kamati hii. Utendaji kazi wao umekuwa makini, wa kujituma na uvumilivu wa hali ya juu sana jambo ambalo sio tu ni muhimu kwa Ulinzi na Usalama wa Taifa hili, bali pia ni la lazima kwa ajili ya uhai wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED J. SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa hoja za Kamati baada ya Mheshimiwa Mwenyekiti kutoa hoja, tunakuwa tumetarajia wale wote wanaotaka kuchangia hoja hii wanakuwa wameshawasilisha majina yao hapa. Sasa ninaomba kuwaambia ya kwamba, nimepokea jina la mtu mmoja tu, Mheshimiwa Felix Kijiko ndio atakayechangia hoja hii na baada ya hapo tutaendelea na utaratibu kama Serikali itapenda kutoa maelezo ya ziada na mwishoni mtoa hoja atajibu hoja ya Mheshimiwa Kijiko na baadaye tutaamua hoja hii tuipitishe na tutaendelea na hoja inayofuata. Kwa hali hiyo naomba nimuite Mheshimiwa Felix Kijiko, ili atoe mchango wake katika hoja ambayo iko mbele yetu.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa ripoti nzuri ambayo imetoka. Ni ripoti inayojieleza vizuri sana, lakini mimi naizungumza hii kwa sababu Wilaya yangu inaathirika na suala hili la wakimbizi na nina taarifa inayoeleza kwamba kweli Kamati hii ilifika kule kwenye Wilaya yangu mahali ambapo wakimbizi wapo na Kamati hiyo ilizungukia mipaka na kuona athari ambazo kwa kweli zinaweza zikawa zinatokana na ujio wa Wakimbizi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi wa Wilaya ya Kibondo, haishi kwa amani na utulivu kutokana na mashambulizi yanayotokana kila wakati kutoka kwa Wakimbizi, wanafanya ujambazi, lakini kwa makusudi mazima ni kwamba tunao walinzi walioko kutoka kwenye vyombo vya Ulinzi na Usalama, lakini kwa makusudi mazima ni kwamba tunao walinzi walioko kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Wapo! Kinachasikitisha ni kwamba, kwa kweli hayo matukio yote ya mauaji yanayofanyika, hakuna tukio ambalo limekamatwa na mtu wa chombo cha ulinzi na usalama zaidi ya wananchi wenyewe.

Nilijaribu kufuatilia sana suala hili, nikagudua kwamba, kusema kweli watu walioko, walinzi walioko kwenye vyombo vya ulinzi na usalama ni wachache, hawatoshi. Sijui kama hii Kamati iligundua hilo. Ni wachache mno, ni wachache mno kwa sababu

mpaka mkubwa kwa makusudi mazima ni lazima sasa vyombo vinavyohusika na wale walinzi wa vyombo vya ulinzi na usalama walioko kule katika Wilaya ya Kibondo mahali ambapo tunapakana na Burundi waongeze watumishi ili kuweza kukabiliana na suala la ujambazi linaloendelea kila siku.

Katika Wilaya ya Kibondo, mpambanaji mkubwa na suala la ujambazi unakuta ni *DC,* anashindwa kufanya kazi za Serikali kwa kupambana na ujambazi. *OCD* ndio hakai kabisa ofisini kwake. Lakini yote hayo yanafanyika baada ya matukio kufanyika ama kutokea, sasa katika kufuatilia hili na katika kuzungumza na wapiga kura wangu, tumekuja kujikuta kwamba mbali na uchache wa watumishi walioko kwenye vyombo vya Ulinzi na Usalama, lakini kinachosababisha kingine ni suala la nyumba. Askari hawana nyumba na kutokana na tatizo hilo, hata hizi Wizara zinazohusika kuwapeleka watu kule inakuwa ni kazi kubwa sana kwa sababu hawapati mahali pa kuwalaza. Kwa hiyo, wanashindwa kupeleka hao watu kule.

Lakini nilikuwa najiuliza kitu kimoja juzi nikiwa Jimboni, nikazungumza na watu, wanasema, utaratibu ambao umewekwa na Serikali ni kuwahusisha ama ni wakukubali ombi la hizi nchi nyingine kujiunga na Jumuiya ya *East Africa*, Burundi ni moja wapo, ambayo ina wakimbizi wengi sana Tanzania hasa Mkoa wa Kigoma na Kagera kidogo. Hawa watu tukishawahalalisha kwamba wamejiunga na Jumuiya, wakati Serikali inajikita kwamba sasa ni lazima wakimbizi warudi kwao, kambi moja imefungwa, lakini bado na kambi kama nne sasa zimebaki katika Wilaya Kibondo.

Sasa wakishahalalishwa kwamba wamejiunga na hii Jumuiya ya *East Africa,* sijui hatuoni kwamba tutakuwa tunawakaribisha? Hii maana ya kusema wakimbizi waondoke, mimi nadhani ni nadharia tu, lakini ni kwamba hatuko *serious* kwamba wakimbizi watatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hilo tukio litafanyika wakati wakimbizi tunao ndani ya Tanzania, sasa wakishakubaliwa kwamba wajiunge na *East Africa* sijui kama kutakuwa na msimamo kwenye Vikao Vikuu vya *East Africa* vitakavyohakikisha kwamba wakimbizi waliotangulia kuja ama wanaoishi katika Mikoa iliyokumbwa na wakimbizi wanarudi kabla ya zoezi hilo kufanyika. Hili nilikuwa nalizungumza tu kwa sababu linagusa Wizara nyingi, mbali na Wizara zinazohusika na vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Lakini kuna tatizo lingine ambalo liko, kubwa tu, nalo ni tatizo la hawa watumishi wa vyombo vya Ulinzi na Usalama kukaa kwenye vituo kwa muda mrefu, hali inayosababisha kujenga mazoea makubwa sana na hawa wakimbizi. Sio wakimbizi tu, mtu ukishakuwa na mazoea na adui, kumdhibiti inakuwa ni kazi.

Sasa labda ningeomba hilo pia tujaribu kuangalia kwamba hawa wanaopelekwa kule kwenda kufanya kazi, niliuliza nikasikia wanaokwenda kulinda kwenye makambi wanakaa muda wa miezi sita halafu wanarudi, anayepata bahati kukaa kwa muda wa mwaka mmoja ni bahati yake binafsi. Lakini nilikuwa nadhani kwamba ni sasa muda umefika tuwe na muda maalum wa kuhakikisha kwamba hawa wakimbizi wanakaa kwa kipindi maalum *then* waondoke kwa sababu kuwaachia ni kuzidi kuwapa nafasi ya kujenga mazoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *inter-marriages* nyingi sana zinatokea kule kwetu mpakani na wengine wanatokana na hawa hawa walioko kwenye vyombo vya Ulinzi na Usalama. Sasa umekwishakwenda kuoa Burundi, sijui kama huo udhibiti utaufanya vizuri sana. Lakini kama tungekuwa na muda maalum wa kuzuia kwamba huyu mtumishi akae kwenye kituo kwa muda fulani, hayo yote yasingetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nimelizungumza kwa sababu limekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma na Kagera. Ujambazi sasa hivi unakwenda Kigoma. Kama umefika Kigoma unakwenda Kibondo, unakwenda Kasulu, huwezi ukaenda bila kupata *escort* ya Polisi. Sasa hii hali isiwepo na kuhakikisha kwamba Polisi anafanya kazi yake mbali ya hiyo ya *escort* ya watu kwenye mabasi utakuta kuna Polisi, viongozi wa Serikali kule hawawezi kwenda mpaka wapate *escort* ya Polisi. Ilikuwa ni kuhamasisha watumishi wa vyombo vya Ulinzi na Usalama waongeze watumishi wa kwenda kupambana na hali ya ujambazi ambao umekuwa ni tishio sana kwa watu wa kule Kibondo.

Haya imebidi niyazungumze kwa sababu wakati wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anasoma taarifa yake ilikuwa imenifurahisha kwa sababu amegusa vipengele vyote ambavyo kama vitafanyiwa kazi, ama ushauri ambao umetolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama kama utafanyiwa kazi kama ulivyoainishwa kwenye jendwali hili waliloligawa, mimi nadhani hali itakuwa ni ya kuridhisha. Nilikuwa naomba kwamba, basi tuheshimu hii taarifa ya Ulinzi na Usalama ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilikuwa nasema kwamba ni taarifa iliyonihamasisha, nikaona kwamba niizungumzie tu kwa sababu kwangu ni kero kubwa sana na kwa wananchi wa Kigoma na Kagera ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, natoa shukrani zangu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa maelekezo yangu kuhusu utaratibu wa kuchangia hoja, nimeletewa majina ya Wabunge wengine watatu zaidi wakiomba kuchangia hoja hii. Naomba niwaambie kwamba ninayapokea majina hayo, kwa sababu yote ni ya Wabunge wageni ambao labda utaratibu huu ulikuwa bado haujaeleweka vizuri kwao.

Lakini ninaomba tu niseme kwamba, tunapochukua *Order Paper* ya siku, tafadhali naomba tuipitie na kila kilichowekwa kwenye *Order Paper,* kama unaona una hoja ya kuchangia ndani ya Bunge ni wakati muafaka wa kuomba toka asubuhi tunapoanza maswali na majibu. Kwa hiyo, tunakuwa tumeshajiweka katika utaratibu wa kujua ni wangapi wangependa kuchangia hoja hiyo.

Lakini kwa hali ilivyojitokeza leo, ninaomba nirudie tena, utaratibu wa kuchangia hoja za Kamati, ninaomba kama tunavyofanya katika utaratibu wa kuchangia hoja nyingine ndani ya Bunge. Kwa hiyo, toka asubuhi, Waheshimiwa Wabunge tuangalie na tulete maombi yetu.

Kwa hiyo, ninapokea maombi ya hao Waheshimiwa Watatu, nitawapa muda wa kuzungumza na nadhani sasa hoja ya maliasili tutaiahirisha kidogo mpaka tumalize hoja

hii kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wameongeza katika orodha ya wachangiaji. Basi nitamwita Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, lakini kuna Mheshimiwa Felista Bura na Mheshimiwa Sereweji nao pia wameomba kuchangia mada hii.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Kwanza ningependa kukushukuru kwa kutoa maelezo yako, juu ya utaratibu mzima wa kuchangia hoja kama hizi.

Pili, nami kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili katika kipindi hiki, basi ningependa kuchukua nafasi hii kutoa salamu zangu za pole kwa wafiwa wa mwenzetu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti na wengi wote ambao wametuaga duniani hapa baada ya ajali ya ndege, Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema Peponi na kuwataka wanafamilia wawe na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ningependa kuchangia kidogo tu na eneo ambalo ni eneo la kurudisha utaratibu wa zamani wa *Compulsory National Service Training* kwa vijana ambao wanamaliza Kidato cha Sita na Vyuo, pamoja na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuchangia hili kwa sababu za msingi kabisa kwamba huko nyuma tulikotoka tulikuwa na utaratibu huu mzuri sana, kwamba vijana waliokuwa wanamaliza Kidato cha Sita na wale ambao walikuwa wanamaliza Vyuo Vikuu walikuwa wanakwenda *JKT*. Utaratibu huu ulisaidia mambo mengi sana katika nchi yetu hii. Kwanza, ulijenga uzalendo kwa vijana wetu hawa; Pili, ulijenga mshikamano mkubwa wa utaifa katika nchi yetu; tatu, ulisaidia sana kukuza lugha ya Kiswahili; Nne, ulisaidia sana kujenga ukakamavu na uaminifu na kuweka msingi mzuri wa kujitegemea kwa vijana wanapomaliza masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, najua kulikuwa na sababu za msingi za kuyasimamisha mafunzo haya. Nasema kuyasimamisha kwa sababu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi amesema sheria hii bado ipo, kwa hiyo, tunaweza kabisa kuirudisha.

Kama unataka kufanya utafiti, haya utayaona kwa wale vijana ambao wamepitia katika Jeshi la Kujenga Taifa, ambao sasa ni watu wazima na vijana ambao hawakupata bahati hii kuna tofauti kubwa kabisa. Vijana waliopitia Jeshi la Kujenga Taifa wa zamani utawakuta wanauzalendo mzuri tu, wako tayari kulitumikia Taifa lao bila maswali yoyote. Wana ukakamavu mzuri tu, wanajiamini katika maeneo mbalimbali na wanaijua sana nchi yao na wanaipenda sana.

Lakini kwa vijana ambao hakupitia, sisemi hakuna vijana wazalendo, lakini nina uhakika kabisa utaona kuna kasoro kasoro miongoni mwao nyingi tu, kiasi ambacho wakati mwingine wanaweza wakafanya jambo kwa sababu ya kukosa uzalendo, kwa sababu ya kushindwa kuielewa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hali hii ni hatari sana. Kama kuna kipindi ambacho tutakiwa tuwe na mambo haya, ni sasa hivi kwa sababu dunia ina mambo mengi. Juzi tumepitisha hapa Sheria ya Ugaidi katika nchi yetu. Juzi tumekuwa na Semina ya Usalama ya jinsi gani nchi inaweza kujilinda na watu wake.

Haya yote yamekuja kwa sababu ya hali halisi ya dunia hii ambayo uadui, kutokuaminiana kunachukua nafasi kubwa sana na kwa kuwa watu siku hizi ni wasomi wazuri sana, teknolojia inaongezeka na sayansi, uwezekano wa kuangamizana ni mkubwa sana. Sasa ya moja kati ya maeneo ambayo yanaweza kusaidia kuilinda nchi yetu na kujilinda sisi wenyewe ni kuwajaza uzalendo vijana wetu. Tukiwajaza uzalendo vijana wetu uwezekano wa nchi yetu kuendelea na amani na usalama ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipata bahati ya kukaa sana nje na kutembea sana ma-*continent* yote haya. Moja kati ya mambo ambayo wenzetu wanayajali sana ni haya ya uzalendo, haya ya kuwapeleka vijana Jeshini yanafanyika mpaka leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifika nchi moja ilikuwa siku ya kukumbuka uhuru wao, nikawakuta vijana wamekaa kando ya redio na televisheni wanaangalia matukio yaliyopita huko nyuma, jinsi nchi yao ilivyokuwa inavamiwa na sasa jinsi nchi yao ilivyo. Wale vijana lugha wanayozungumza pale ni ya uzalendo wa nchi yao! Utafikiri walikuwepo kipindi hicho, pengine hata baba yake alikuwa hajazaliwa bado. Lakini kwa sababu ya haya ya kuelimisha kupitia *JKT,* historia wamejazwa na uzalendo kweli kweli, huwezi kumwambia kitu chochote kile! Wako tayari kutembea usiku na mchana kwenda kuilinda nchi yao.

Sisi haya tulikuwanayo, tunayo mpaka hivi sasa, lakini kasi yake imepungua. Kwa hiyo, ninaomba sana suala la kurudisha *JKT* kwa vijana wetu wanaomaliza Kidato cha Sita na Vyuo, na Vyuo Vikuu, Serikali irudishe mara moja iwezekanavyo. Dunia inageuka! Kwanza *JKT* pamoja na kwamba tunaweza tukasema gharama na mambo mengine, lakini *JKT* mahali ambapo vijana wanaweza kujilisha wao wenyewe, inawezekana kabisa ndivyo tulivyokuwa tunafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hakuna sababu ya kuchelewa, hakuna sababu ya kuhofia ya kutokurudisha utaratibu huu wa vijana wetu kwenda *JKT* wanapomaliza masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, narudia tena, naomba Serikali ikaandae utaratibu ili utaratibu huu uanze na mimi nitaomba kwa wale wenzetu wanaochupia chupia jenda hizi za kutaka kutukatisha tamaa, kwa hili waliache, ama tukubaliane nao ili utaratibu huu uwezekane, tuilinde nchi yetu tujenge uzalendo wetu, maana ninajua wako wenzetu wengine hawana cha kufanya wanasubiri ajenda kama hizi wachupie. Hao hawatakuwa wenzetu katika nchi hii, hawatutakii mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia tena kwa kusema naomba Serikali utaratibu wa kuwapeleka vijana wanaomaliza *Form Six* ama Kidato cha Sita, Vyuo na Vyuo Vikuu kwenda *JKT* hata kwa miezi sita tu naomba Serikali irudishe. Kwa hayo, machache nasema ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia ripoti ya Kamati ya Ulinzi na Usalama na niwapongeze Wanakamati hawa kwa kazi nzuri walioifanya na kuleta taarifa Mezani kwako.

Lakini kabla sijafanya kazi ya kuchangia, nianze kwa kuwapa pole wananchi wa Tunduru kwa kufiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Marehemu Juma Akukweti na kwa

niaba ya wanawake wa Dodoma, nimpe pole sana mwanamke mwenzetu, mama Akukweti kwa msiba mkubwa alioupata na pia sijawasahau wale wenzetu wamefariki katika ajali ya ndege ya Mbeya. Naendelea kuwapa pole familia zilizopata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa pongezi sana Mheshimiwa Asha-Rose Migiro, kwa nafasi aliyoipata na Mheshimiwa Bernard Membe na Mheshimiwa Batilda Burian na Manaibu Mawaziri, Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Kayombo kwa nafasi zao walizozipata na niwaahidi tu kwamba sisi wananchi wa Dodoma tuko pamoja nao kusaidiana nao katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kuchangia katika ripoti hii iliyoletwa kwetu na Kamati ya Ulinzi na Usalama, jambo ambalo nimeona sio vizuri likapitia bila ya mimi kuchangia katika ripoti hii. Ukurasa wa 10 Wanakamati walipofanya ziara katika Kisiwa cha Pemba, walibaini kwamba hakuna Kituo cha Uhamiaji, jambo ambalo ni hatari sana katika usalama wa Taifa na ukizingatia kwamba Watanzania hatuna Vitambulisho vya Uraia. Kama kweli Kituo cha Pemba hakina Kituo cha Uhamiaji, ina maana tuna raia wengi waliovamia nchi yetu kupitia Kituo cha Bandari ya Pemba na wanaishi nchini pasipo na kibali na bila Serikali ya nchi yetu kujua kwamba kuna watu wanaoishi nchini kwa kupitia Bandari ya Pemba pasipo kufahamika.

Naiomba Serikali kwamba hili jambo litizamwe kwa mtazamo mwingine kwa sababu ni jambo la hatari sana na nashindwa kujua kwamba kama bandari haina Kituo cha Uhamiaji, inawezekana kabisa kwamba bandari hiyo pia ikatumika kuingiza silaha za hatari na ikatumika kuingiza hata watu wanaoweza wakachochea usalama wa nchi yetu.

Nikikumbuka kwamba kwa siku zilizopita, kuna baadhi ya wananchi walihamia Kenya wakiogopa usalama na vurugu zilizotokea Kenya na sasa nasita kusema kwamba inawezekana wale waliokimbia wakaenda Kenya kuomba hifadhi, pengine hawakuwa wananchi, pengine hawakuwa Wazalendo kwa sababu bandari ile mtu yoyote anaingia na taarifa ya Kamati inasema kwamba kuna uingiaji na utokaji wa wageni katika Kisiwa na unaongezeka. Yaani uingiaji na utokaji wa wageni katika Kisiwa hicho unaongezeka siku hadi siku. Napata wasiwasi kwamba usalama wa Kisiwa hicho uko hatarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa waangalie namna ya kuweka Kituo cha Uhamiaji katika Bandari ya Pemba ili Watanzania tuendelee kuwa na amani na tuendelee kuamini kwamba tuko salama. Lakini kama hatutakuwa na Kituo cha Uhamiaji katika Bandari ya Pemba, bado na wasiwasi kwamba usalama wetu uko hatarini kwa sababu vitu vinavyoingia katika Bandari ya Pemba hatuna uhakika navyo na wageni wanaoingia katika Kisiwa cha Pemba hatujui wamebeba nini na hatujui wanakuja kwa lengo gani. Naiomba Serikali kutazama hilo jambo kwa haraka na kituo cha Pemba kiweze kupata Kituo cha Uhamiaji na wageni wanaoingia wafuate taratibu za kuingia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuongelea ni suala la msongamano wa mahabusu katika Magereza yetu. Tukumbuke kwamba mwaka uliopita Mheshimiwa Rais alitembelea baadhi ya Magereza katika Mkoa wa Dar es Salaam, akakuta mahabusu na wafungwa wako nusu kwa nusu na hii ionyesha kwamba aidha, uwajibikaji kwa Polisi wanaoendesha kesi Mahakamani siyo nzuri au sijui niseme ni kitu

gani. Lakini Mheshimiwa Rais alisema na wananchi tulisikia kile ambacho kilizungumzwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kamati ya Ulinzi na Usalama bado wamekuta kuna msongamano katika Magereza yetu. Tukumbuke kwamba hao mahabusu wanalishwa kwa fedha za Serikali na wanahudumiwa kwa fedha za Serikali. Inawezekana kabisa kwamba baadhi ya mahabusu matumizi wanayotumia wakiwa Magerezani ni fedha nyingi kuliko hata faini wanazotozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali iangalie upya namna ya kushughulikia wahalifu au aidha walegeze masharti ya dhamana au iangalie utaratibu mwingine mbadala ambao unaweza ukatumika kwa mahabusu hao tusiwaweke wengi na wakatumia fedha nyingi za Serikali. Fedha ambazo zingetumika katika masuala mengine ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni la muda mrefu na mimi nilidhani kwamba baada ya Mheshimiwa Rais kutembelea Magereza yetu, suala hili lingeshughulikiwa mapema. Lakini kama kweli bado kuna msongamano kama Kamati ya Ulinzi na Usalama ilivyosema, naiomba Serikali sasa iangalie utaratibu mwingine ambao utawaondoa hao mahabusu haraka ili wanaofungwa wafungwe na wanaoachiliwa waachiliwe. Lakini ni mzigo mkubwa sana kwa Serikali kuwalisha watu ambao hata wakilipa faini na hata wakifungwa miezi mitatu, fedha watakazolishwa kwa kufungwa miezi mitatu na walizokaa kama mahabusu ni nyingi kuliko hata adhabu wanayopata kutokana na kesi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limenishtua kidogo ni suala la ulinzi katika mipaka yetu. Ripoti ya Kamati inasema kwamba walipotembelea Kituo cha Tarime walikuta katika Kituo hicho kuna Polisi nane tu. Lakini kwa upande wa nchi jirani kuna Polisi 200. Kwanza, niwashukuru hao Polisi kwa kazi kubwa wanayoifanya. Watu nane kuwa katika Kituo cha mpakani, wakati upande wa pili kuna Polisi 200, ina maana wanafanya kazi ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi ni kitu gani kinachoendelea. Inawezekana amani tuliyonayo au usalama tulionao umetusahaulisha tukadhani kwamba wahalifu ni wachache au tuna usalama kiasi kwamba tunaweza tukalala milango wazi. Kwa sababu kuwa na Polisi nane mpakani ni sawa na kulala mlango wazi. Sielewi! Upande wa Kenya kuna matatizo mengi ndiyo maana wana Polisi 200 katika Kituo kimoja au wanajua wajibu wa Polisi katika Vituo vya mpakani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi ni kutokana na kuwa na Polisi wachache katika nchi yetu, kwa hiyo, inaonekana kwamba hata kama Maaskari watakuwa wachache katika maeneo ya mipaka yetu hakuna tatizo lolote!!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nadhani kuna haja ya kuwa na Maaskari wa kutosha katika maeneo ya mipaka yetu. Kwa sababu hii ndiyo maana katika maeneo ya Kigoma wakimbizi wanapita tu, inawezekana hata huko Kigoma Askari Polisi wako wachache na ulinzi na usalama katika mipaka yetu hiyo inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie suala hili kwa ukaribu zaidi na kuongeza Maaskari katika maeneo ya mipaka yetu na ukizingatia kwamba hata huko mipakani sijui kama wana nyumba kwa sababu nyumba kwa Maaskari pia ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ingeangalia kwa ukaribu zaidi suala hili la kuongeza Maaskari katika maeneo ya mipaka yetu na inawezekana ikasaidia sana katika kudhibiti uingiaji wa wageni au wakimbizi katika nchi yetu. Tumeona katika miaka ya hivi karibuni kwamba kuna wakimbizi waliokamata pale Kibaha sikumbuki vizuri. Wasomali walikamatwa na wale waliingia inawezekana kutokana na uchache wa Maaskari katika mipaka yetu. Serikali ilitazama hili suala na kuongeza Askari Polisi wanaolinda usalama katika mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la *SUMA JKT*. Mradi wa *SUMA JKT* wa kutengeneza dawa za kutibu binadamu. Ripoti ya Kamati inasema kwamba *process* ni ndefu au kupata kibali cha kusajili utengenezaji wa dawa kwa *TANZASINO* ni kazi kubwa. Lakini tukumbuke kwamba nchi yetu inaagiza madawa.

Mimi nafikiri watu hawa watafutiwe namna ya kupata kibali cha kutengeneza dawa na itusaidie kupunguza uagizaji wa dawa nje ya nchi. Tukizingatia kwamba *SUMA JKT* ni ya Umma. Sasa tunapowasaidia wenye uwezo wa kuanzisha viwanda mbalimbali nchini tunainua uchumi wa nchi yetu. Naiomba Serikali iwasaidie *TANZASINO* kupata kibali cha kutengeneza dawa nchini na kuziuza. Wenzetu Ulaya walishawapa tuzo kama ripoti inavyosema kwamba walipata tuzo kule Marekani kama sikosei. Lakini nchini kwetu hapa walipo sisi hatujawatambua. Naomba tuwatambue hawa kwa kuwapa kibali na kuwapa uwezo wa kuendelea na utengenezaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache. Nakushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Ripoti ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu kuchangia Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya ndani ya Mikoa yetu hapa nchini. Niwapongeze kuhusu maoni yao yote waliyoyatoa ambayo yanaendana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitazungumzia ukurasa wa nane wa Ripoti ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ambayo kama kweli mambo haya yanafanyika, naweza kusema kwamba nchi inawekwa mahali pabaya na Askari wale ambao siyo waadilifu. Hivi sasa nchi yoyote kwenye usalama lazima iendane na wakati na lazima iende sambamba na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama bado kuna Askari wa Jeshi la Polisi wanawababambikizia kesi wananchi, hili litakuwa sio jambo nzuri, kwa sababu wananchi hao wataondoa imani na Jeshi letu la Polisi na kila tukisimama hapa Bungeni tunawaomba wananchi waende sambamba na walinzi wetu wote ili nchi yetu iwe katika hali ya amani na utulivu. Kutokana na Jeshi letu la Polisi lilivyo, hatuendi na wakati na

hatuendi kama wenzetu wanavyokwenda kwamba Askari mmoja awe anawalinda raia kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwetu sisi utakuta Askari mmoja anawalinda raia chungu nzima. Kwa hiyo, unaweza kusema raia ni wengi sana kuliko Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, Jeshi la Polisi lazima liweke upendo kwa wananchi wetu ili wawe na imani na Jeshi hilo. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwachukulie hatua Askari kama hao wakati wakigundulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili, Kamati imefanya kazi nzuri sana kwa kusema kwamba Zimamoto wawekewe Sheria ili kama bado ningeomba tu liwepo ili ndugu zetu hao wakifanya kazi wajue wanajikita vipi katika kazi zao hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu magari ya doria. Naliomba Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuondokane na wakati wa kusema kwamba Tanzania ni nchi ya amani na utulivu kila wakati. Isipokuwa hivi sasa tukae kwamba Tanzania ni nchi ya amani na utulivu, lakini Tanzania iweke ulinzi kila wakati.

Katika Kanuni za Polisi, Jeshi la Polisi linasema kwamba doria peke yake ni ulinzi kwa sababu yule mhalifu akiwa anakuona kila wakati unafanya doria anakuwa na wasiwasi. Kwa hiyo, kama tutakuwa na gari za doria au gari kwa kila sehemu ya Vituo vya Polisi, kazi ya doria itakwenda vizuri. Kwa hiyo, naipongeza sana Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kulileta hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, doria ndiyo inayofanya hata wale wahalifu wakifanya uhalifu wao na wananchi wakipeleka taarifa haraka, wale Askari walioko Vituoni moja kwa moja wanatoa amri kwa zile gari zilizokuwa nje zinafanya doria kwamba sasa ondoka Malindi nenda Pangawe mara moja kashughulikie jambo fulani. Sasa utakuta kwamba dakika chache tu Maaskari wameshafika kwenye sehemu ya tukio na wanakabili tatizo hilo. Kwa hiyo, kwa hili naipongeza Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kuliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mwenzangu hapa kanifilisi na kanuni za Bunge zinasema usirudie yale ambayo yamesemwa na mwenzako isipokuwa nazidi kulitilia mkazo tu kwamba Pemba ni Kisiwa kikubwa na hivi sasa watu wengi wanapitia Pemba kuingia Zanzibar. Kwa hiyo, ningezidi kuipongeza Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kuliona hilo kwamba kwenye Bandari hiyo kuweko na Ofisi ya Uhamiaji kama kawaida ya Bandari zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa muda mfupi tu wa kipindi cha mwaka mmoja na mwezi mmoja hivi kwa kuweza kuzuia kasi kubwa ya ujambazi ambayo ilikuwa tishio kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini vilevile nilipongeze Jeshi la Polisi na Majeshi yote hapa nchini kwa kuweza kukabili hali hiyo. Nawapongeza wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa taarifa nyingi kuhusu hali ya ujambazi na uhalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu wanasema kwamba mcheza kwao hutunzwa. Kwa hiyo, ningeiomba Wizara iwatazame vizuri sana Maaskari hao wa Jeshi la Polisi na

vilevile kuwaondoa zile kero zinazowafanya Jeshi letu la Polisi kurudi nyuma kiutendaji.

Ningeomba Wizara hii kama wanavyofanya Wizara nyingine wakishaona tu hili haliendi sambamba na wakati na wakishaona tu kwamba hilo linawabana wafanyakazi wao, huwa wanalileta hapa ili lirekebishwe. Lakini Wizara hii naona ina kigugumiza sana kwa Jeshi letu la Polisi kuleta yale ambayo yanawabana na hasa *PGO* bado wanakwenda na *PGO* ile ile ya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninastaajabu sana kuona kwamba Jeshi hili la Polisi bado lina Mikataba isiyopungua minne. Naweza kusema kwamba haliendi na wakati. Kuna Mkataba wa miaka mitatu, mtu ajaze fomu, ajiulize kwamba niendelee, ile sio mbaya, kuna Mkataba wa miaka 12 ajiulize: Je, niendelee au nisiendelee? Ile sio mbaya, unaweza kusema nisiendelee unatoka pale pale. Lakini ule Mkataba ambao umefunga wengi hivi sasa kwamba awe *pensionable* au awe wa mpito, sasa Askari wengi sasa hivi wameshabaini na Askari wengi wanalalamika.

Kwa hiyo, kama inavyokuwa kwa Wizara nyingine zinaleta hoja zao za kuwapa afueni wafanyakazi wao, basi na Jeshi la Polisi walete tupitishe kwamba ikiwa miaka 12 mwananchi yeyote ambaye yumo kwenye Jeshi la Polisi pale atazame: Je, nitoke au niendelee na Jeshi la Polisi niwe *pensionabl*e moja kwa moja? Awe *pensionable* kuliko Askari anayekaa miaka 30 halafu anakuwa sio *pensionable,* analipwa Sh.800,000/=. Ile imepitwa na wakati na wanastaafu na masikitiko. Lakini vijana wetu wakishafika miaka 12 waulizwe, unaendelea? Akisema anaendelea, moja kwa moja awe *pensionable,* ile itakuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afande *Inspector General* tunakuomba ikifika miaka 12 Askari atoke moja kwa moja awe *pensionable* kwa sababu anahangaika. Lakini baadaye anashindwa na sisi Waheshimiwa Wabunge wanatupa matatizo sana kutupa malalamiko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naishukuru Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa maoni yake na ninaishukuru Kamati kwa jinsi inavyofanya kazi saa zote. Nawaona mimi na mwaka 2000 hadi 2005 nilikuwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama. Naipongeza sana Kamati kwa hoja zake na maelekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono maoni ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu na mimi niweze kuchangia Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ningependa na mimi nitoe mkono wa rambimbi kwa ndugu na familia ya ndugu yetu Marehemu Juma Akukweti ambaye aliaga dunia. Bwana alitoa na Bwana ametwaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niwapongeze Mawaziri na Manaibu Waziri wote walioteuliwa. Nafikiri naweza nikaishia hapo kwa sababu ya kuokoa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, ninataka nichangie katika vipengele mbalimbali. Lakini nitaanza na kipengele cha ujambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Ulinzi na Usalama taarifa yake ni nzuri sana na mimi kwa kweli imenifurahisha kwa sababu inaridhisha. Kama Serikali itakwenda kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii tunaamini mabadiliko mbalimbali yataendelea kwa ajili ya kuleta ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujambazi umekuwa ni tatizo ambalo limekuwa sugu sana hasa wakati wa Awamu ya Nne ilipoingia madarakani. Lakini tunashukuru kwa juhudi za Serikali zilizofanywa. Ninachosema katika maeneo mbalimbali na katika Wilaya ya Bukombe, mwenzangu wa Wilaya ya Kibondo ameeleza matatizo yanayosababisha ujambazi huo ni kwa ajili ya wimbi kubwa la wakimbizi. Tunaiomba Serikali iendelee kulidhibiti kama walivyokwishachangia wenzangu kwa sababu hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Wilaya ya Bukombe, ambacho ninataka kusema ni tatizo hili pia linaweza hata likachangiwa na upungufu wa Maaskari katika eneo hilo, kwa sababu Wilaya yetu ya Bukombe kumekuwa na matukio ya ujambazi ya mara kwa mara. Lakini namshukuru *IGP* amewahi kutuma hata Tume ikaenda kule wakati inaendelea na ziara yake ambacho mimi labda niseme ninashukuru kwa sababu na Tume hiyo wakati ikiwa katika ziara yake ujambazi uliendelea kufanyika na yenyewe ikiwepo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tunaiomba Serikali ilitilie maanani ni tatizo la Bukombe na hasa kwa kuongeza pengine Maaskari, lakini pia wapewe vitendea kazi. Wilaya ya Bukombe ni Wilaya ambayo ni kubwa sana na imezungukwa na misitu. Tunahitaji tupate hata gari, Idara ya Upelelezi imekuwa ikihangaika sana. Tunaiomba Serikali ifikirie tatizo hili. Nashukuru hata Naibu Waziri tumeishawasiliana naye na yeye amesema atalifanyia kazi. Kwa hiyo, nazidi kusisitiza na kukazia kwamba Serikali ilichukua kwa umuhimu wake ili ipeleke gari la upelelezi katika Wilaya hiyo. Pengine Maaskari wetu tusifikie hatua tukaanza kuwalaumu kumbe vitendea kazi hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Desemba mwaka 2006, kuna ujambazi ambao ulitokea pale Bukombe katikati ya operesheni na ujambazi wa kulipua ulifanyika pale. *SACCOS* ambacho ni chombo cha wananchi wanyonge wameunganisha nguvu wakaweka fedha yao ilikuja kulipuliwa pale. Taarifa ambazo tumezipata kutoka Benki ambayo ndiyo wanayoifadhili *SACCOS* hiyo wanasema huenda ikawa ndiyo *SACCOS* ya kwanza kwa ufanisi katika nchi hii. Lakini *SACCOS* hiyo ilibomolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo ninaliona na ambalo nimetamani na nikashawishika niliongea hapa ni kuiomba Serikali pia iangalie utaratibu wa kuweka walinzi katika *SACCOS* zinazoanzishwa hasa tunazoziona kwamba zinafanya kazi kubwa ya huduma za kibenki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bukombe hatuna Benki, Ushirombo, *SACCOS* ndiyo tunatumia kama Benki pale na Benki hii bahati nzuri tulikuwa tumeshawasiliana na

Waziri Mkuu kwamba angekuja kuzindua muda sio mrefu, lakini ndipo hapo mwezi Desemba mwaka 2006 ikalipuliwa, *safe* ikapigwa ikasambaratika. Sasa wanaolinda pale ni vijana tu wana magobole wakati ambapo Jeshi la Polisi lingeweza kuteua watu wake wakaenda kulinda katika Benki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili nimeona niliseme na kusisitiza kwamba Serikali iliangalie upya ili *SACCOS* angalau katika kila Wilaya panapokuwepo na *SACCOS* moja inafanya kazi kama Benki kwenye eneo hilo watume walinzi kuliko kusubiri kutuma *NMB* na *CRDB* na Benki nyingine za kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala hili la ujambazi naomba niongelee suala la sungu sungu. Serikali tunaiomba iwekwe sheria ambazo zitaweza kuisaidia sungusungu kuipa nguvu ili ziweze kusaidana na Askari Polisi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kweli ni nzuri na inaridhisha na imeongelea suala la msongamano wa mahabusu. Suala la msongamano nakumbuka tarehe 2 Oktoba, 2006 mimi na Mkuu wa Wilaya tulitembelea Gereza la Kahama ambapo ndiko mahabusu wa Bukombe wanawekwa pale. Tulikuta mahabusu zaidi 200 wako pale na tulipoongea nao wengi wanalalamika wanasema wana kesi za kubambikizwa.

Kuhusu hili ninaiomba Serikali kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na mimi ninatoa pendekezo hapa Serikali ifanyiwe kazi haraka suala hili. Kwa sababu wananchi wengi kwa mfano, Gereza la Kahama ambalo *Capacity* yake ni kama wafungwa 70, lakini tayari mahabusu wa Wilaya ya Bukombe walikuwepo zaidi ya 200. Sasa sijui kama tunaokoa au tunaendelea kuangamiza fedha ya Serikali. Tunaiomba Serikali ilifanyie kazi hili na ikiwezekana watu ambao wataonekana hawana hatia waondolewe au kama wanapigwa faini wapigwe faini waondoke katika maeneo hayo. Unakuta watu wamekaa pale kwa muda mrefu zaidi ya mwaka mmoja na upelelezi haukamiliki.

Kwa utaratibu huu, tutakuwa tunadhoofisha wananchi wetu, lakini pia katika maisha bora kwa kila Mtanzania tunaweza tukashindwa kuyafikia hususan tunapokuta mwananchi ambaye amekwenda kufungwa pengine amebambikizwa kesi na huku familia yake inaendelea kuhangaika kila siku njiani kwenda umbali wa kilomita 100 kushughulikia kesi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninapenda kuipongeza sana tena Serikali na Kamati kwa ajili ya taarifa yake nzuri na ninaomba Serikali iendelee kuifanyia kazi. Naamini kwamba kama Serikali itayatekeleza yote yaliyoandikwa katika ripoti ya Kamati. Sikupenda kuyasema ukurasa kwa ukurasa kwa sababu yameeleweka kwa kila mmoja. Ninaamini tutafika mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na kwa kuokoa muda ninashukuru kwa taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Kama nilivyokuwa nimetoa maelekezo ya utaratibu, hoja hii ni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Lakini kwa kuwa

utekelezaji wa hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama mambo yake yanatekelezwa na Serikali. Sasa nitatoa nafasi kwa Serikali kupitia kwa *Chief Whip*, lakini kwa Manaibu Mawaziri ambao wako hapa ndani kama wana mchango wowote kuhusu hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Kwa hiyo, baadaye hoja hii tutaiamua tutakaporudi katika Kikao cha saa 11.00 jioni ndipo tuhamie kwenye hoja nyingine ya Kamati ya Maliasili na Mazingira. Sasa kwa dakika chache zilizobakia nitawomba wachangiaji wawili kwa maana ya Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed - Naibu Waziri wa Usalama wa Raia na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee - Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wao sasa wazungumze kwa niaba ya Serikali, wagawane huu muda mfupi uliobakia na saa 11.00 jioni tutamalizia na Mwenyekiti wa Kamati ili aweze kujibu na kuhitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed naomba uanze kwa muda mfupi na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee atafuatia.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii. Aidha, nimshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa namna ambavyo amewasilisha vizuri hoja yake na pia kwa uzito wa maelezo yake. Aidha, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa katika Wizara yetu na umekuwa dira nzuri sana ya utendaji kazi katika shughuli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimepata fursa hii kwa mara ya kwanza katika kikao hiki, ningependa na mimi niungane na waliotangulia kusema, kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu mpendwa, mwenzetu Mheshimiwa Juma Akukweti. Ningependa nitoe salamu zangu za rambirambi hizi kwako wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, wananchi wake wa Jimbo lake la Tunduru na wafiwa wote, Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya Marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, niwapongeze wale wote waliopata nyadhifa kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa nafasi mbalimbali za Uwaziri na Manaibu Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nifanye haraka haraka ili kwa kifupi sana niweze kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawashukuru wale wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia kwa kuanzia kumtambua Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kuwasilisha hoja hii. Aidha, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Suleiman Kumchanya, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Jenista Mhagama amechangia kwa maandishi, Mheshimiwa Juma Sereweji na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hao ndiyo ambao wamechangia kwenye hoja yetu hii. Ninataka niseme kwamba michango yao imekuwa mizuri sana na

imekuwa ni mwongozo katika utendaji wa kazi. Ningependa niwafahamishe tu kuwa yale ambayo yanahitaji kwenda kufanyiwa kazi, nasema kwamba tumeyachukua twende kuyafanyia kazi na yale ambayo nitatoa kwa ufupi maelezo nitajitahidi kufanya hivyo. Kwa jumla hali ya nchi yetu inaendelea kuwa shwari hata katika maeneo ya mipakani na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola vimechukua hatua kubwa sana ya kupambana na uhalifu katika maeneo hayo yakiwemo maeneo ya Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu litaendelea kuchukua hatua ya kupanga mikakati, operesheni maalum, misako na doria na kuhakiki silaha ili kuhakikisha kwamba silaha haramu nchini mwetu zinadhibitiwa ipasavyo kwa nia ile ile ya kuwalinda wananchi wetu na waendelee kukaa katika hali ya usalama na utulivu.

Kama nilivyokuwa nikijibu suala asubuhi ya leo kuhusiana na operesheni maalum inayoendelea huko mipakani, ningependa tu nitamke wazi kwamba katika operesheni hiyo kama nilivyosema, kuna mafanikio makubwa yamepatikana na ningependa niwapongeze sana vijana wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola kwa kazi nzuri wanayoifanya ili kuhakikisha kwamba hali ya usalama inakuwepo na watu wetu wanaendelea kukaa katika hali ya utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi moja kubwa ambayo sasa hivi Jeshi la Polisi inaifanya ni kufanya *job listing* kwa nia ya kuweza kuweka utaratibu mzuri wa kuweka ajira katika Jeshi la Polisi na nia yetu kubwa ni kuongeza idadi ya Askari wetu ili kuweza kumudu mazingira yote yale yanayojitokeza ya uhalifu nchini. Kwa hiyo, ningependa sana niishukuru Serikali kutukubalia kufanya kazi hiyo na ningewaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi muwe na subira kwa kuwa kazi hiyo katika hatua za mwisho ili tuweze kuongeza na kuimarisha Jeshi letu vizuri zaidi.

Aidha, hivi sasa tunafanya kazi ya kuimarisha Idara ya Upelelezi katika Jeshi la Polisi kwanza kwa kutoa mafunzo. Hivi karibuni tumemaliza kuwapa mafunzo Askari 300 wa upelelezi ili wawe na uwezo mkubwa zaidi katika kufanya shughuli zao za upelelezi. Aidha, tumo katika hatua za awali katika ujenzi wa Chuo cha Upelelezi hapa Dodoma kwa nia hiyo hiyo ya kuwaimarisha Askari wa Upelelezi ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi na kwa kitaalamu zaidi pamoja na kuwapa semina za mara kwa mara ili watekeleze wajibu wao ipasavyo. Nia yetu kubwa ni kuondoa misongamano kule Magerezani, wakati huo huo kuondoa kabisa malalamiko ya wananchi kwenye kubambikiziwa kesi kwa kujenga uwezo mzuri wa Askari wetu wa Upelelezi.

Aidha, tunaendelea kuchukua kila jitihada kuhakikisha kwamba tunaimarisha kujenga nyumba za Askari wetu ili Askari wawepo wanakaa katika Makambi na waweze kutoa huduma vizuri zaidi. Hivi sasa licha ya bajeti ya Serikali katika kuendeleza kujenga nyumba za Askari, lakini pia tunashirikiana na *NSSF* katika kuendeleza ujenzi wa nyumba za Polisi na kwa kuanzia, tuna nia ya kujenga maghorofa 60 nchi nzima. Kwa upande wa Dar es Salaam tunajenga maghorofa 50 na Zanzibar tunajenga maghorofa 10 ikiwemo na Pemba. Kwa msingi huo tunajitahidi kufanya kila jitihada kutokana na hali halisi ya uwezo wa nchi ili kuimarisha makazi ya Askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Jeshi la Polisi linafanya tathmini ya kina ya kuweza kujua idadi halisi inayohitajika Vituo vya Polisi nchini kwa kufuata vigezo vya Polisi na mara nyingi nakuwa nikijibu suala hili ili kuwahakikishia kwamba nia yetu ni

kuongeza Vituo vya Polisi pale ambapo pana uhitaji wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, ningewaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi waendelee kuvuta subira wakati kazi hiyo inafanyika mara zoezi hili litakapomalizika tuweze kuendelea na kazi ya ujenzi wa Vituo vya Polisi katika yale maeneo yanayohitajika hasa yawe na Vituo vya Polisi.

Aidha, tunaendelea kuhakikisha kwamba Askari wetu tunawajenga kinidhamu na tumeunda Kamati ya Nidhamu pale Wizarani ili kuwachunguza Askari wale ambao wanafanya makosa na hatua za kisheria zichukuliwe. Napenda tu kutoa taarifa kwamba Askari mbalimbali wameshachukuliwa hatua mbalimbali zikiwemo kufukuzwa kazi kwa wale ambao wanawabughudhi au kuwasumbua wananchi na waliokuwa hawatekelezi wajibu wao vizuri. Naomba tu Waheshimiwa Wabunge muendelee kutuvumilia wakati tukifanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na magari ya doria. Hivi karibuni tunatarajia kupata magari 40 na pikipiki 177 kutoka nchi ya Dubai. Huu ni msaada kutoka mtawala wa Dubai na napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana mtawala huyo kwa imani yake hiyo. Aidha, tumetenga fungu katika bajeti ya Serikali kwa ajili ya kununua magari mengine mapya ili yasaidie Askari wa Upelelezi na doria. Kwa hiyo, ningewaomba Waheshimiwa Wabunge muendelee kushirikiana na sisi kutuunga mkono katika jitihada hizo, nakuhakikishieni kwamba tutajitahidi kupeleka pale ambapo pana upungufu mkubwa ili kuweza kuziba pengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la *PGO,* napenda nimhakikishie Mheshimiwa Sereweji kwamba *PGO* imefanyiwa kazi na hivi sasa nataka niliarifu Bunge lako Tukufu na kwa sababu ninalo suala la Mheshimiwa Sereweji linalohusiana na *PGO,* lakini kwa sababu umefanya haraka kutaka kujua hii habari, ni kwamba kazi imekamilika na *PGO* mpya iko tayari na hivi sasa tunaitumia katika utendaji wetu wa kazi za Kijeshi. Kwa hiyo, taarifa rasmi hiyo kwamba *PGO* jipya lipo na lile halipitishwi hapa Bungeni, ni utaratibu wa kiaskari katika utekelezaji wa kazi zao.

Aidha, yako malalamiko sana yanajitokeza kuhusu suala la *pension* na *gratuity.* Hili ni suala la msingi sana. Tatizo hapa sio kufunga kusimamisha utaratibu wa *gratuity*, tatizo hapa ni kutoa elimu kwa Askari wetu wakaelewa lipi kwao lina maslahi. Kwa sababu ukiondoa *gratuity,* msingi wake ni kwamba unawanyima fursa wale Askari ambao wangependa kutumia utaratibu huu. La msingi, hili hulazimishwi, ni uchaguzi wa Askari mwenyewe. Kwa hiyo, kitu cha msingi ni kutoa elimu zaidi wakaelewa tofauti baina ya pensheni na *gratuity.* Hulazimishwi kuchagua *gratuity.* Tukiliondoa hili, maana yake wale ambao wana hamu ya kutumia utaratibu wa *gratuity* unawafungia. Kwa hiyo, hutoi nafasi nyingine kwa Askari, kitu ambacho huko mbele tutajutia. Ni jambo ambalo ni utaratibu mzuri katika Jeshi la Polisi kuwemo suala hilo na tumelizungumza sana ndani ya Jeshi na imeonekana umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuifunga *gratuity* maana yake wale ambao wangependa kutumia nafasi hiyo wasingepata fursa hiyo vizuri. Kwa hiyo, ningeomba Waheshimiwa Wabunge mtuelewe kwenye hili. Jambo la msingi ni kutoa elimu ya ziada na tumeshawaagiza Makamanda wa Polisi wa Mikoa kuhakikisha kwamba wanawapa Askari wetu elimu ya kutosha ili waelewe umuhimu wa kutofautisha baina ya pensheni na *gratuity*. Nina hakika na wao wenyewe watafurahia kubakia katika utaratibu huo.

Kuhusiana na Kituo cha Uhamiaji, bahati mbaya hapa ndani Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani simwoni, lakini ningependa kwa sababu mimi mwenyewe nyumbani kwetu ni Pemba, ni kwamba pale tatizo la Uhamiaji kwa kuwa hawana kituo, tatizo lililopo pale ni kwamba kwa wakati huu sasa hivi kwa upande wa Uhamiaji wanatumia majengo yale ya Bandari ya Mkoani na Wete kwa shughuli za Uhamiaji kule Pemba. Kwa hiyo, nafikiria Kamati ilipokuwa inazungumzia hili inazungumzia labda kwenye maeneo mengine ya ujenzi wa kituo kipya kama kule kufikiriwa kujenga Kituo cha Bandari katika sehemu za Micheweni hasa sehemu za Mkia wa N'gombe kule.

Lakini nafikiri kwa Bandari ya Mkoani na Wete, Askari wa Uhamiaji wako pale tatizo ni kutokuwa na jengo lao wenyewe. Lakini nina hakika lile jengo la Bandari linatosheleza kumudu kufanya kazi zao. Labda siku za usoni tutafikiria kujenga Kituo, sio vibaya, lakini kwa wakati huu naona huduma za Uhamiaji zinatolewa vizuri kwa kupitia Askari wa Uhamiaji walioko pale Bandarini Wete na Mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda hautoshi, tutaendelea kufikiria zaidi kuhusu suala la maslahi ya Askari wetu kwa maana ya kuwaboresha katika masuala ya mishahara, posho na mambo mengine muhimu ili Askari wetu waweze kufanya wajibu wao vizuri. Kwenye hili suala la ulinzi kwa vyombo vya fedha, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Luhahula kwamba suala hili tayari Serikali imeshalitolea ufumbuzi kwamba Mabenki na vyombo vingine vya fedha vilindwe na Askari wetu wa Polisi. Kwa hiyo, utaratibu huo utafanyika ili kuhakikisha usalama katika maeneo haya muhimu ya kulinda fedha za wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka nikushukuru sana kwa kunipa hizi dakika zilizosalia ili niweze kutoa maoni ya Serikali kuhusiana na michango ambayo imetolewa na wajumbe mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi ni mara yangu ya kwanza, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kiembesamaki, naomba nitoe salamu zetu za pole kwa familia ya Marehemu Akukweti. Vile vile, nataka nichukue fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wamepata wadhifa mbalimbali za Kimataifa na za Kitaifa.

Tatu, naomba vile vile nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na Wajumbe wake wote. Wakati wote tulipokuwa tunao walikuwa wakitupa faraja kubwa sana na tulikuwa tunafanya kazi nao vizuri kwa utiifu na kwa uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, napenda kumuahidi Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwamba Wizara yangu itaifanyia kazi ripoti hii na itayatekeleza yale yanayotuhusu kila wakati muafaka unapofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka nijielekeze katika hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge bila kupoteza muda. Hoja kubwa ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ile ya *JKT*. Kwanza nataka

tujikumbushe sababu gani zilizofanya nchi yetu kuanzisha *JKT*. Kwa kifupi tu zipo sababu kadhaa ambazo zilizopelekea nchi yetu kuanzisha Jeshi la Kujenga Taifa.

Kwanza ni kuwajenga vijana wetu ili wawe na hisia na ulinzi na usalama wa nchi yao, kwa maana kwamba vijana hawa wapatiwe mafunzo ya ulinzi na usalama ili wawe vijana bora, waaminifu na waadilifu pale linapotokea lolote lile linalohusiana na ulinzi na usalama.

Pili, kwa kuwa Serikali haiwezi ikawaajiri vijana wote hawa, ni dhahiri kwamba Jeshi hili limeanzishwa kwa kuwaelekeza vijana hawa katika suala zima la uzalishaji mali na kujitegemea na ndiyo kazi ambayo tunaendelea nayo hadi hivi sasa. Lakini kama hayo hayatoshi, suala la uzalendo na kuipenda jamii ndiyo hili ambalo linaongelewa kila baada ya muda. Vijana wetu wasijaribu kubadilisha maadili tunayowajenga ili wawe wazalendo na waipende jamii baada ya kumaliza mafunzo yao ya *JKT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ni suala zima la kufanya *JKT* kuwa ni jiko la kuwatengeneza hawa vijana pale inapotokea ajira iwe katika vyombo vya ulinzi na usalama hata katika vyombo vingine vya Serikali na vile visivyo vya Serikali. Lakini hili linategemeana na sifa za kila kijana ambaye anahitajika kuajiriwa katika ile Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi walielezea pamoja na ripoti ya Mwenyekiti azma yao na ushauri wao wa kurejesha utaratibu wa zamani vijana wa Kidato cha Sita pamoja na wale wa Vyuo kujiunga na *JKT*. Nataka niseme kwamba ile sheria haijafutwa, ile sheria ipo, tuliiweka pembeni tu kwa muda kutokana na hali yetu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikubaliane nao kwamba tunajipanga upya kwa maana ya majengo na wakufunzi. Tunajipanga upya kwa maana ya vifaa na zana ili tutakapokuwa tayari tutaelekeza nguvu zetu katika suala la kuwarejesha vijana katika mafunzo ya *JKT*. Kwa sasa kilichopo, wanaojiunga ni kwa hiari, lakini vile vile nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba uendeshaji wa *JKT* una gharama na nakuombeni sana itakapofika wakati wa bajeti muweze kutusaidia ili tuweze kufanikisha suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo lililozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni suala la upungufu wa magari hasa kwa Askari wetu walioko mipakani. Kama tunakumbuka vizuri, wakati wa bajeti Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliliarifu Bunge hili kwamba kupitia Wizara ya Ulinzi, Serikali imeshaagiza magari 628 ambayo baadhi yao yatatumika kuwapatia Wanajeshi wetu walioko mipakani ili waweze kuwa na usafiri wa uhakika waweze kufanya doria katika maeneo yetu wakishirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Hali hiyo nataka nieleze mbele yako vile vile kwamba imeungwa mkono na nchi marafiki na ndugu zetu Wachina wametusaidia magari 30 ambayo zimeshawasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Serikali ya China kwa msaada huo na nawaomba waendelee kushirikiana na Serikali ya Tanzania ili kuweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo lililozungumzwa na Wabunge ni suala la mafunzo kwa mgambo. Nataka niliarifu Bunge lako kwamba kila Mkoa Tanzania tuna Afisa wa Jeshi ambaye anashughulikia masuala ya Mgambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu ni kuwafunza wananchi Mgambo ili waweze kushirikiana na wananchi katika ulinzi wa Mikoa na ulinzi wa nchi yetu kwa ujumla.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwahamasisha vijana walioko ndani ya Mikoa yao, ndani ya Majimbo yao kujiunga na Jeshi la Mgambo ili waweze kupata mafunzo yaweze kutusaidia katika suala zima la ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kwamba suala la makazi vile vile limezungumzwa hasa katika suala la Wanajeshi wetu walioko katika maeneo ya mipakani. Wizara yangu imejipanga vizuri tu. Kama nilivyoeleza jana, wakati nilipokuwa najibu suala la Mheshimiwa Mohamed Said alilotaka kuelewa suala la makazi katika eneo la Makue, vile vile hali hii iko kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Mikoa, Majimbo tunajenga kupitia fedha zetu wenyewe za bajeti. Lakini vile vile tuna mkakati wa kushirikiana na vyombo vya ndani na nje vya fedha ambavyo vitaweza kutusaidia kujenga nyumba za Wanajeshi kwa njia ya mkopo wa muda mrefu.

Naomba sana Waheshimiwa Wabunge wavute subira na muda utakapofika wataweza kuona. Wale Wabunge wa Dar es Salaam na Wabunge wa Arusha nadhani sasa hivi wameanza kuona, *NSSF* ameshaanza kushirikiana na sisi katika kujenga nyumba pale Arusha na Dar es Salaam, nyumba 270 tayari zimeshaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami namalizia kwa kuunga mkono taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti, nasema tutaendelea kushirikiana naye. Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

Kanuni ya 55, lakini nataka kuzungumzia kanuni ya 50 (8)(d), kujiingiza katika mambo ya kuwasema wenzake au kuleta malumbano ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Mbunge Felister Aloyce Bura alipokuwa akichangia taarifa ya Kamati hii katika kipengele cha kwamba kule Pemba kutokana na kwamba hakuna Kituo cha Uhamiaji yumkini wale watu waliokimbia wakati wa vurugu inawezekana sio watu wa kule. Naomba usemi huo ufutwe, wale ni Wapemba. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kwa kutumia kifungu Na.54 cha Spika kuweza kuzungumza katika Bunge, Mheshimiwa Mbunge wakati Mheshimiwa Felister Bura alipokuwa anazungumza hapo ulitakiwa uombe mwongozo wa Spika na kumwomba Mheshimiwa Bura aweze kutoa maelezo yake inavyotakikana.

Kwa hali hiyo, kama unaona tatizo la Mheshimiwa Felister Bura katika maelezo yake halijakuridhisha basi nitaliomba ulilete kwa utaratibu unaotakiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge shughuli za asubuhi kulingana na muda wetu zimekwisha na kwa kuwa hoja hii bado hatujahitimisha kwa kuiamua mbele ya Bunge na kwa kuwa tumebakiwa na Msemaji mmoja, Mwenyekiti wa Kamati wa Ulinzi na Usalama kuweza kujibu michango ya Wabunge mbalimbali ambayo imetolewa, leo saa 11.00 jioni tutakaporudi tutaanza na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati baada ya hapo tutaamua hoja yetu na tutamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira aweze kuendelea na hoja nyingine ambayo imepangwa katika ratiba ya leo.

Baada ya kusema maneno hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.50 mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa. 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. JESNISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnakumbuka tulishamaliza majadiliano ya jumla na tulishapata maelekezo kutoka Serikalini. Sasa nitamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ili aweze kumaliza hoja yake. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama karibu.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kufanya majumuisho katika Taarifa yangu niliyoiwasilisha asubuhi katika Bunge lako Tukufu. Kabla ya kufanya hivyo naomba kwa heshima niitambue michango ya Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Taarifa yetu ya mwaka 2006/2007. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge saba walichangia ndani ya Bunge lako Tukufu na Wabunge watano walichangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue kwa kuwataja kwa majina waliochangia ndani ya Bunge lako Tukufu ni Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Mohamed Omar Mohamed na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa Rosemary Kirigini. Kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia taarifa hii naomba kwa niaba ya Kamati ya Ulinzi na Usalama niwashukuru kwa dhati kabisa kwa michango yenu mizuri kwa sababu wote waliochangia kwa kusimama hapa ndani ya Bunge hili Tukufu au kwa maandishi wote waliipongeza na kuunga mkono taarifa yetu. Kwa hiyo, kwa niaba ya wenzangu ninawahakikishieni kwamba michango yenu imetutia moyo sana na yametufariji sana na tunaahidi kwamba tutaendelea kutekeleza majukumu ambayo mmetukabidhi tuyafanye kwa niaba yenu, kwa nguvu mpya, kasi mpya na ari mpya baada ya michango yenu hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua umenipa muda mfupi sana uliniambia dakika 15 tu, kwa hiyo, napenda tu niende haraka haraka, kwanza niwashukuru sana Naibu Waziri wa Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Naibu Waziri Usalama wa Raia kwa michango yao katika taarifa yetu hii. Kwa sababu michango yao kwa kweli ilijibu hoja zote ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia taarifa yetu, walijibu karibu hoja zote zilizojitokeza na kwa misingi hiyo wamefanya kazi yangu hii kuwa rahisi sana na baada ya michango ya Serikali ambayo ilitolewa asubuhi hii mimi nataka niseme tu haya ya ujumla, sitapitia michango ambayo ilitolewa na Wabunge mbalimbali kwa sababu kama nilivyosema hoja zao mbalimbali zilijibiwa na Waheshimiwa Mawaziri na kuna mengine ambayo nimechukua mimi nitaendelea kujadiliana nao ili tuyafanyie kazi. Mheshimiwa Rosemary Kirigini aliwasilisha suala ambalo ni nyeti kidogo nataka nimhakikishie tu kwamba nimelichukua na nitalifanyia kazi kwa kushirikiana na Serikali.

Sasa la jumla ambalo nataka kusema ni kwamba Waheshimiwa Wabunge katika kutekeleza majukumu ambayo tumekabidhiwa na Bunge hili Tukufu tumegundua au tumeona kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge waliochangia hapa wamesema kwamba vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vinakabiliwa na matatizo mengi, Jeshi la Wananchi, Polisi, Uhamiaji vinakabiliwa na matatizo mengi kutokana na hali halisi ya uchumi wa Taifa hili. Kwa hiyo, kwanza kuna upungufu wa wafanyakazi katika maeneo mbalimbali, kuna upungufu wa vitendea kazi, kuna tatizo la makazi, yote haya yanavikabili karibu vyombo vyetu vyote na kama walivyoeleza Mawaziri walipokuwa wanajibu hoja mbalimbali za Wabunge, kuna jitihada kubwa na za dhati kabisa ambazo Serikali inazifanya katika kukabiliana na matatizo haya mbalimbali na sisi kama Kamati tunaridhika sana na juhudi na hatua mbalimbali ambayo Serikali inachukua kukabiliana na matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka tu kusema sisi kama Kamati tumekuwa tukiiambia Serikali na tutaendelea kuiambia Serikali na kuihimiza kwamba hakuna gharama kubwa zaidi ya gharama ya kulinda raia, mali zao na usalama wa nchi kwa ujumla. Kwa sababu thamani ya raia na mali zao ni kitu ambacho hakipimiki, kwa hiyo, nasema kwamba pamoja na matatizo mbalimbali tuliyonayo ya kiuchumi, basi kwa sababu kupanga ni kuchagua basi tunapopanga mipango yetu mbalimbali suala la ulinzi na usalama wananchi wetu na kwa nchi yetu, lazima liendelee kupewa umuhimu ambao linastahili kwa hiyo katika kugawana hicho kidogo, hiyo keki ndogo basi matatizo yanayovikabili vyombo vyetu mbalimbali vya ulinzi na usalama yatafakariwe na kupewa umuhimu ambao unastahili.

Mheshimiwa Felix Kijiko alizungumzia suala la uchache wa askari polisi na JWTZ katika mkoa wa Kigoma na Kagera na kutokana na matatizo makubwa sana ambayo yanaikabili mikoa hiyo, matatizo ambayo yametokana na tatizo la wakimbizi, mimi nakubaliana naye kabisa Mheshimiwa Felix Kijiko kwamba hiyo hali hata sisi tuliiona, Kamati iliiona. Lakini kama nilivyosema ni hali ambayo ipo *across the board* ni katika maeneo yote, lakini ninachotaka kusema tu ni kwamba suala la ulinzi na usalama wa wananchi ni wadau wakubwa na ndio wadau namba moja na ningependa niwapongeze sana wananchi wa mkoa wa Kigoma na wananchi wa Mkoa wa Kagera kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya katika kupambana na uhalifu ambao ulikuwa umekithiri katika mikoa hiyo miwili, uharifu ambao umetokana na uwepo kwa wakimbizi katika mikoa hiyo. Kutokana na ushirikiano mzuri sana ambao vyombo vya ulinzi,

vyombo vya dola vimepata kutoka kwa wananchi imewezekana kukusanya silaha nyingi sana zilizokuwa katika mikono ya uhalifu na kuziharibu. Juzi juzi hapa polisi wameteketeza silaha zaidi ya 2,700 ambazo zimepatikana kutokana na ushirikiano mkubwa ambao wananchi wamewapa polisi na vyombo vingine vya dola katika kuzisaka na kuzikusanya silaha hizo.

Kwa hiyo, wakati tunaendelea kuihimiza Serikali na sisi tutaendelea kufanya hivyo kwamba suala la upungufu wa askari katika majeshi yetu ya polisi, JWTZ liendelee kupewa umuhimu na tuendelee kwa ajili ya askari zaidi ili kukidhi matakwa yaliyopo, basi tunaomba vile vile nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi kama wadau wakubwa katika suala hili la ulinzi na usalama tuendelee kuvipa vyombo vyetu vya dola ushirikiano ambao unatakiwa ili tukabiriane na uhalifu na tuendelee kuilinda amani ya nchi yetu, tuendelee kuishi katika amani na kwa kweli Kigoma wameonyesha mfano, ulikuwa ni mfano wa kuigwa na natoa wito kwamba na mikoa mingine vilevile wafanye hivyo ili tuweze kukabiliana na uharifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile nitumie muda huu mfupi ambao umenipa nizungumzie suala la kituo cha uhamiaji katika Kisiwa cha Pemba. Tunapozungumzia kituo cha uhamiaji tunamaanisha kujengwa ofisi na vile vile tunamaanisha vilevile kwamba kutakuwa na wafanyakazi wataalam na wafanyakazi wengine kwa ajili hiyo. Sasa Pemba, Pemba ni kweli kuna watumishi wa Idara ya Uhamiaji, lakini watumishi hao hawana ofisi hawana majengo ndio hivyo wamejibanza banza tu maeneo mengine, na *concern* ya Kamati hapa ilikuwa ni hiyo kwamba Idara ya Uhamiaji katika Kisiwa hasa kule Kaskazini, nafikiri bandari ya Kaskazini hawana ofisi kabisa na kwa misingi hiyo tuliona hiyo ni tatizo ambalo ni lazima lifanyiwe kazi, wapo watumishi wachache lakini hawana makazi basi wanajibanza banza kwenye ofisi za polisi na ofisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoelezea katika taarifa yangu kwa bahati nzuri sana, Kamati iliona ushirikiano mkubwa sana baina ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama Visiwani Zanzibar na Pemba, kuna ushirikiano mzuri sana kati ya polisi, uhamiaji hata Jeshi la Wananchi na kwa hiyo, kutokana na ushirikiano huo mkubwa walionao, basi wanasaidia matatizo yao, lakini kwa hali ambayo hata Waheshimiwa Wabunge wameielezea hapa katika hali ya dunia hivi sasa na matatizo ya ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali na ukitazama Jiografia ya Kisiwa cha Pemba ni sehemu ambayo inaweza kuwa ni muafaka sana kwa kutumiwa kwa makusudi mbalimbali. Kwa hiyo, kiulinzi hata na kiusalama ni sehemu ambayo hatuwezi kupuuza katika taratibu mbalimbali za ulinzi na usalama. Kwa hiyo, ni moja ya eneo ambalo ni lazima tuwe macho nalo na tusilipuuze ni hili eneo la uhamiaji tuhakikishe kwamba Pemba kuna watumishi wa kutosha na wana ofisi, ili tuweze kudhibiti, kuingia na kutoka kwa wageni. Kwa sababu kuingia na kutoka kwa wageni ndiko kunaweza kukaingiza na kutoa matatizo mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza imelia, lakini kama nilivyosema Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Wizara zinazohusika walifanya kazi nzuri sana walipochangia taarifa yetu hii walijibu hoja zote zilizojitokeza kutoka kwa Wabunge mbalimbali na kwa hiyo, mimi niliposimama hapa nilikusudia tu kwanza kabisa niwapongeze Waheshimiwa Wabunge na niwashukuru kwa kuiunga mkono taarifa yetu na kueleza tu hayo ya ujumla ambayo nimewaeleza hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kusema hayo basi naomba nitoe hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2006 ilipitishwa na Bunge)*

**Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika Taarifa**

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa kipindi cha mwaka 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni Namba 101(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira katika kipindi cha mwaka 2006 ilitekeleza kazi zake kwa kuzingatia majukumu iliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu hayo ni pamoja na haya yafuatayo, kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo hushughulikia Mazingira, kusimamia shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo hushughulikia sekta za uvuvi, maliasili, utalii na mambo ya kale, kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii, ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa hii nitajielekeza katika maeneo yafuatayo, kwanza, kazi zilizotekelezwa na Kamati, pili ziara zilizofanywa na Kamati na mwisho ni maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kazi zilizotekelezwa na Kamati kwanza Kamati ilishiriki katika mikutano mbalimbali ambapo Kamati ilipata nafasi ya kufanya mikutano katika nyakati tofauti kwa lengo la kuongeza upeo wa Wajumbe wa Kamati katika maeneo yanayohusu sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Mikutano iliyofanyika ni pamoja na Mkutano na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, pamoja na wataalam kutoka Ofisi yake.

Katika mikutano hiyo Kamati ilijadili kuhusu mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji, pia wajumbe wa Kamati walielezwa muundo na majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iliainisha maeneo nyeti ambayo yanapewa kipaumbele kuhakikisha Mazingira yanayotunzwa ipasavyo, maeneo hayo ni pamoja na mazingira ya vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na

mito, bahari na maziwa. Pia mazingira ya maliasili ya Ukanda wa Pwani, mazingira katika maeneo ya uchimbaji madini, mazingira ya kambi za wakimbizi, masuala yanayohusu kuenea kwa ukame na hali ya jangwa, lakini pia mazingira ya mijini kutokana na utupaji wa taka ovyo na uchafuzi wa hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ilifanya mikutano na Mheshimiwa Antony Diallo, aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, pia na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii wa sasa kuhusiana na shughuli zinazofanywa na Wizara pamoja na maelezo ya sera ya wanyamapori, sera ya uvuvi na sera ya utalii. Katika mikutano hiyo Kamati ilishauriana na Serikali kutayarisha sera ya mambo ya kale, pia kufanya mapitio upya ya sheria za maliasili ambazo zimepitwa na wakati ili ziwe endelevu katika kusimamia maliasili zilizopo.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hata leo tulikuwa na Mkutano na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kuhusiana mambo mbalimbali ya ushauri wa Kamati kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya mikutano ya kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Mashirika ya Umma pamoja na Taarifa za Ukaguzi wa Hesabu za mwaka 2004/2005, mashirika yaliyohusika ni Shirika la Makumbusho ya Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Bahari, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania pamoja na Baraza la Taifa la Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ilifanya mkutano wa kupokea na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka 2005/2006 na Makisio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2006/2007. Baada ya Kamati kukamilisha kazi hiyo ilitoa maoni na ushauri na kuwasilishwa Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine iliyofanywa na Kamati ilikuwa ni kushiriki katika semina na warsha mbalimbali. Wajumbe wa Kamati walishiriki katika semina ya Mazingira kuhusiana na Hifadhi ya Taifa ya Gombe (Kigoma) na hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale, hifadhi mbili ambazo zinamaliasili ya kipekee kabisa ya sokwe mtu ambao ni adimu. *(Makofi)*

Lakini pia kulifanyika semina kuhusiana na masuala ya Utunzaji wa Maliasili na Mazingira *(Natural Resource Management and Environment)* iliyofanyika Dar es Salaam Mei, 2006 katika Ofisi ya Bunge. Vilevile ilifanyika semina kuhusiana na tathmini ya athari kwa Mazingira *(Environmental Impact Assessment).* Lakini pia palifanyika semina inayohusiana na nafasi ya wafugaji wa Tanzania katika ufugaji wa kisasa ambayo ilifanyika hapa Bungeni ambayo pamoja na Kamati yangu lakini pia walikaribishwa Wabunge wote wanaotoka maeneo ambayo yanawafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine ni ziara za Kamati katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu ziara hizo zililenga katika kukagua utekelezaji wa mipango au miradi mbalimbali. Miradi iliyotembelewa ilihusu usimamizi wa uhifadhi wa Mazingira na matumizi endelevu ya Maliasili na Utalii. Kamati ilitembelea maeneo

yafuatayo, Hifadhi ya Mbuga ya Wanyamapori ya Serengeti na mapori ya Akiba ya Ikorongo, Grument mwezi Machi, 2006. Lakini pia Kamati ilitembelea maeneo ya mazingira yaliyoathiriwa na wafugaji na wakulima katika bonde la Usangu ndani ya hifadhi ya mbuga za wanyama na eneo la ardhi owevu la Ihefu, Mbarali mkoni Mbeya mwezi Mei, 2006. Lakini pia Kamati ya mwezi Oktoba, 2006, ilitembelea viwanda vya Samaki Mjini Mwanza na kutoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Serikali na hivi majuzi mwezi Desemba Kamati ilitembelea Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya kina kuhusushughuli zilizofanywa na Kamati katika kipindi cha mwaka 2006, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira naweka bayana mambo ambayo Kamati ingependa kuona utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa upande wa uhifadhi wa mazingira tunaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kutekeleza kwa dhati mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji kama ulivyoanishwa na Wizara hiyo.

Pia Kamati bado inaweka msisitizo, iwe inahusishwa katika kupitia ripoti za tathmini ya athari kwa mazingira ya miradi mikubwa ya maendeleo kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo, ili Kamati iweze kutoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii, suala la Makumbusho ya Taifa bado halina mkakati madhubuti. Maeneo mengi nchini yaliyo na kumbukumbu za mambo ya kale au kwa Kiswahili cha sasa zinaitwa mali kale hayatunzwi vizuri na hata kuandikiwa historia zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kutenga kiasi cha fedha za kutosha ili kuweza kuanzisha Makumbusho ya Taifa katika kila Wilaya na kuandaa mpango mkakati wa Makumbusho ya Taifa *(National Museum Strategic Plan)* na kuuwasilisha mkakati huo mbele ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kwamba mawasiliano na miundombinu mibovu na duni katika Hifadhi za Taifa hasa hifadhi zilizo Kusini na Magharibi mwa Tanzania unasababisha kutoendelea kwa utalii Kusini na Magharibi mwa nchi yetu. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuendeleza na kuwekeza katika hifadhi hizo badala ya kung'ang'ania kuendelea kuwekeza katika sehemu za Kaskazini pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *Corridor* zinazotumiwa na wanyamapori wakati wa kuhama toka sehemu moja kwenda sehemu nyingine mfano toka Tanzania kwenda Kenya au toka Kenya kuja Tanzania ni muhimu sana kwa wanyamapori. Baadhi ya maeneo ya hapa nchini na *Kenya corridor* hizo zimefungwa kwa kugawa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa makazi. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha *corridor* hizo zinafunguliwa na pia iwasiliane na Serikali ya Kenya ili kutatua suala la ufungaji wa *corridor* hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tafiti mbalimbali za wanyamapori ambazo zinafanywa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapoti *(TAWIRI)* na watafiti wengine huwa

haziwafikii walengwa. Kamati inashauri kwamba *TAWIRI* ikusanye tafiti zote zilizowahi kufanywa na kuzifikisha kwa walengwa kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali mkoani Mwanza inasuasua katika kutafuta kiwanja kwa ajili ya kujenga mtambo wa kuchakata mabaki ya samaki yanayotoka katika viwanda vya samaki, Kamati inaiomba Serikali kulifanyia utafiti suala hili na kuhakikisha kwamba ardhi inapatikana kwa ajili ya shughuli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wenye viwanda vya samaki wanapata faida kubwa kutokana na biashara ya samaki na kwa kuwa bei wanayonunulia samaki kutoka kwa wavuvi ni ndogo sana. Kamati inaishauri Wizara ya Maliasili na Utalii kufanya utafiti wa bei ambayo wafanyabiashara wanawauzia wenye viwanda katika soko la nje na kuweka bei nzuri itakayowawezesha wavuvi kupata maendeleo. Aidha, wenye viwanda vya samaki wachangie kwa kiasi kikubwa maendeleo ya wananchi katika elimu, afya, maji na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Afrika Mashariki kuna sera tofauti za kodi na bei ya biashara ya samaki katika Ziwa Victoria zinatofautiana, Kamati inaishauri Serikali kujadiliana na wenzetu na kuangalia uwezekano wa kuweka sera zilizo sawa katika nchi zote tatu yaani Kenya, Uganda na Tanzania hasa katika masuala ya kodi na bei za samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, mafanikio ya Kamati ya Maliasili na Mazingira katika kutekeleza shughuli zake katika mwaka 2006 yametokana na ushirikiano wa karibu sana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii na kwa jinsi hiyo kutoa shukrani za pekee kwa niaba ya Kamati kwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, lakini pia kwa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu wake Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa ushirikiano mkubwa ambao wameupatia Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka, pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Lawrence Makigi na Michael Kadebe, kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakizifanya za kuratibu shughuli zote za Kamati kwa kipindi chote cha mwaka 2006 pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya nachukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote 29 wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kwa kutoa maoni, ushauri pamoja na ushirikiano wa kutosha kwenye Kamati hali ambayo imewezesha kutekeleza na kufanikisha kazi nyingi za Kamati yetu ya Maliasili na Mazingira. Lakini kipekee niwashukuru Wajumbe hawa 29 kwa kunichagua na kuniamini kuwa Mwenyekiti wao wa Kamati kwa kipindi chote cha mwaka 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi hiyo naomba niwatambue wajumbe wa Kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mheshimiwa Prof.

Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Abdukarim E. Shah, Mheshimiwa Salim Khamis Salim, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni moja ya Kamati kubwa kabisa katika Kamati za Bunge kwa kuwa na wajumbe 29.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kuwasilisha rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira Katika Kipindi cha mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru nimemuona Mheshimiwa Riziki, amekuwa wa kwanza kuunga mkono hoja ya Mwenyekiti wake. Kwa hiyo, naomba kukupongeza sana Mheshimiwa Riziki kwa kuwa wa kwanza kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapa mezani kwangu nina majina mawili tu ya wachangiaji na orodha imefungwa. Kwa hali hiyo, naomba nianze kumwita Mheshimiwa Mgana Msindai na baada ya Mheshimiwa Mgana Msindai, atafuatia Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi na nafikiri maelezo yote nilishayatoa toka mwanzo, naomba Mheshimiwa Mgana Msindai aanze. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi niweze kuchangia taarifa ya Kamati iliyowasilishwa sasa hivi. Kwanza, niwapongeze kwa kazi waliyoifanya na mimi nina machache sana ya kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti aliyetoa taarifa yake sasa hivi ametaja mambo mengi ambayo yanakwamisha Wizara hii zikiwepo *corridors* au kwa Kiswahili chepesi, njia zinazotumiwa na wanyama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa wakati fulani. Yeye amezungumzia juu ya njia kati ya nchi yetu na nchi ya jirani.

Mimi ningependa kuzungumzia njia zilizoko humu ndani ya nchi. Njia hizi nyingi zimezibwa, wananchi wamejenga. Njia hizi nyingi wamegawiwa wawindaji. Kwa hiyo, zinaleta vurugu sana. Nikitoa mfano wa njia chache, kuna njia ambayo inaunganisha Hifadhi ya Tarangire na Manyara kupitia kwa kuchinja. Halafu kuna njia inayounganisha Hifadhi ya Manyara na Ngorongoro kupitia Mang'ora, inapitia ya Idachini, Mang'ora, inakwenda Ngorongoro na hatimaye inakwenda mpaka Serengeti. Hizi njia zote kwa uzembe kabisa ziliachiwa na zimezibwa, watu wamepewa mashamba makubwa wanalima humo, wananchi wameruhusiwa wamejenga.

Kwa hiyo, wanyama wanashindwa kuhama, aidha, kwenda kutafuta maji au chakula kutoka Hifadhi moja kwenda Hifadhi nyingine na hiyo ndiyo inayoleta mgogoro, kunakuwa hakuna mahusiano mazuri ya wanya pori na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayotumika sasa, imeainisha aina ya mapori. Kuna mapori ya wazi ambayo wananchi wa kawaida wanaruhusiwa kwenda kuwinda, kuna *Buffer zones* ambayo ndiyo zinakaa kuwatenganisha wananchi na wanyama, halafu kuna *Controlled Areas* na *Game Reserves*. Sasa hivi hizi zote zimedharauliwa. *Open Areas* ni maeneo ambayo wananchi wanakwenda kufanya shughuli zao, kukata miti, kuwinda na kufanya shughuli zingine kwa maendeleo. Sasa hivi hakuna, zote zimegawiwa kwa wageni na hawa wanamiliki kama maeneo yao. Nikitoa mfano mdogo, ukienda Serengeti, kuna Hifadhi ya Serengeti, halafu kuna Pori la Akiba la Gurmeti, halafu kuna *Buffer Zone* ya Natasbora na Nichoka. Hiyo ndiyo amemilikishwa mgeni, amejenga Hoteli na ndiyo pale ambapo tunasikia kila siku wananchi wanakwenda wanapigwa na askari, wanadhalilishwa bila sababu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli uhasama upo kati ya watendaji wa Hifadhi zetu, wanyama na wananchi na tusipoangalia, haya mambo yatatupeleka pabaya. *(Makofi)*

Sasa hivi Sheria ya Wanyamapori wadau walishaipitia miaka karibu mitatu iliyopita, lakini mpaka leo haijaja Bungeni na ile Sheria imeainisha mambo, ingefuta haya mambo ya zamani, *Game Reserves* nyingine, *Open Areas* na *Controlled Areas* na ndio walikuwa wanaanzisha *Wildlife Management Areas* ambazo hizo zingemilikiwa na wananchi. Lakini mpaka leo, mimi ningeishauri Serikali, kwa kweli wakati umefika tusifanye kazi kwa mazoea, tusifanye kazi kwa sababu mtu yuko pale. Kuna misingi ya kazi iliyowekwa, labda Serikali ije ituambie kwa nini mpaka leo hiyo sheria haijaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilisikitika sana asubuhi Serikali ilipokuwa inajibu Swali Namba 73 linalohusu fidia kwa wananchi. Serikali ilisema wananchi ndiyo wanawafuata wanyama. Si kweli! Mimi ningeshauri kabisa, baada ya Serikali kuzembea, ndio wanawafuata wananchi na ni lazima tuangalie, kwanza ni aibu kutaja kwamba mtu ameuwawa na myama, analipwa 50,000/=, aibu sana. Kabisa, ni aibu kweli kweli! Maisha ya binadamu unalinganisha na 50,000/=! Hata kama ni kifuta machozi, hicho kifuta machozi gani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba niende kwenye lingine, taarifa inatuambia kwamba majangiri kesi zao zinakwenda muda mrefu na wengi wanaachiwa. Kwanza, zinakwenda muda mrefu kwa sababu siyo Mahakimu wote waliona sheria za wanyama pori. Mahakimu wengi sana hapa nchini wa Mwanzo, wa Wilaya, hawana hizo sheria. Kwa hiyo, wanafanya kwa kubahatisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sina hakika, labda waniambie, mtu anakamatwa na Swala, ngozi za Swala au na nyama ya Swala, hiyo kesi inaitwa ya uhujumu uchumi. Haya mambo mengine yamepitwa na wakati, leteni sheria tubadilishe hayo! Kesi inakaa miaka mitatu, yule mtu analetwa mara ya kwanza, ngozi ya swala, analetwa mara ya pili mwezi unaofuta anaachiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningeshauri kabisa sheria hizo ziletwe, sheria hii mpya ya wanyamapori iletwe tuipitishe na sheria ambazo zinatumika sasa zipelekwe kwa Mahakimu na hizi mpya pia zipelekwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ukiangalia mahala ambapo kuna Vikosi vya Kuzuia Ujangiri ambao kuna waendesha mashitaka wa idara, kesi hazikai sana na nyingi zinahukumiwa kwa kuwaadhibu wahusika. Siyo Waendesha Mashitaka wote wanaojali kesi za Wanyamapori, lakini ingekuwa ni muhimu sana kama Idara ingefundisha Waendesha Mashitaka wao *at least* kila Mkoa wawepo, pale kesi zitakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo juu ya Makumbusho. Kwa kweli hapa kwetu Tanzania suala la Makumbusho hatulitilii maanani. Maeneo mengi sana yenye Makumbusho ya kudumu yanaharibika, yanapitwa na wakati. Tunaangalia ile Makumbusho iliyoko Dar es Salaam tu. Ukienda nchi zingine, kila Mkoa una Makumbusho yake, kila Wilaya ina Makumbusho yake na kuna maeneo yenye mambo ya zamani, kuna maeneo yenye mapango, yenye ngoma za asili, yenye michoro ya asili, yenye vifaa vya asili, lakini Wizara haitilii manani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Jimboni kwangu, kuna mapango yenye ngoma ambayo watu wawili/watatu hamuwezi kubeba, mpaka leo zipo. Kuna vifaa vingi vya kale vilikuwa vinatumika, vinaharibika, yale mapango yanaharibika. Kwa hiyo, mimi ningeomba sana Serikali itilie maanani mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye uwindaji, tunasema hapa Bungeni Serikali inapoteza hela nyingi sana kwenye dhahabu na maadini mengine, mimi niwaambie mpaka sasa Serikali inapoteza hela nyingi sana kwenye hawa wawindaji wa kitalii. Ushahidi upo na kwanza kwa sababu askari wa kukaa na hawa sasa hivi wamepungua au wamezeeka, wako wachache sana na nikisema Idara ya Wanyamapori, upande wa Misitu, upande wa Uvuvi, hawa watu wanaotakiwa kukaa kuangalia mapori yetu, kuangalia mambo ya uwindaji, wengi wameshafikia umri wa kustaafu na mpaka sasa kasi ya kufundisha wengine ni ndogo sana.

Kwa hiyo, wanakuja baadhi ya wageni, anapata Nyati anampiga. Akikutana na Nyati mwenye *trophy* kubwa zaidi, ile ataitupa apige ile, nani atamzuia? Usimamizi wa hizi kambi ni mdogo, ni hafifu sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nigeshauri sana, tuna Vyuo vyetu vya kufundisha, tuna Chuo cha Mweka. Watanzania kutoka Idara ya Wanyamapori wanaokwenda pale ni wachache sana na huku hatuna askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Chuo cha Pasiansi, kile Chuo kinazeeka, hakipewi pesa za kutosha. Kwa hiyo, hata askari wanaokwenda pale, sasa hivi kwa kweli wanatoka hawatoshi. Sasa mimi ningeiomba sana Serikali iangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema naishukuru sana Wizara ya Maliasili, lakini Kamati bado hamjafanya kazi ni juu yenu kupita kuona haya matatizo na mnayafichua! Tusiendelee kupoteza urithi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tunataka hiyo sheria ambayo zaidi ya miaka mitatu wadau wote walishapitia ije Bungeni. Tunataka zile *Wildlife Management Areas* ambazo ndio wananchi watapewa nguvu za kuzimiliki na kuwatunza wanyama wetu, zije, zipitishwe, zianze kazi. Tunataka wale wawindaji wanaopewa maeneo, wakorofi, kwa mfano ukienda Pori la Wazi la Makao, kuna Wahadzabe wanakaa pale na Wahadzabe huwa wanaruhusiwa kukaa kwenye haya maeneo hata kwenda kukata kuni, kupata maji, kupata asali, wanazuiwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningeshauri sana na tuzingatie kwamba tuchukue mfano wa Namibia, sasa hivi wale Hotetotsi waliishitaki Serikali na wakashinda kesi na hawa Wahadzabe tusiwachukulie kwa mzaha. Tuwape haki zao na wale wanaowanyanyasa hawa watu, wachukuliwe hatua kali. Tusiwalee watu ambao hawaendani na misingi ya ubinadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, tunasema tunaibiwa kwenye madini, kwenye Wanyamapori tunaibiwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Taarifa ya Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi pia napenda nitoe pole kwa wafiwa wote ambao wamepatwa na msiba wa Mheshimiwa Juma Akukweti pamoja na Waandishi wa Habari. Nawapa pole sana. Marehemu roho zao ziwekwe mahala pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa wale Wabunge wenzetu ambao wamepewa nyadhifa za kuwa Mawaziri na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina maelezo mengi isipokuwa nitaeleza maeneo machache. Kwanza, nitaanza kuhusu vitalu na Hifadhi za Wanyama. Ningependa kufahamu kwamba kuna asilimia 25 ambazo huwa zinatolewa kwa vijiji ambavyo viko karibu na Hifadhi hizi au na Vitalu hivi. Hizi asilimia 25 kwa kweli zimekuwa ni utata mkubwa katika Halmashauri zetu na maeneo yetu hususan katika Wilaya ya Kilwa ambako tunayo maeneo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 25 hizi zinatusumbua kwa sababu hatuelewi nani anazijua kwamba hizi ni asilimia 25 katika mapato ambayo wanapewa wanakijiji. Mfano, wanakijiji wanapewa milioni 3 au milioni 6 kwa mwaka kwamba ndio asilimia 25 na wakati huo huo watu wa Kilwa, pengine ni ngumbalu, hatuelewi chochote. Mimi sioni uwiano uliopo, mwaka mzima milioni 3 au milioni 6 ziwe asilimia 25. Ni wanyama wangapi wameuwawa katika kipindi cha mwaka? Sielewi kila mnyama ni kiasi gani pale anapowindwa na sielewi ni nani ambaye anasimamia hizi asilimia 25 kujua kwa mwaka wamewindwa wanyama kiasi gani na mnyama wa aina gani na kila mnyama shilingi ngapi ili ipatikane hii asilimia 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi natoa ushauri, Serikali iwe wazi kwa jambo hili ili wananchi waelewe hii, asilimia 25 iko vipi kwa sababu naona haieleweki shilingi milioni 3 au milioni 6 iwe asilimia katika mapato ya mwaka mzima kwa ajili ya kijiji kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulifahamu katika Wilaya yetu tuna maeneo mbalimbali ya kitalii. Kuna eneo moja linaitwa Maliwe. Eneo hili la Maliwe kuna ndege makundi mengi, makundi makubwa makubwa ya ndege wazuri, kuna Viboko vinapata kama 3,000, kuna Mamba, kuna Tembo. Eneo hili ni bwawa, lakini eneo hili kuna mwekezaji ambaye amejenga kuzunguka lile bwawa. Wananchi wa eneo lile hawaelewi ni wakati gani hawa wamepewa ruhusa ya kuja kujenga pale, kibali kimetoka wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe lile ni eneo ambalo wanyama mbalimbali, licha ya wale ndege wanaoishi pale na viboko, ni njia maarufu ya kwenda kupata maji kwenye lile eneo. Lakini wao wamejenga vibanda na mwananchi haruhusiwi kuingia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi wa Wilaya, Madiwani waliwahi kwenda pale kuulizia wapate kujua nani wamewapa kibali, lakini majibu yaliyotoka pale ni ya kijeuri ya kujibu kwamba Bwana mkubwa yuko kwenye kibanda, kwanza anapumzika na anapata chakula, kwa hiyo, hawezi kuwaoneni nyie. Hii ni jeuri kubwa kwa watu ambao wanalinda mali za maeneo yao na waangalizi wa wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hawa wawekezaji jeuri hiyo wanapata wapi? Si hayo tu, kuna maeneo mengine ambayo tayari yana mipaka kamili kwa wawekezaji na wanakijiji walikuwa tayari wanajua kwamba sisi tunakaa hapa, mwisho wetu ni hapa. Lakini, la kusikitisha ni kwamba wawekezaji hawa wanaongeza mipaka wao wenyewe wakidai kwamba maeneo yao yameongezwa na wananchi hawana taarifa. Matokeo yake wananchi wanasogezwa kidogo kidogo kwenye maeneo yao na wao wakijichukulia nafasi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kusikitisha ni kwamba hata maeneo yale ambayo yalipaswa wananchi wayatumie, mfano kuna Mto Matandu, hawa watu walikuwa wanatumia eneo mpaka wa mwanzo lilikuwa ni eneo linaitwa Hololo hadi kwenye eneo la Mbuga hiyo *Selous*. Lakini sasa hivi wamejiongezea mpaka hadi katika Mto Matandu ambako wananchi walikuwa wanaenda kuvua, lakini sasa hivi wananchi hawana ruhusa ya kuvua kwenye lile eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa pia Madiwani walikwenda, lakini matokeo yake yalikuwa ni karibu watu wapigane mangumi pale kwa jeuri ya hawa watu. Bado nauliza jeuri hii wanapata wapi na haya ni maeneo yetu ya asili na sisi tunahitajika kupata manufaa kwenye maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ningependa kujua na utatuzi wake pia ufahamike na wananchi wa Kilwa waelewe ni ipi haki yao katika maeneo yao! Tuendelee kuwa maskini wakati rasilimali tunazo au tuendelee kuibiwa na hawa wageni wakipewa kipaumbele kuliko wananchi wa Kilwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama nilivyoeleza sina maelezo mengi, isipokuwa ninachotaka kujua kingine, kuna huu mpango wa kuhusu mifugo kupelekwa Mikoa ya Kusini, siyo mpango mbaya, kwa ujumla nauzungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpango huu haujakamilika. Nina maana kwamba tangu ulipotangazwa huu mpango, mifugo ile mifugo ianze kuingia pale. Lakini ninavyokueleza hivi sasa hiyo miundombinu, hakuna malambo ya hawa wanyama kwamba wakifika pale watakuwa wanatumia, hakuna majosho ya kutosha na inawezekana kama ni kuna josho basi ni moja au ni mawili na hiyo mifugo yatari imeishaanza kuingia katika Mikoa yetu kabla hata hiyo ruhusa haijatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi kwamba mpaka itakapokuwa tayari naona ile idadi ya 75,000 itakuwa imekamilika kabla na ikiwezekana sasa hivi tayari imeishafikia mifugo hiyo wakati maandalizi haya hayajaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona wananchi wa Kusini, tuko kwenye matatizo. Sisi wakati huo tunahimizwa tuandae kilimo, tuwahimize wananchi kilimo, tuwahimize wananchi utunzaji wa mazingira, bado tunaletewa mizigo mingine ambayo haijakamilika imeishajaa kule. Nina amini kwamba si matakwa yetu, si kwa faida yetu ya watu wa Kusini, ni faida ya wale ambao wanaleta ile mifugo. Sisi kwetu watu wa Kusini au wa Mkoa wa Lindi ni adha tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba hili suala ni zuri, lakini likamilike pale watakapokamilisha yale ambayo wameahidi kuyatekeleza kabla ya kuleta mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo, itengeneze mkakati maalum au mazingira mazuri kabla ya kutuletea hii mifugo maana yake mpaka sasa hivi hali halisi ukipita hii njia ya kwetu ni mizoga mitupu huko njiani harufu, hakuna sehemu ambayo utapita bila kukuta mizoga na mifugo imeshaona maeneo mbalimbali hata zile Wilaya ambazo hazikuhitaji kuletewa mifugo tayari mifugo imeshaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatoa hili kama ni kero na ninaomba Wizara iliangalie tena kwa uangalifu na ipange mkakati kabla ya kutuletea hii mifugo kwenda kututia adha katika Mkoa wetu wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie katika Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira.

Kwanza kabisa, ningependa nipongeze utaratibu huu wa kuruhusu Waheshimiwa Wabunge kuchangia katika kazi zinazofanywa na Kamati mbalimbali. Uchambuzi huu unatuwezesha sisi wote kuwa wamoja katika kazi kwa sababu mgawanyo wa Kamati una maana tu kwamba hatuwezi wote tukakaa Kamati moja. Kwa hiyo, mimi naupongeza sana utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili, uchambuzi wa Kamati ni kazi muhimu ya Bunge. Bunge lina kazi moja kubwa labda nitumie neno la Kiingereza, *oversight* yaani

usimamizi wa shughuli za Serikali. Kwa maana hiyo basi, tunapopata nafasi ya kuchambua kazi za Kamati, tunapata nafasi pia za kusimamia kazi za Serikali ambazo zimeletwa na sisi wenyewe katika kazi zetu mbali mbali za Kamati. Ninayo haya yafuatayo:-

Wakati nikiwa Waziri wa Maliasili na Utalii mwaka 1985, kabla wengine hawajazaliwa, kwa hiyo, hapa ni ka-*encyclopedia* kadogo kamesimama, nilipata nafasi ya kuongoza ujembe wa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na wote wanaohusika katika sekta hii katika mikutano ya Utalii Ujerumani. Wataalam wangu wakaniambia, "Mama Mongella hatuna hoteli nzuri," wakati ule ndio kulikuwa na mbanano mpaka watalii wetu wanajaa kwenye Mbuga hatuna pa kuwalaza. Sasa tutasema nini katika hotuba yetu! Nikawaambia nyie subirini. Kwa hiyo, nilipofika pale nikasema *"I have just come here to tell you that in a village you can have a beautiful girl but poor, without shoes, without very fancy jewels, but that girl is beautiful. Tanzania is beautiful but poor." (Makofi)*

Kwa hiyo, wote wakaona kwa kweli niliyoyasema ni ukweli. Lakini mimi nafikiria miaka imepita, *we can not continue to be beautiful and poor.* Naomba nitoe mifano michache, ukiangalia maeneo ya Tanzania hakuna Wilaya hata moja ambayo haina sehemu nzuri, ukifika utabaki mdomo wazi. Naanzia Kojani, Pemba kuna mandhari nzuri, ni mahali pazuri na kuna maeneo makubwa ya fukwe katika kisiwa hiki cha Kojani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija katika visiwa vingine vya Zanzibar na Unguja na vyenyewe vina uzuri huo huo. Ukienda Kitulo, Makete hali ya hewa na uzuri wa Kitulo utashangaa utafikiria uko Swaziland. Lakini pia ukienda sehemu inaitwa Umalila, Mbeya huko ni pazuri mno. Ukipanda Mlima Kilimanjaro ambao mimi nilifanikiwa kuupanda mwaka 1986 napo utashangaa kuona uzuri na maajabu ambayo Mungu ameyaweka katika sehemu hiyo, ndio maana Wachaga walikuwa wanauabudu huu mlima kwa sababu una maajabu ya peke yake. Ukienda Kisiwa cha Mafia na visiwa vingine vidogo ni vizuri mno. Sisi tunaotembea duniani huwezi kuona sehemu nzuri kama ya Mafia, *unpolluted,* maji yake safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, ukienda Kondoa na ukifika Ukerewe ndiyo utashangaa zaidi. Visiwa vile ni vizuri kweli kweli na ninawakaribisheni wote siku mmoja mje muone uzuri wa visiwa vile. *(Makofi/Kicheko)*

Nimetaja mifano michache tu ya kuonyesha nchi hii ilivyo nzuri. Katika utalii kuna kitu kinaitwa *product,* mnauza *product*. Tanzania *tourism product* tunazo nyingi *sea plan*, milima, mambo ya kale na mambo mengi tu, tunazo ngoma, kuna kitu kinaitwa *cultural tourism* mtu akija tu akaanzia Dar es Salaam anaangalia ngoma zetu ni utalii wa kutosha mpaka akifika Mwanza atakuwa ameona wanadamu wanaoishi katika eneo hili wana ujuzi wa muziki, nyimbo na mambo mengi tu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimeyataja haya, leo asubuhi nilipokuwa nasikia kwamba dhahabu ni kitu kidogo kuliko wale wanaowekeza, nilikuwa nashangaa. Hivi sisi tukiwa na dhahabu tuna tofauti gani na Libya iliyo na mafuta? Hivi mafuta yana thamani kuliko dhahabu au sisi ndiyo hatujaona ya kwamba dhahabu tuliyonayo ni mtaji ndiyo tungekuwa tunakuja hata katika uwekezaji wa utalii tusingejiona ya kwamba sisi hatuna kitu. Ardhi ni mtaji mkubwa kwa hiyo mimi ningependa kusema kama ingewezekana wenzetu walio kwenye

Kamati hii watusaidie kuangalia thamani na kuthaminisha sehemu mbalimbali tulizo nazo na tuziangalie kama mtaji wa kuweza kuzungumza na wale wanaowekeza *if not at par,* basi sisi tukiwa na nafasi kubwa zaidi kuliko wao kwa sababu wanapokuja huku saa nyingine hawana kitu, wanakuja wanawekeza kidogo ambacho wanajua baada ya muda mfupi wataondoka na kuacha sehemu zetu mbaya kama vile walivyozikuta. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningependa wakati Kamati hii inaangalia na kusimamia shughuli za Serikali iweke umakini katika kuangalia mikataba ya uwekezekaji katika maeneo ya utalii. Lakini pia, kuangalia ni kiasi gani ambacho nchi yetu tunaweza tukawekeza katika maeneo yanayoweza kuzalisha kwa haraka zaidi. Kwa mfano, ukienda Rufiji na ukafika mpaka visiwa vya Mwera ambako mimi nilifika kuna uzuri wa Mikoko ambao hujapata kuona, utafikiria ile bahari ina barabara na *airports* za maji. Hatuoni uzuri huo ikawa ndiyo *(bargaining power)* kichocheo chetu cha kuombea kwamba wewe unakuja kuwekeza usionione mimi kama sina kitu, mimi nilichonacho ni hiki na thamani yake ni hii na ndivyo dunia nzima wanavyofanya ya kwamba kila kitu kinathaminishwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, na sisi tuthaminishiwe uzuri tulionao na tukikutana na wawezaji siyo kujionyesha sisi ni kama mbwa mbele ya chatu. Kwa sababu mbwa akiona chatu anajipeleka mwenyewe kwenye mdomo wa chatu analia anakwenda, sisi tunapaswa tukae tuonyeshe ya kwamba na sisi tuna mali. Kwa hiyo, unapokuja kuwekeza tuzungumze mazungumzo ambayo mimi ninacho na wewe unacho. Kama una mitambo mimi nina dhahabu, kama wewe una fedha za kujenga hoteli mimi nina ardhi na nina fukwe ambazo ni nzuri au visiwa ambavyo ni vizuri. Mimi ningependa wenzetu mnaosimamia Kamati hii, mtazame namna ya kuthamanisha uzuri wa Tanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Jambo la pili ninalotaka nilizungumzie ni uvuvi. Kwanza, nafurahi kwamba Mwenyekiti ameona taabu ya wavuvi kwamba katika Ziwa Victoria wavuvi wananyonywa. Kama kuna mrija mkubwa ni ule unaonyonya wavuvi walioko katika Ziwa Victoria na nimekuwa nikiangalia kwa makini kwa nini uvuvi haramu unaongezeka kwa sababu thamani ya samaki kwa wanaovua ni kidogo kwa hiyo, lazima wavue samaki wengi sana ili aweze kukidhi mahitaji yake. Nadhani hili suala ni vizuri likaangaliwa kwa makini na kuangalia pia kwa mfano ukichukua mazao kama pamba inasindikwa pale inapolimwa. Hivi kwa nini Wilaya ya Ukerewe hamjatusaidia kuwa na kiwanda, samaki waende wafike Mwanza wameshaoza na kumbe wangesindikwa humo humo ndani ya kisiwa tukatoa *made in Ukerewe* wanapelekwa Ulaya. Kwa hiyo, nilifikiria ni namna ya kuondoa umaskini. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini napenda niseme kuna wanyama, mamba na kiboko na hawa wanalindwa Kimataifa, wako Rufiji, wako Rukwa, wako Ukerewe. Lakini hata siku moja hatujafikiriwa kupata 25% ya kwamba tuko kwenye mbuga, tunakumbana kule majini sisi tukiogelea na wakati mwingine wanawatafuna watu. Bahati mbaya Ukerewe hatujapata hata shilingi 50,000 labda tutatoa *list* ya wote waliokwishaliwa ili fidia itolewe. Kwa hiyo, mkubali Kamati kunisaidia nitakapokuwa nimetoa orodha ya watu walioliwa katika Vijiji vya Kamea, Busagami, Ngoma na mahali pengine waweze kupewa angalau kifuta machozi. Lakini kwa kweli ni aibu shilingi 50,000 haitoshi hata sanda. Kwa hiyo, nadhani tufikirie kama hii ilitungwa zamani wakati fedha yetu bado ina nguvu nadhani ibadilishwe. *(Makofi)*

Mwisho, ningependa tu nipendekeze ili tuweze kuthaminisha Tanzania *(mapping)* upimaji wa ramani na kujua nini kiko wapi ni muhimu ndiyo maana sasa wafugaji wanagombana na wakulima, wakulima wanagombana na misitu na hivyo hivyo tunakwenda nadhani tufanye *mapping* na wako vijana watalaam ambao mimi nawafahamu wana taasisi yao ya upimaji wakipewa nyenzo wanaweza wakapima tukajua kipi kiko wapi na namna gani tutaweza kukitumia kwa manufaa yetu na huenda tukakiwekea hata Wilaya zikawa kama tunavyopata ardhi ofa na ukapewa hati ya kumiliki. Kwa hiyo, nayo iwepo ndiyo itakayowawezesha Watanzania wanaoishi katika maeneo hayo kama hawa Wahadzabe waweze kupata haki ya kusema na wao wana haki katika ardhi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ningependa niseme naunga mkono Kamati, lakini nawaomba tu wawe macho zaidi katika hivi vya kuthamanisha kile tulichonacho ili kesho na keshokutwa tusiwalalamikie hawa wawekezaji ambao sisi ndiyo tumewaleta na tukajifanya ya kwamba sisi hatuna, wao ndiyo wana kitu kuliko sisi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikiliza mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Mama Getrude Mongella sasa kupitia kwa Mheshimiwa *Chief Whip,* Serikali nayo ingependa kuchangia katika hoja hii na kwa kuwa hoja hii ni ya Mwenyekiti wa Kamati, basi yeye ndiyo atakuwa mtu wa mwisho wa kuhitimisha hoja yake. Kupitia kwa *Chief Whip* ninao Waheshimiwa wawili, Waziri mmoja na Naibu Waziri mmoja. Kwa hiyo, nitaanza kumpa nafasi Waziri wa Maendeleo ya Mifugo halafu baadaye tutampa nafasi Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda na mimi kuchangia hoja iliyo mbele yetu inayohusu Kamati ya Maliasili na Mazingira. Kwanza, napenda kuwapongeza Wanakamati kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakitoa hasa kwa Wizara yangu. Lakini pili, kwa taarifa ambayo imeandikwa kwa umakini na hoja ambazo zimetolewa ambazo ni za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitazungumzia suala moja ambalo linazungumzia juu ya kuhamisha wafugaji kutoka maeneo ya vyanzo vya maji na kwa kufuata agizo la Serikali lilikuwa eneo la Ihefu, Mbarali Mkoa wa Mbeya. Mpaka ninavyozungumza hivi leo, zaidi ya ng'ombe 204,000 kati ya ng'ombe 235,000 ambao walitarajia kuhamia au kuondolewa kwenye eneo wamekwishaondolewa. Sasa napenda nikiri kwamba katika kufanya shughuli hiyo kuna makosa yamejitokeza kwanza makosa hayo ni kweli kutokana na kwamba nchi nzima tulikuwa kwenye matatizo makubwa ya ukosefu wa umeme kwa hiyo, maagizo tulipoyatoa na *panic,* wanaishi bila taa, viwanda vinaishi bila umeme na kadhalika kwa hiyo, zoezi hilo ikabidi lifanyike kwa haraka.

Sasa kama ilivyo binadamu, kawaida binadamu hatuko *perfect* kwa hiyo kuna matatizo madogo yamejitokeza hapa na pale, lakini zoezi lenyewe naweza kusema limefanikiwa kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Lakini hoja moja ambayo mchangiaji mmoja amezungumza kwamba mahali ambako tulikuwa tunapeleka mifugo tulitakiwa kuweka miundombinu. Mpango wa Serikali uko pale pale maeneo hayo kweli na kuna fedha tumetenga yatawekewa

miundombinu ili kuweza kuhudumia mifugo pamoja na familia ambazo zitahamia maeneo hayo nina hakika zinahitaji shule, zinahitaji zahanati na kadhalika. Sasa hii itakwenda sambamba na mipango ya Halmashauri zenyewe za Wilaya kwa sababu hatuwezi kufanya operesheni kwamba tutengeneze maeneo kwanza kabla ya kupeleka mifugo kama nilivyosema tulikuwa na tatizo la umeme ambao chanzo kikubwa cha maji kilikuwa kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, tungeacha hali hii, nina hakika kwamba hata leo tusingekuwa tunazungumza linalozungumzwa leo. Taarifa tulizonazo kwamba bwawa la Mtera limejaa maji sasa hivi na limeshaanza kufanyakazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna hayo matatizo kwamba kuna baadhi ya maeneo tumepeleka hizi huduma lakini hazitoshelezi, ni majukumu yetu kama Serikali kutoa hizi huduma kwa wafugaji ambao walipangiwa maeneo ya kwenda. Hawakwenda kiholela tu tuliwapangia Wilaya za kwenda ambazo ni Kisarawe pamoja na Wilaya ambayo Mheshimiwa Mbunge aliyeyazungumza ni sahihi kwamba kuna baadhi ya wafugaji wamepelekwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Watanzania na ndugu zetu wafugaji wawe na subira ambayo tutaweza kupeleka huduma hizi kulingana na mipango na kwa bahati nzuri kama nilivyoeleza hapo zaidi ya shiligni bilioni 6.3 zimetengwa kwa shughuli hiyo ambazo ni nje ya kawaida ya bajeti yetu. *(Makofi)*

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba kuna baadhi ya mifugo wamekufa na kufa kwa mifugo kunatokana na siyo kwa magonjwa lakini pia uchovu kwa sababu wengi walikuwa wanasafiri umbali mrefu zaidi na kwa bahati mbaya sana kwa sababu ya *panic* na uharaka wenyewe. Kawaida mifugo wakati inasafirishwa inatakiwa ipumzike kila baada ya siku kadhaa inatakiwa ikae sehemu fulani kwa muda ili iweze kupumzika hasa kuchekewa hasa mifugo ambayo inakuwa na magonjwa ambayo hayajagundulika wakati wanaondoka sehemu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema nakubaliana kuna baadhi ya watendaji wetu wamefanya makosa ya hapa na pale lakini zoezi lenyewe ukweli ni kwamba limefanyika kwa hali ambayo kama nilivyosema ya udharura. Matatizo mengine ambayo yamefanyika kwa makusudi kama nilivyotoa tamko la Serikali hivi karibuni, Serikali inafanya uchunguzi ili tuone ni mambo gani hayo ambayo tunaweza kuyarekebisha. Uhamishaji bado umebaki kiwango kidogo lakini tunakubaliana kwamba kuna baadhi ya mifugo wameingia ambao hawakuwa wamepangiwa. Sasa ni kawaida chini ya Waraka namba moja wa mwaka 2002 Serikali, ilielekeza jinsi ya kusafirisha mifugo kutoka eneo moja hadi jingine. Lakini kwa bahati mbaya sana kuna baadhi ya watendaji wetu kwenye Halmashauri ama kwenye Wilaya hawakufuata hivyo.

Kwa hiyo, uhamishaji huo angalau ulilenga kutoa mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine kuna baadhi ambao siyo wengi walichukua *advantage* hiyo wakahama kutoka eneo moja kwenda lingine nje ya ule utaratibu. Sasa hayo ni makosa ambayo ni *percent* ndogo sana ambayo haiwezi kutufanya tuseme kwamba zoezi lilikuwa ni baya.

Kwa hiyo, Serikali kupitia Wizara yangu imeelekeza kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Halmashauri husika ili mahali ambapo makosa yamejitokeza yaweze kusahihishwa. Lakini ninaloweza kulisema ni kama nilivyokuwa siku ile nawasilisha Muswada wa Nyama hapa kwamba wafugaji ni Watanzania na kwa miaka mingi tangu tupate Uhuru, Watanzania tumejua Tanzania ya wafanyakazi na wakulima.

Tunapozungumza juu ya wakulima, wafugaji wako ndani ya *group* la wakulima. Sasa tusifike mahali tukaanza kubagua wananchi kwa shughuli zao wanazozifanya. Tukianza kujenga tabaka la kusema kwamba kuna wafugaji na ni watu wabaya… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ya moto ililia)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Hebu tunaomba wenzetu wanapofanya utaratibu wa kuzingatia hili linalotokea basi sisi tuendelea.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Ni *alarm* ya moto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unaniruhusu niendelee nisikimbie. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, kama nilivyomalizia kusema Watanzania wote tuna uhuru, Katiba inaturuhusu kuishi sehemu tunakopenda kwa kufuata utaratibu. Matamko mengine yamefanywa na baadhi ya wanasiasa wenzetu kusema kwamba wafugaji wanataka kuonekana kama ni watu wabaya ambapo siyo sahihi. Ufugaji ni uchumi, ni kama wanavyofanyakazi kama Watanzania wengine wanaofanyabiashara za maduka, biashara za kilimo, ufugaji nao ni shughuli mojawapo ya kiuchumi. Siyo vema tukasema kwamba wafugaji hawaruhusiwi kwenda mahali. Sehemu zimeainishwa, Mikoa tuliiuliza vizuri ikatueleza maeneo ambayo wana ardhi ambayo wanaweza kufanyakazi na ikatumika kwa ajili ya ufugaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi kama wana siasa, kama viongozi Watanzania hao ni vema tukaona ni Watanzania wanaofanyakazi zao za kihalali. Kwa hiyo, napenda nimalizie kwa kuwaomba Watanzania wote tusaidie wafugaji kama tunavyosaidia wakulima, tusaidie kama tunavyosaidia wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii sekta binafsi ndiyo *engine* ya maendeleo yetu. Namalizia kwa kusema na mimi naunga mkono taarifa yangu ya Kamati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira na Maliasili. Kwanza, niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa waliyofanya na kwa kuwasilisha ripoti nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii, imefanya kazi kubwa katika kutueleza matatizo yaliyopo katika kulinda mazingira, kutunza hifadhi zetu za wanyamapori, sekta ya uvuvi, sekta ya mambo ya kale, sekta ya mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina vivutio vingi na kama mtu angependa ku-*sample* vichache angesikiliza hotuba nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Rais wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Lakini ningependa kuongeza kwamba nchi yetu ina hifadhi kama Serengeti ambayo hivi karibuni ilitangazwa kuwa ni ajabu jipya la saba la dunia. Aidha, nchi yetu ina kivutio kikubwa kama Ngorongoro ambapo wakati Mtume Noah alipokuwa anapeleka watu wake kwenye ile nchi aliyoahidiwa na Mwenyezi Mungu wanyama wake

walitawanyika ndani ya *Ngorongoro Crator*. Hata hivi leo ukifika pale Ngorongoro utakuta mguu wa Nabii Nuhu uko pale na watu wangejua haya na wangejua kwamba pale Ngorongoro ndipo ilipo *Olduvai Golge* ambapo mtu wa kwanza duniani aliishi ni uhakika kabisa kwamba wangekimbilia kwenye nchi yetu. Sasa katika sekta ambayo ina vivutio vingi namna hii, ina hifadhi nyingi kiasi hiki pia yanakuwepo na matatizo. Tunawashukuru sana Kamati kwa kuyaelezea kwa kifupi na Waheshimiwa Wabunge, walioyazungumza kwa kuyaelezea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuyatolea maelezo machache tu kati ya hayo. Moja ya hayo ni hizi *WMA*. Miaka mitatu iliyopita, Wizara ilianza kazi ya kuwahusisha wananchi katika kuhifadhi na kufaidika na malialisi tulizonazo. Katika *pilot project* ya kwanza idadi ya vijiji 16 ilianzishwa katika Mikoa mbalimbali na ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba jana *WMA* za kwanza nne zilikuwa zimeshaandikwa kwenye Gazeti la Serikali na zilipatiwa shilingi milioni 50 jana kwa kutekeleza na kufikia viwango vile vinavyohitajika. Aidha, *WMA* hizo ziko Ipole katika Wilaya ya Sikonge, Uyui katika Wilaya ya Urambo, Burunge katika Wilaya ya Babati na Ngarambe Tapika katika Wilaya ya Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *WMA* zingine tano ziko njiani kufikia hatua hizo. Nazo ni Enguimeti katika Wilaya ya Longido, Wami Mbiki katika Wilaya ya Morogoro, Mvomero, Bagamoyo mpakani hapo, Idodi Pawaga katika Wilaya ya Iringa, Ikona katika Wilaya ya Serengeti na Songea katika Wilaya ya Namtumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WMA* zingine tano zimebakiza hatua moja tu ya kutekeleza na kufikia kiwango cha kuandikishwa na kuwa *authorized areas* nazo ziko Tarime katika Wilaya ya Tarime, Makami katika Wilaya ya Kiteto, Tunduru katika Wilaya ya Tunduru, Liwale katika Wilaya ya Liwale na Ukutu katika Wilaya ya Morogoro. *(Makofi)*

Aidha, katika *WMAs* 16 ambazo ndizo zilikuwa zimeanza kama *pilot project* ni *WMA* mbili tu ambazo bado hazijafikia hatua hiyo. Kwa hiyo, tumepata uzoefu wa kutosha na sasa tunaweza kuendelea na shughuli hii kwa kuwa na *data,* kuwa na taarifa na kujua namna ya kwenda. Ningependa tu kusema kwamba kazi ya kuanzisha na kuziwezesha *WMA* ziweze kufanyakazi vizuri ni kazi kubwa kwa sababu kiutamaduni sisi tukiwa na maeneo yenye wanyamapori kwa kweli huwa tunakwenda kuwinda, kuhifadhi na kutumia mali hizi kwa muda mrefu ni kazi ambayo tunahitaji kuelimishana kwa muda mrefu na mimi kama tunafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa nilitolee maelezo ni juu ya kupiga marufuku usafirishaji nje ya nchi wa magogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa kwamba Waheshimiwa Wabunge, wanataka kujua *WMA* ni kitu gani. Alieleza Mheshimiwa Mgana Msindai, *Wildlife Management Area* maana yake eneo la wanakijiji kuhifadhi na kutunza maliasili kwa manufaa yao. Ile aliyosema kwamba inatusaidia sisi kama wananchi kuweza kuhifadhi na kutunza maliasili zetu kwa faida yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumze kuhusu suala la kusafirisha magogo nje ya nchi. Wote mtakumbuka kwamba tarehe 1 Julai, 2004 Serikali ilipiga marufuku

uuzaji wa magogo nje ya nchi. Sababu zenyewe ni kwamba kulikuwa na ukataji mkubwa sana wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mdudu gani analia humu ndani? *(Kicheko)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Taarifa. Naomba maelekezo ya Mwenyekiti.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Kanuni namba ngapi Mheshimiwa?

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Kanuni namba 42.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa, tafadhali endelea!

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakuwa na wasiwasi mmoja. Hivi vyombo viliwekwa kutupa *alarm.* Je, tukiendelea kutovisikiliza kuna siku tutakuwa na matatizo tutafikiria ni yule mbwa mwitu. Kwa hiyo, sasa ningependa angalau utupe maelekezo kuhusu hizi *alarm.* *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kuipokea taarifa ya Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella. Kwa maelezo ambayo ninayo hapa Mezani sasa hivi nimeombwa tutulie kwa sababu kinachoonyeshwa si kwamba ni kitu ambacho kinaweza kuleta matatizo, lakini maelekezo zaidi sasa hivi wataniletea na nitawapa taarifa ni nini kinachoendelea zaidi ya hapo. Naomba tuendelee Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa maelezo yako. Tunategemea kwamba *alarm* hizi hazitatokea tena na kwamba tutakaa kwa usalama usalimini humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema tarehe 1 Julai, 2004 Serikali ilipiga marufuku uuzaji na usafirishaji wa magogo nje ya nchi na sababu ya kupiga marufuku hiyo ilikuwa ni ukataji magogo na miti ambao ulikuwa umepita kifani, ambao ulikuwa unahatarisha mazingira ya nchi na kuongeza joto na kuhatarisha nchi yetu kuwa jangwa.

Pili, ukataji huu wa magogo na uuzaji wa magogo nje ulikuwa hauna tija kwa sababu magogo hayo yalikuwa yanauzwa kama ghafi, kwa bei ya chini na yalikuwa yanapelekwa kwenye nchi ambazo zenyewe zimepiga marufuku uuzwaji na ukataji miti kwa ajili ya kuuzwa kama magogo. Baada ya kupiga marufuku huko Makampuni 16 yaliilalamikia Serikali kwamba yalikuwa yameshakata magogo na mengine yamesafirishwa mpaka Dar es Salaam na mengine yako kwenye maghala katika maeneo mbalimbali nchini na makampuni hayo yakapewa muda wa miezi sita kusafirisha magogo hayo. Baada ya muda huo kukamilika bado makampuni kumi yakalalamika kwamba bado yanayo magogo maeneo mbalimbali ya nchi na yalikuwa yanaomba yahurumiwe tena na yapewe nafasi ya kuyauza. Serikali ikayaruhusu tena makampuni hayo yasafirishe hayo magogo yaliyokuwemo na baadaye yakajitokeza makampuni

mengine 26 yakasema bado yana magogo. Wizara yangu ika-*commission, commission* ya wataalam kwenda kufanya tathmini juu ya magogo yanayosemwa na kuangalia katika maeneo mbalimbali kuona hali halisi ilivyo. Baadaye wakaruhusiwa kusafirisha magogo hayo. Lakini hivi leo kuna bado makampuni matano yanalalamika yanataka yapewe ruhusa ya kusafirisha magogo. Kinachoonekana ni kwamba makampuni haya yalipoona kwamba vibali vinatolewa yanarudi msituni yakikata miti ili yalalamike na kupewa kibali. Kwa hiyo, nimepewa agizo kwamba wataalam waangalie na kweli kuhakikisha kwamba magogo yanayosemwa ni yale yanayoruhusiwa ya aina ya *paurosa* na tiki peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa hapa kwamba mwaka 1985 alipokuwa Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Getrude Mongella alikwenda Ujerumani akawaeleza kwamba kwetu hakuna hoteli huku. Katika kutangaza Utalii hapa nchini kwetu bado tunalo tatizo la vitanda vya kutosha katika hoteli zetu. Aidha, bado tunalo tatizo la kuangalia ukubwa wa hifadhi zetu, nafasi ya kujenga hoteli na kuangalia maeneo yanayozunguka hifadhi zetu na kuyaweka kama maeneo maalum ya ujenzi wa hoteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi yetu ya Serengeti peke yake ni kubwa kuliko nchi ya Belgium. Katika hifadhi hiyo, sasa kuna hoteli tano pekee. Sasa katika eneo ambalo ni kubwa kuliko Mkoa wa Kilimanjaro hoteli tano kwa kweli ni chache sana na kusema kwamba zinaweza kuharibu *eco system* yote ni ku-*exagurrate* kidogo. Kinachotakiwa ni kuangalia upya *general management plan* za hifadhi hizi na kuangalia maeneo ambayo tukiongeza ujenzi hayataingilia taratibu za *eco system,* taratibu ya wanyama na jinsi wanyama wanavyopita na kutembea katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Aidha, ni vizuri tukawa wazi, tukaangalia na maeneo yanayozunguka hifadhi hizi ili na zenyewe zitoe nafasi ya kujenga hoteli ili watalii wanaokuja waweze kupata mahali pa kukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa rai hapa kuhusu biashara ya uwindaji wa utalii na mimi nakubaliana na wasemaji waliopita kwamba tunayo kazi ya kufanya ya kuhakikisha kwamba uwindaji wa kitalii unaleta faida kwa nchi yetu. Aidha, wakati huu tunafanya juhudi kubwa kurekebisha kasoro muhimu zilizopo. Aidha, tunarekebisha ukubwa wa maeneo ya uwindaji, maeneo mengine ni makubwa sana hata kupita Wilaya yangu na Jimbo langu la Uchaguzi. *(Makofi)*

Kurekebisha malipo ya uwindaji, kurebisha malipo ya trofi ambazo zinachukuliwa na kuweka taratibu ambazo zitamruhusu mtu kuwinda wanyama adimu. Kwa mfano, hatutaruhusu mtu kuwinda simba kama hakwenda safari ya utalii inayozidi siku 21 na kwa sababu si kila siku ya utalii ni dola 400 basi itabidi alipe gharama ya kukaa kwenye safari hiyo kwa siku 21 ndiyo aweze kumwinda simba. Aidha, hatutaruhusu mtu kuwinda simba na tembo katika safari moja na tunafanya marekebisho ambayo yatahakikisha kwamba mapato kutoka kwenye biashara ya uwindaji yataongezeka kuanzia kiwango cha sasa cha dola milioni nane mpaka milioni kumi kwa mwaka na tunategemea kwamba itafika milioni 30 mpaka 35 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa pia rai katika ripoti hii juu ya utafiti katika taasisi yetu ya utafiti ya *TAWIRI.* Napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba utafiti wa wanyamapori ni kuwaelewa wanyamapori wenyewe, makazi yao, chakula yao,

miili yao na jinsi wanavyohusiana wenyewe katika jamii zao na katika jamii za wanyama aina mbalimbali, magonjwa yao na vitu ambavyo vinaathiri kukua na kupendekeza kwa madhari yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, siyo ripoti zote zinazotokana na utafiti wa namna hii zinaweza kuletwa mbele ya Bunge. Aidha, ripoti muhimu za kueleza kazi za Taasisi kama *TAWIRI,* mahesabu ya mwaka na uzuri wake baada ya kukaguliwa ndiyo mambo muhimu sana katika hili. Aidha, taasisi pia inafanya kazi kubwa ya kuhesabu wanyama wa aina mbalimbali ili kuhakikisha kwamba kota zinazotolewa za uwindaji, matumizi mengine ya maeneo ya wanyamapori yanafanywa kwa makini. Aidha, ripoti hizi zinatolewa katika warsha, makongamano na katika vipindi vya Redio na Televisheni. Ni kwamba kuna tatizo la bei ya samaki katika Ziwa Victoria. Tatizo hili tumeanza kujadiliana kati ya Wizara, wenye viwanda pamoja na wauzaji wa samaki. Tunagemea kwamba kabla ya muda mrefu tatizo hili litakuwa limemalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi sana ambayo yako kwenye ripoti hii na Wizara yangu inawashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuiweka ripoti hii kwa pamoja na ninategemea kwamba kila Mheshimiwa Mbunge atakuwa na fursa ya kuisoma ripoti hii ili aelewe shughuli za Kamati hii lakini pia kazi ambazo zinafanywa na Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ili na yeye aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI – MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuweza kuhitimisha hoja iliyo mbele yetu. Ningeanza kwa kuwashukuru sana waliochangia kwa kusema ambao ni pamoja na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Anthony Diallo na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Suaan Lyimo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema ripoti yetu hii ni ya kazi za mwaka mmoja, mwaka 2006 na kama mnavyofahamu Kamati hii inasimamia Wizara mbili moja ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ambayo Waziri wake ni Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na nyingine ni ya Maliasili na Mazingira, ambayo Mheshimiwa Waziri wake ni Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe.

Kwa hiyo, tuna maprofesa pande zote mbili. Lakini na sisi Kamati yetu inaye Profesa Mwalyosi, kwa hiyo, mzani ume-*balance.* Tunawashukuru sana Waheshimiwa

Mawaziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa msaada mkubwa ambao tumekuwa tukipata. Kamati imefanya kazi bila matatizo yoyote yale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, michango ni mingi na yote imekuwa ni mizuri na baadhi nashukuru baadhi ya hoja zimejibiwa na Waheshimiwa Mawaziri kama hoja za Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, kuhusiana na masuala ya mifugo kule Lindi. Lakini pia suala la mgao wa asilimia 25 naamini Wizara italifanyia kazi ili wale Wabunge wanaotoka katika maeneo ambayo asilimia 25 inahusiana nao basi waweze kupata takwimu halisi zenye mchanganuo wa kila kitu kwa sababu naamini zipo na Wilaya hizi zinapaswa kushukuru sana Serikali kwa vile ambavyo Serikali inaweza kutoa asilimia 25 ya kilichopatikana ikawarudishia wananchi wa maeneo yale. Ni mfano mzuri ambao ndiyo Bunge tunapigania mara kwa mara na maeneo mengine nayo utaratibu huu uweze kuigwa.

Kuhusu njia za wanyamapori, Mheshimiwa Mgana Msindai, alilizungumzia ambazo ni muhimu sana kwa uhai wa hifadhi. Hifadhi za wanyamapori huwa siyo visiwa. Ni vigumu sana hifadhi moja ikakaa peke yake na nyingine ikakaa peke yake. Huwa zinaunganishwa na njia ambazo wanyama hupita wakati kwa wakati katika mwaka na hii inawezesha bayonuwai ya pande mbili kukaa sawasawa, vinginevyo ikishakuwa ni kisiwa basi uwezekano wa wanyama hawa kuwepo miaka 100 ijayo unazidi kuwa mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba Wizara inayo mikakati wakisaidiana na Wizara ya Ardhi, ili kuhakikisha kwamba maeneo haya ambayo ni muhimu sana kama njia za wanyama hayatazibwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya watu kama njia za wanyama kwa Ngorongoro, Serengeti, Loliondo, Mbulu, Karatu, Yaeda Chini, *West Kilimanjaro*, ukilinganisha na wanyama wanaokwenda Amboseli. Lakini vile vile maeneo ya Tarangire na hifadhi nyingine nyingi zina njia za wanyama ambazo ni vizuri tukaweka taratibu nzuri za kuhakikisha kwamba njia hizo hazizibwi. Taratibu mojawapo ni uwanzishwaji wa alichokisema Mheshimiwa Waziri wa *WMA,* maeneo ya uhifadhi kwa wananchi, ambayo wananchi watafaidika nayo.

Lakini vile vile patakuwa na faida ya wanyama kuweza kupita katika maeneo hayo bila kuzuiwa. Mheshimiwa Mgana Msindai alizungumzia pia kuhusu masuala ya uwindaji wa kitalii na Mheshimiwa Waziri mhusika ameyazungumzia vizuri. Ningeongeza neno moja tu kwamba Mheshimiwa Anthony Diallo aliwahi kuunda Kamati Maalum ya kufuatilia na kutoa mapendekezo kuhusiana na suala zima la uwindaji wa kitalii na Kamati hiyo ilimuhusisha Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na mimi ninayeongea hapa nilikuwa Mjumbe wa Kamati hiyo na Kamati hiyo ilifanya kazi nzuri sana na Kamati hiyo iliweza kupita katika nchi karibu zote za Kusini mwa Afrika ikiwa ni pamoja na Namibia, Zimbabwe, Msumbiji, Zambia, nchi zote hizi ambazo wanafanya uwindaji wa kitalii na *South Africa* yenyewe.

Kwa hiyo, ikatoa mapendekezo mazuri sana ambacho ningeweza kumshauri Mheshimiwa Waziri, Profesa Jumanne Maghembe ni kuipata ripoti hiyo na kuangalia mapendekezo yale ambayo yana nia njema ya kuboresha sekta nzima ya Uwindaji wa Kitalii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Paul Kimiti alitoa mapendekezo yake ambayo tunayakubali na nilishawasilisha kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu kupewa kipaumbele vivutio vya utalii katika Mkoa wa Rukwa ikiwa ni pamoja na Msitu wa Mbizi, eneo la *Kalambo Falls* na *Bizima Point* kule Kasanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungewaomba na Waheshimiwa Wabunge wengine wenye maeneo ambayo yana vivutio vya kipekee tuwasiliane na Kamati yetu, tuwasiliane na Wizara ya Maliasili na Utalii ili tuweze kuona namna ambayo tunaweza tukaboresha vivutio vyetu vikaweza kutembelewa na watalii. Lakini watalii ili wazidi kuwa wengi wanaotembelea nchi yetu lazima utalii utangazwe vizuri nje na kutangaza utalii nje ya nchi huwezi tu kutoka na *brief case* yako unakwenda Ulaya unasema unatangaza watalii waweze kuja katika nchi yetu, ni ngumu sana au kuvutia wawekezaji watakaokuja kuwekeza katika sekta ya Utalii. Huwezi kuondoka tu wewe ni tajiri fulani hapa Tanzania basi unaondoka tu unakwenda kule. *(Makofi)*

Tunaye Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, hapa siku moja akipata nafasi, anaweza akatueleza. Ni vigumu sana, wazungu wale wana mageti makubwa, wana majumba, wanakaa huko ndani, si rahisi hata kuwapigia simu. Huwezi kufika kama tunavyofanya sisi kwenye Ofisi zetu, hodi, hodi, hodi, karibu, mimi nimekuja bwana, natafuta mwekezaji, utampata wapi. Ndiyo maana wakati fulani nilimshangaa mtu mmoja akawa analaumu ziara za Rais wetu au viongozi wetu wa Kitaifa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais au Waziri Mkuu au kiongozi wa Kitaifa, Mawaziri wanapoenda nje ya nchi, inakuwa ni *news* katika nchi ile, ni habari tosha. Vyombo vya habari, televisheni, magazeti, redio za huko na kadhalika, zinabeba habari zile katika kurasa zake za mwanzo. Kwa hiyo, nchi yetu inakuwa katika ramani ya nchi ile na wananchi wa nchi ile wanasikia habari za nchi inayoitwa Tanzania. Kwa namna moja au nyingine ni njia moja rahisi zaidi ya kupata wawekezaji, ya kupata watalii, kutumia ziara hizi vizuri zaidi. Zina faida kubwa sana. Vyombo vyote vya habari vinabeba habari zile, vile vikubwa. Ni kama viongozi wa nje wanapokuja katika nchi yetu sidhani kama inakuwa siri kwa ziara za Kiserikali. Wote tunakuwa tunajua kuna mgeni fulani anaingia, magazeti yote yanaeleza na wananchi wanampokea na kadhalika. Inaisaidia nchi yetu na wananchi wetu kujua kuhusu nchi ile. Kwa hiyo, tutumie fursa hizi ambazo tunazo na niishukuru sana Serikali kwa utaratibu huu ambao wamekuwa wakichukua wafanyabiashara, ambao wamekuwa wakichukua watu wanaohusiana na masuala ya matangazo ya utalii na hata Mheshimiwa Waziri wetu wa Maliasili na Utalii mara kadhaa amekuwa kwenye safari hizi. Ni jambo ambalo litatusaidia sana katika kuboresha na kuimarisha utalii wetu.

Waheshimiwa Wabunge, katika wiki mbili, tatu zijazo kutakuwa na ujumbe ambao tulijulishwa na Mheshimiwa Waziri utatoka Kenya na Uganda wa Serikali kuja kujifunza Tanzania wanafanyaje katika masuala ya hifadhi ya maliasili na utalii kwa vile ambavyo rasilimali zimeisha kwao. Mimi niliwahi kutembelea Kenya wakati fulani, nikatembelea mbuga ya *Tsavo National Park. National parks* za Kenya ni tofauti sana na *National Park* za Tanzania. Ukifika kwenye Hifadhi ya Taifa ya Tanzania unakutana na wanyama kuanzia kwenye geti wa kila aina. Kule *Tsavo National Park* wameweka mabango na kwenye hoteli wameandika kwa tafsiri yake kwa kifupi kwa Kiswahili wanasema, wanyama wa hifadhi hii ni vigumu sana kuwaona, kwa sababu wana-*blend* na

*environment* na wanyama wale rangi zao na misitu na nini wanafanana nayo sana kiasi kwamba inafurahisha sana ukiweza kumwona mmoja. Ni mbinu kwamba wanyama wameisha. Ni mbinu ya kumweleza mtalii kwamba wewe hukuwa makini sana katika kutazama, wako lakini wewe ongeza umakini. *(Kicheko)*

Lakini sisi wanyama bado tunao wengi kabisa wa aina mbalimbali katika hifadhi zetu. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwamba uhifadhi huu unaendelea katika utaratibu huu na tunaamini utaendelea vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Phillip Marmo alikuwa amezungumzia umuhimu wa kuongeza idadi ya wawindaji bingwa, wanaitwa *professional hunters.* Jambo hili ni muhimu na ni zuri. Kwa sababu katika ma-*professional hunter* ambao wanawinda katika nchi yetu wanawindisha watalii ambao ni kama 250 hadi 300 Watanzania hawafiki hata 30 ni chini ya hapo. Ukizungumza na wenye makampuni haya kwa nini Watanzania hawako katika kada hii ya *professional hunting* ni kada moja nzuri, *professional hunter* anapowindisha mgeni siku 21 kila siku moja analipwa si chini ya dola 300. Ni kipato kizuri.

Lakini wako wenzetu Watanzania ni wachache sana. Sasa mara nyingi makampuni haya husema kwamba ni kwa sababu Watanzania hawana mila na desturi za kuweza kuishi na mgeni mzungu. Hawana mazungumzo ya kuzungumza naye. Hawajui jinsi ya kuishi na huyu mtu, anatakiwa aishi naye kwa karibu. Ndiyo maana utamaduni wao hawa, kwa hiyo tunashauri kabisa Wizara kukitumia Chuo cha Mweka ambacho ni Chuo cha Kimataifa kutoa mafunzo maalum kabisa kwa *professional hunters* ili waweze ku-*cope* na wageni hawa ili nyanja hii isiwe ni nyanja ya wageni peke yake, Watanzania nao wawe ni sehemu ya watu wa kufaidika na uwanja huu wa wawindaji bingwa. Lakini pia tunashauri Idara ya Wanyamapori kwa mtihani ambao wanatoa kwa wawindaji bingwa wanaowinda Tanzania basi mtihani huo uwe wa Kiswahili itasaidia sana kuwawezesha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, ametoa masikitiko yake makubwa sana kuhusu uchafu kutoka katika miji ya Bukoba, Mwanza na Musoma na miji mingine midogo midogo ambayo inapakana na Ziwa Victoria, Bunda, Magu na kadhalika ambayo inazalisha uchafu mwingi sana kutoka katika matumizi ya wananchi wa kawaida na viwanda ambao uchafu ule unamwagwa katika Ziwa Victoria. Tumekwishalizungumza hili, tuliwahi kutembelea Kamati yetu Ziwa Victoria na tumejionea wenyewe hali halisi ya Ziwa mpaka hata rangi ya maji imebadilika kwa kiasi kikubwa. Tumeshauri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba udhibiti wa uharibifu wa mazingira unakuwa ni kigezo muhimu cha kuruhusu viwanda katika maeneo hayo na tumewaomba sana Shirika, ndugu zetu wa *NEMC* waangalie sana viwango vya uchafuzi wa mazingira katika maeneo hayo ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Kamati yetu iliwahi kutembelea maeneo mbalimbali kama tulivyoeleza. Katika Halmashauri nyingi ambazo tumeweza kupita ni nadra sana tumekuta utekelezaji wa wito wa Serikali wa kuanzisha vitalu vya miti ili kupanda miti milioni moja kwa kila Wilaya au zaidi. Tunatoa wito wa kipekee kabisa kwa Halmashauri zetu zote kuwa na vitalu vyenye miche ya kutosha inayozidi milioni moja kwa kila Halmashauri ili tuweze kupanda miti katika nchi yetu tuitikie wito wa Rais wetu, tuitikie wito wa Wizara, tupande miti kila mahali kadri inavyowezekana. Ningependa kutoa wito kwa

Waheshimiwa Wabunge katika ziara zenu Majimboni, kila Mheshimiwa anayefanya ziara majimboni katika wakati ambao ni muafaka kwa kupanda miti moja ya shughuli yake iwe ni kupanda miti. Litakuwa ni jambo jema na litasaidia sana katika suala zima la hifadhi ya mazingira. Kwa mara ya mwisho, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, niwashukuru Wabunge wote, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara zote mbili, tuwashukuru Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wao na wasaidizi wao wote ambao wamewezesha kazi ya Kamati yetu kuwa nyepesi. Tunategemea ushirikiano huu utaendelea kwa mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono ingawa Mheshimiwa Riziki, amejisahau. Amesimama wakati tayari imeshaungwa mkono. Sasa Waheshimiwa Wabunge, hatua inayofuata ninaomba kuwahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hiyo. *(Kicheko)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira ya mwaka 2006 ilipitishwa na Bunge)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kutangaza rasmi kwamba Bunge limepokea na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hiyo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali izingatie maoni na ushauri uliotolewa na tuitakie kila la kheri Kamati iendelee tena kufanya kazi kwa msimu wa mwaka huu 2007 na tunasubiri tena taarifa ya utekelezaji kwa kadri itakavyopangwa na Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa hatua hizo.

Kabla hatujamalizia kikao chetu kwa sababu *agenda* zilizopo hapa mezani kwangu zimekwisha, ninayo matangazo mawili. Nninalo tangazo moja la Kikanuni. Waheshimiwa Wabunge bado inatupa tatizo kubwa sana kuomba Miongozo ya Spika ama Mbunge anapotaka kutoa taarifa yoyote, ninaomba mjitahidi sana kuipitia Kanuni Namba 55 ile itatoa utaratibu nzuri sana wa kuweza kusaidiana kuongoza vikao vyetu humu ndani na kutoa hoja zetu mbalimbali. Ukiiangalia Kanuni Namba 55 inaeleza taarifa kuhusu utaratibu. Kwa hiyo, Wabunge wengi wamekuwa wakiomba taarifa kwa Mheshimiwa Spika. Sasa ninaomba kusema kwamba Mheshimiwa Spika, haombwi taarifa, yapo maneno yanayotumika kuomba kupewa Mwongozo katika hatua mbalimbali. Kwa mfano unaweza ukatumia neno kuhusu utaratibu ama ukaomba mwongozo wa Spika. Kwa hiyo, ninaomba Waheshimiwa Wabunge tujitahidi kuzipitia Kanuni hizi ili ziweze kutusaidia kushirikiana katika kuongoza vikao vya Bunge na kupeleka maamuzi yetu katika utaratibu wa Kikanuni vizuri zaidi. *(Makofi)*

Lakini pia Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwape pole kwa lililotokea leo. Naona tumemaliza Kikao chetu cha jioni tukiwa na hofu na wasiwasi kwa sababu ya *alarm* ambayo ilikuwa inatuashiria uwepo wa jambo fulani. Kama nilivyosema Kiti

changu kilishashughulikia kujua tatizo ni nini. Kama Spika wa sasa nisingeweza kuthubutu kuwaacha Wabunge katika hali ya hatari ndani ya Ukumbi wa Bunge bila kuelewa nini kinachoendelea. Kwa hiyo, tulishafanya mawasiliano na wenzetu ambao wanazingatia usalama wa Waheshimiwa Wabunge humu ndani na kama nilivyosema kwamba hakukuwa na tatizo lolote lililoashiria kwamba kuna hatari. Kwa hiyo, wenzetu wanaendelea kufanya marekebisho hapa na pale kwa kadri ya kile kilichojitokeza. *(Makofi)*

Mwisho, kesho tutaendelea tena na hatua ya kujadili hoja za Kamati. Hoja za Kamati hizo zitakazojadiliwa kesho, zimeshawekwa ndani ya *Pigeon holes* zetu. Kwa hiyo, ningewaomba wale wote wanaojisikia kuchangia hoja hizo, basi wapitie taarifa hizo kwenye *pigeon holes* ili wapate nafasi ya kuzisoma tayari kwa kuchangia mada hizo kesho. Niendelee kusisitiza maombi ya kuchangia hoja hizo yataanza kupokelewa kesho asubuhi. Haipendezi sana tunapoanza mjadala halafu mtu ndiyo analeta karatasi ya kuomba, inatupa taabu kupanga muda wa kukamilisha shughuli zilizopangwa katika orodha yetu ya kazi za leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa ushirikiano na sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.00 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 7 Februari, 2007 saa tatu asubuhi)*